# BUNGE LA TANZANIA

# MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA TATU

**Kikao cha Arobaini na Tatu – Tarehe 15 Juni, 2016**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Tukae! Katibu.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge wa Kambi Rasmi ya Upinzani Waliondoka Ukumbini)*

**NDG. ZAINAB ISSA- KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Taarifa ya mwaka ya Chuo Kikuu cha Dodoma kwa mwaka wa fedha 2014/2015 *(The University of Dodoma Annual Report for Financial Year 2014/2015)*.

**NAIBU SPIKA:** Katibu!

**NDG. ZAINAB ISSA- KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Amina Saleh Mollel, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 364

**Matatizo Yanayowakabili Watu Wenye Ulemavu Vijijini**

**MHE. AMINA S. MOLLEL** aliuliza:-

Masuala ya watu wenye ulemavu kwa kiasi kikubwa yanazungumzwa na kushughulikiwa katika maeneo ya mijini na kusahau maeneo ya pembezoni ambapo kuna watu wa jamii hiyo.

Je, Serikali ina mpango gani kuhusu watu wenye ulemavu waishio vijijini ambapo matatizo yao ni mengi na makubwa kulingana na jamii inayowazunguka?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu napenda kujibu swali la Mheshimiwa Amina Saleh Mollel, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua changamoto zinazowakabili watu wenye ulemavu waishio vijijini. Ili kuwa na mipango mahsusi ya kushughulikia kundi la watu wenye ulemavu vijijini Serikali imefanya ugatuaji wa shughuli zinazohusu watu wenye ulemavu kwenda katika Serikali za Mitaa. Serikali inaendelea kuzijengea uwezo wa Halmashauri na watoa huduma wengine ili kutatua kero zinazowakabili watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na Sheria ya Watu Wenye Ulemavu Namba 9 mwaka 2010 imeelekeza kuanzisha Kamati za Baraza la Huduma na Ushauri kwa watu wenye ulemavu kuanzia ngazi ya Kijiji, Mtaa hadi ngazi ya Taifa ambazo zitasaidia utoaji huduma kwa watu wenye ulemavu. Katika kusimamia utekelezaji wa matakwa ya sheria hii Serikali imewaagiza Makatibu Tawala wote wa Mikoa kusimamia uanzishwaji wa Kamati za Mikoa, Halmashauri Kata na Vijiji, kutoa huduma kwa watu wenye ulemavu maana ndiko watu wenye ulemavu wengi waliko.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amina Mollel, swali la nyongeza.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na nashukuru pia kwa majibu mazuri kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri katika Wizara husika, nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kutokuwepo kwa takwimu sahihi hasa maeneo ya vijijini kumesababisha kutokuwepo na mipango mahsusi yenye kuleta maendeleo na tija kwa watu wenye ulemavu. Je, Serikali ina mpango gani wa kupata takwimu sahihi za watu wenye ulemavu zitakazosaidia kuwepo kwa mipango mahsusi itakayowasaidia watu wenye ulemavu hasa maeneo haya ya vijijini?

Swali la pili, uwepo wa Sera ya Taifa ya Huduma na Maendeleo kwa Watu Wenye Ulemavu ya mwaka 2004, pamoja na uwepo wa sheria ambayo Naibu Waziri ameitaja Sheria Namba 9 ya huduma kwa watu wenye ulemavu zimesaidiaje kutatua matatizo ya walemavu na Waziri haoni kwamba mfuko wa watu wenye ulemavu ambao ungesimamia Baraza la Watu Wenye Ulemavu kutokutengewa pesa kutasababisha jitihada na mafanikio kwa watu wenye ulemavu yasiwepo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji wake, lakini kwa namna ambavyo amekuwa akitetea na kutushauri hasa katika mambo yanayohusu watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lililoulizwa hapa ni Serikali ina mpango gani kupata takwimu halisi za watu wenye ulemavu. Serikali tayari imekwishaanza mchakato na wameshazindua utaratibu wa kuanzisha kanzidata ambayo itasaidia kupata takwimu sahihi ya watu wenye ulemavu katika maeneo yote ya mijini na vijijini. Lengo kubwa la kanzidata hii itatusaidia pia kuwatambua watu wenye mahitaji hasa watu wenye ulemavu katika maeneo ya vijijini na kushirikiana na Kamati zile ambazo zimeundwa kuanzia ngazi ya Kijiji, Mtaa mpaka Halmashauri ili iwe rahisi kuweza kuwatambua na pia iwe rahisi kuweza kuwasaidia katika kutatua changamoto zao mbalimbali ambazo zinawakabili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la pili ameuliza Sera na Sheria Namba 9 ya mwaka 2010 imesaidiaje kutatua changamoto na kero ambazo zinawakabili watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikiri kwamba uweo wa sheria hii kwanza kabisa imetengeneza msingi na imetengeneza haki za walemavu na sasa sheria hii imekuwa ndiyo sehemu nzuri na *platform* ya kuweza kusaidia Serikali katika kutimiza matakwa yake mbalimbali ya kusaidia watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma katika Sera ya watu wenye ulemavu ya mwaka 2004 imezungumza moja ya jambo ambalo Serikali imeshaanza kulifanyia kazi hivi sasa, changamoto kubwa sana ya watu wenye ulemavu ilikuwa ni upatikanaji wa vifaa vyao ambavyo gharama imekuwa kubwa hasa kutokana na kodi ambayo imekuwa ikitozwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukifuatilia katika hotuba ya Waziri wa Fedha ambayo aliwasilisha hapa Bungeni Hotuba Kuu ya Serikali ukurasa wa 50, Mheshimiwa Waziri ameainisha bayana kabisa kwamba Serikali sasa inaandaa utaratibu wa kuondoa kodi na kuweka msamaha wa ushuru katika vifaa vyote ambavyo vinawahusu watu walemavu lengo lake kubwa ni kuhakikisha kwamba huduma hizi zinawafikia kiurahisi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia katika sheria yetu, Sheria Na. 9 ya mwaka 2010 ukiangalia kifungu namba 30 mpaka kifungu namba 34 kimezungumza wazi namna ambavyo watu wenye ulemavu na wenyewe wanapaswa kupata fursa za ajira katika taasisi za umma na taasisi binafsi. Kwa hiyo, naamini kabisa uwepo wa sheria na sera imechangia sana katika maendeleo ya watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kangi Lugola

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipa nafasi kuuliza swali dogo la nyongeza.

Majibu ya Serikali kwa kweli yanawakatisha tamaa walemavu na hasa ambao wako vijijini. Kwa sababu Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba hii Sheria Namba 9 ni tangu mwaka 2010, lakini leo katika majibu yake ya msingi ndiyo anatamka mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba Serikali sasa inawaagiza watendaji waharakishe kuunda Kamati za Walemavu Vijijini.

Je, kama Mheshimiwa Amina Mollel asingeuliza swali hili leo ina maana Serikali haikuwa na mpango wa kuwaagiza watendaji kwa ajili ya uharakishaji wa uundaji wa hizi Kamati za Walemavu kule Vijijini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE WALEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwanza kabisa naomba nimshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa katika swali la msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo kweli kwamba Serikali haijaanza kutekeleza Sheria Namba 9 ya mwaka 2010 ambayo inasimamia huduma kwa watu wenye ulemavu. Naomba nikuhakikishie wewe binafsi na Bunge lako Tukufu kwamba haya yote ambayo mnaona yamekuwa yakiendelea, yanayowagusa watu wenye ulemavu katika nchi yetu ya Tanzania ikiwemo upunguzaji wa gharama ya vifaa vyao; ikiwemo namna tofauti ya kuhakikisha kwamba elimu inakuwa *inclusive* kwa watu wenye ulemavu katika nchi yetu ya Tanzania, ikiwemo namna ya kuunda Mabaraza hayo kwenye maeneo yetu ya Halmashauri zetu ndani ya Serikali za Mitaa. Ni utekelezaji wa sheria hiyo, ninaomba tu niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge mipango yote ipo na imeshaanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu cha msingi hapa wote kwa pamoja sasa na hasa tunapokaa katika vikao vyetu vya Mabaraza ni kuendelea kuona kwamba yale maagizo ambayo tumeshayaweka na kuyateremsha kwenye Serikali za Mitaa ni kuhakikisha kwamba yanatekelezeka na kama mnaona kuna tatizo mtupe taarifa ili tuweze kusimamia zaidi. Lakini naomba niwathibitishie kwamba sheria hiyo hiyo imeanza kufanya kazi na sisi kama Serikali tumekuwa tukiisimamia na siyo tu tumesubiri swali hili la Mheshimiwa Amina Mollel. Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Rose Kamili Sukum, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Ezekieli Maige.

Na. 365

**Upotevu wa Fedha za Ruzuku ya Chakula**
**Shule za Bweni Wilaya ya Hanang**

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE (K.n.y MHE. ROSE K. SUKUM)** aliuliza:-

Serikali ina utaratibu wa kutoa fedha kwa ajili ya shule za bweni nchini. Kwa kipindi cha kuanzia tarehe 31/08/2013 hadi tarehe10/02/2014 Halmashauri ya Hanang ilipokea kutoka Serikali Kuu kiasi cha shilingi 508,779,500 kwa ajili ya chakula cha shule za bweni. Taarifa zinaonesha kwa fedha zilizotumika kununua chakula ni shilingi 225,585,000 kwa takwimu hizo bakaa ni shilingi 283,194,500 kwa mujibu wa Mkaguzi, bakaa hiyo haionekani kwenye *account* yoyote benki.

(a) Je, fedha hizo zinarudishwa Hazina bila ya kuwa na uwepo wa nyaraka zozote toka Halmashauri kuonesha muamala unavyofanya kazi?

(b) Je, kama fedha hizo hazikurudishwa Hazina nani anaweza kuidhinisha matumizi bila ya mpango wake kupitishwa na Kamati ya Fedha na Mipango ya Halmashauri?

(c) Je, kama fedha zimetumika bila kupangiwa na Kamati halali, ni kwa nini wahusika bado wanaendelea kuwa ofisini bila ya kufunguliwa mashtaka ya wizi wa kuaminika?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rose Kamil Sukum, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014 Halmashauri ya Wilaya ya Hanang iliidhinishiwa shilingi 225,585,000 kwenye ruzuku ya uendeshaji wa shule za msingi kwa ajili ya chakula cha wanafunzi kwa shule za bweni za Katesh, Balangdalalu, Bassodesh na Gendabi. Fedha zilizotolewa zilikuwa ni shilingi 508,779,500 zikiwa ni ziada ya shilingi 283,194,500. Fedha hizo hazikurejeshwa Hazina badala yake zilibadilishwa matumizi na kutumika kwa ajili ya vifaa vya shule na ukarabati wa shule hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizo zilizoombewa kibali cha kubadili matumizi ili zitumike kununua vifaa vya shule na ukarabati wa mabweni. Hata hivyo ni kweli maombi hayo hayakujadiliwa katika Kamati ya Fedha na Mipango na kwa mantiki hiyo utekelezaji wa jambo hilo ulikiuka misingi na utaratibu wa uendeshaji wa Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na makosa hayo Mkurugenzi wa Halmashauri amesimamishwa kazi pamoja na Watumishi wengine wanne wakiwepo Afisa Mipango Wilaya, Mweka Hazina Wilaya na Wahasibu wawili ili kupisha uchunguzi. Aidha, Baraza la Madiwani limeelekeza fedha hizo zirejeshwe kupitia mapato ya ndani na tayari shilingi milioni 130 zimepelekwa kwenye akaunti ya vijiji vya Gendabi, Bassodesh, Katesh na Balangdalalu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ezekiel Maige, swali la nyongeza.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba niipongeze Serikali kwa kupeleka fedha hizi kwenye shule za bweni zilizoko kwenye Wilaya ya Hanang. Pamoja na hatua hiyo nzuri na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nilikuwa naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Swali la kwanza, kwa kuwa wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Msalala kwa kushirikiana na Mbunge wao wamefanya kazi kubwa sana ya kujenga shule pamoja na hosteli kwenye shule za Isaka, Baloha, Mwalimu Nyerere, Lunguya pamoja na Busangi. Lakini shule hizi au hosteli hizi hazitambuliki kabisa na Serikali kwa maana ya kutolewa au kupewa msaada wa aina yoyote kama inavyofanyika kwa wenzao wa Hanang. Je, Serikali inaweza sasa ikaziingiza shule hizi kwenye mpango wa kupatiwa huduma ya chakula kama ilivyofanyika kwenye maeneo mengine nchini?

Swali la pili, kwa kuwa tatizo la mabweni kwenye shule nyingi za sekondari za kata ni kubwa sana hasa kwenye shule zilizoko kwenye maeneo ya wafugaji ambao wengi wao wanaishi kwenye maeneo ya pembezoni na yenye mazingira magumu, na kwa kutambua mazingira hayo wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Msalala kwa kushirikiana na Mbunge wao wameanza juhudi au wanaendelea na juhudi za kujenga hosteli kwenye shule ambazo bado hazijapata ikiwemo shule za sekondari za Isakajana, shule za sekondari za Ngaya pamoja na zingine.

Je, Serikali inaweza ikachangia namna gani au ikaunga mkono namna gani juhudi hizi nzuri za wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Msalala pamoja na Mbunge wa eneo hilo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimpongeze Mbunge huyu pamoja na wananchi wake kuhakikisha kwamba wamejenga hosteli katika shule hizo za kata, lengo kubwa ni kuhakikisha kwamba vijana *especially* wa kike au wanafunzi wa kike waweze kusoma katika mazingira rafiki. Mheshimiwa Maige nakumbuka kwamba tulikuwa pamoja katika gari yangu tukisafiri kutoka Msalala pale Mjini tukaenda mpaka kule Bulyanhulu, kwa hiyo ninalijua vizuri jiografia ya eneo lako. Naomba nikupongeze katika harakati kubwa ulizofanya na wenzako wa kule Msalala.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi lako katika eneo la kwanza ulikuwa unaomba kwamba ikiwezekana shule hizi sasa ziingizwe katika utaratibu mwingine wa Kiserikali sasa vijana wa maeneo haya waweze kupewa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchakato wetu mpana tulioufanya na hili nimezungumza katika vipindi tofauti kwamba lengo kubwa lilikuwa kwanza programu ya kwanza ni ujenzi wa shule za kata, lakini suala lingine la pili inaonekana kwamba vijana wengi wanaoenda shule za kata wanapata ushawishi mkubwa sana kurubuniwa katikati tumejikuta kwamba vijana wengi wanapata ujauzito.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeelekeza maeneo mbalimbali kwamba zile shule za Kata zilizojengwa angalau ikiwezekana wazazi waone kama kutakuwa na utaratibu wa ujenzi wa mabweni ili kuweza kuwa- *accomodate* vijana katika mazingira ya karibu zaidi na shule. Jambo hili naomba nishukuru karibu Tanzania nzima limefanyika kwa upana mkubwa zaidi, lakini kuna shule maalum za bweni ambazo zinatambuliwa na Serikali, lakini kuna zile zingine hosteli zimejengwa na wananchi wenyewe. Tunachokifanya sasa hivi Serikali ni kumebainisha zile shule ambazo ziko katika mkakati wa Kiserikali kama tunavyozijua zile shule za Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hivi sasa siwezi kuzungumza wazi kwamba kusema kwamba shule zote ambazo mabweni yamejengwa kwamba zitapewa chakula jambo hilo litakuwa ni jambo la uongo. Isipokuwa Serikali tunaangalia jambo hili kwa uzito wake na kufanya tathmini ya kina basi hapo baadaye kama tulivyoenda na programu ya elimu bure katika *analysis* ya kutosha hapo baadaye kuzibainisha baadhi ya shule tuzi - *upgrade* ziwe *special* shule za hosteli jambo hili Serikali hatutosita kuliangalia lakini jambo kubwa hilo tutafanya *analysis* kwa nchi nzima tutafanyaje kazi kuhakikisha mazingira bora yanatengenezwa kwa vijana wetu wasichana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sehemu ya pili ni kwamba kuna baadhi shule zingine bado hazijapata hosteli, naomba nikuunge mkono tena kwamba endelea na juhudi ile ile. Lakini naomba nikuahidi kwamba katika mipango yenu ya Halmashauri ikiwezekana ninavyofanya mchakato wa bajeti za Halmashauri wekeni vipaumbele hivyo na Ofisi ya Rais, TAMISEMI nia yake itakuwa ni kuweza kusukuma juhudi hizi za wananchi ifike muda kwamba shule zote ambazo zina changamoto kubwa tuweze kusaidia zipate mabweni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema awali lengo kubwa ni kwamba vijana wetu hasa wasichana watakuwa wanakwepa hivi vishawishi ambavyo vimekuwa ni tatizo kubwa sana na likiwagharimu vijana wengi kupata ujauzito.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hongoli.

**MHE. JORAM I. HONGOLI**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, shule hizi za bweni zimekuwa zikipelekewa fedha shilingi 1,500 kwa siku kwa mwanafunzi. Je, nilitaka kujua ni lini Serikali itaongeza hizi fedha ili shule zetu za bweni zisifungwe mapema na kuchelewa kufunguliwa ili watoto wapate muda mwingi wa kusoma wakiwa shuleni? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu mafupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, anachozungumzia ni *unit cost* ya chakula kwa mwanafunzi, na *concern* hii nadhani Wabunge wengi walikuwa wameelezea kusema na hii *rate* ya shilingi 1,500 ni ndogo. *Unit cost* siyo kwa ajili ya chakula peke yake isipokuwa kwa ajili ya mchakato mzima wa elimu, jambo hili watalamu wetu sasa hivi wanalifanyia kazi pale litakapokamilika tutaangalia ni jinsi gani kama kuna uwezekano kupandisha gharama hii kidogo ili mtoto apate lishe ya kutosha ya kuweza kumfanikisha aweze kupata masomo vizuri. Kwa sababu tunajua kwamba suala la lishe ni jambo la msingi sana kujenga akili ya mtoto.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge ni kwamba jambo hili tunalifanyia kazi sasa hivi kuangalia *unit cost* kwa shilingi 1,500 ni kweli tutafanyaje sasa na iende mpaka kiasi gani kwa kuangalia uwezo wa Serikali kwa muda muafaka.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi hii.

Kwa kuwa, Wilaya ya Hanang ni Wilaya ya wafugaji, na wananchi wamejitahidi sana kujenga hosteli kama ya shule ya Mreru, Mulbadau, Endasak na kwa kufuatia suala hilo; je, Serikali ipo tayari kusaidiana na wananchi, kuona kwamba zile hosteli na mabweni yaliyokuwepo toka wakati wa uhuru, tunaimarisha na kuboresha miundombinu ambayo ipo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge *senior* katika Bunge hili amesema jinsi gani Serikali itaboresha hizi shule, ni kweli shule ambazo zimejengwa muda mrefu lazima tuangalie ni jinsi gani tutaboresha miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nilikuwa katika Chuo cha Kigurunyembe, nimepitia shule mbalimbali. Kuna baadhi ya shule zamani zilikuwa zinafanya vizuri zaidi, lakini kutokana na uchakavu wa miundombinu ufanisi wake umekuwa chini sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipotembelea shule ya Iyunga kule Mbeya ambayo bweni lake liliungua, nilivyoangalia nikaona ni kwa nini sasa shule nyingi ambazo zamani zilikuwa ni shule za vipaji lakini sasa hivi uwezo wake umekuwa chini, *bunsen banner* iliyokuwa inatumika mwaka 1980, ndiyo inayotumika mpaka mwaka 2017; jambo hili haliwezekani.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge naomba nikuhakikishie kwamba, jukumu letu kubwa ikiwezekana katika Halmashauri tubainishe katika vipaumbele kwa sababu tumekuwa na tatizo kubwa sana la kufanya ukarabati katika shule zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuungane kwa pamoja, tubainishe shule zilizochakaa katika mipango yetu ya Halmashauri katika bajeti tuliweke hili mapema, Ofisi ya Rais TAMISEMI itaweka nguvu kuhakikisha kwamba shule hizi sasa zinakuwa na ubora ili wanafunzi waweze kupata taaluma inayokusudiwa na shule zetu za Serikali ziwe shindani sawa na shule nyingine za *private* katika Jamhuri wa Muungano wa Tanzania.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cosato Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Nashukuru Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuniona, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, na mimi naomba kuuliza swali dogo la nyongeza, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mafinga Mjini.

Katika Jimbo la Mafinga Mjini tuna shule mbili za sekondari za bweni, mojawapo ni shule ya sekondari ya bweni ya Changarawe. Katika kutekeleza majukumu kama wananchi, bodi ya shule kwa kushirikiana na wazazi imeanza na inaendeleza jitihada za kujenga jiko la kudumu na bwalo la chakula kwa ajili ya wanafunzi hao. *(Makofi)*

Je, Serikali kwa kilio changu kile kwamba hii ni Halmashauri mpya ipo tayari kwa kutuongezea nguvu ili kukamilisha jiko hilo la kudumu na bwalo la chakula kwa ajili ya wanafunzi wa Shule ya Sekondari Changarawe?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge anasema ujenzi wa bweni pamoja na jiko katika Shule ya Sekondari ya Changarawe, naomba niseme kwamba nimelisikia hili jambo, Mheshimiwa Cosato Chumi tumezungumza mambo mengi, ukiachia miradi yake ya maji iliyokuwa imekwama amepambana, na hili naomba niseme kwa sababu hapa siwezi kusema kuna bajeti *special* kwa ajili ya bweni hili, lakini katika mchakato wetu, kama tulivyoahidiana kwamba mara baada ya Bunge tutapitia, nitakwenda kukagua Shule ya Sekondari ya Iyunga ambayo ujenzi wa mabweni unaendelea, tutapita kuangalia kwa pamoja, mikakati gani tuifanye ili bweni likikamilika na jiko likikamilika, watoto watakula na kuishi sehemu rafiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hatuoni tatizo katika eneo hilo, lakini ni lazima tushirikishane kwa pamoja tuangalie ni mkakati gani wa haraka utaweza kusaidia katika eneo hili la Shule ya Sekondari ya Changarawe. Mheshimiwa

Mbunge, naomba niseme kwamba jambo hili nimelipokea tutakapokuwa pale *field* tutapanga mikakati ya pamoja lengo ni kuwasaidia vijana wetu.

Na. 366

**Asilimia 10 ya Fedha zinazotolewa kwenye Halmashauri kwa Ajili ya Vijana na Wanawake**

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA** aliuliza:-

Asilimia kumi ya bajeti ya Halmashauri nchini hutengwa kwa ajili ya mikopo ya vijana na wanawake.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kusimamia fedha hizo zitolewe kwa kila Halmashauri?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyojibu hoja hii mara kadhaa hapa Bungeni, Serikali imejipanga kuhakikisha asilimia kumi ya fedha za vijana na wanawake zinatengwa na zinapelekwa kwa njia ya mikopo. Usimamizi wa suala hili uliwekewa mkazo katika mwongozo wa bajeti ya mwaka 2016/2017 ambapo Halmashauri zote zimetenga shilingi bilioni 56.8 kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Vijana na Wanawake kutokana na mapato ya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa Serikali ni kuimarisha makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri kwa kutumia mfumo wa kielektroniki ili kuhakikisha fedha hizo zinatengwa na kupelekwa kwa vijana na wanawake. Maamuzi ya kutenga fedha hizi ni kadri ya makusanyo kila robo mwaka yanafanywa na Halmashauri kupitia Kamati ya Fedha na Mipango na Baraza la Madiwani.

Hivyo, naomba kutoa wito kwenu Waheshimiwa Wabunge wote tushirikiane katika kusimamia suala hili ambalo liko kwenye Halmashauri zetu ili kila tunapofanya maamuzi ya kugawa rasilimali fedha kutokana na mapato ya ndani, tuweke kipaumbele katika kutenga fedha hizo.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa asilimia kumi iliyopo sasa hivi imepitwa na wakati, na wanawake na vijana wanakuwa kwenye makundi ya watu watano, watano, wanagawana hiyo asilimia 10 wanagawana shilingi laki moja, pesa ambayo haiwezi kukidhi matakwa ya mahitaji yao. Je, serikali ina mpango gani wa kuongeza asilimia kumi iliyoko sasa hivi? *(Makofi)*

Swali la pili, kwa kuwa asilimia kumi iliyoko sasa hivi haitoki kwa wakati na wakati mwingine inasubiri matukio muhimu kama vile Mwenge. Je, ni lini Serikali itafanya sasa asilimia hii itoke kwa wakati? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu mafupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Bupe, kwa sababu nimeona akiguswa sana na kinamama na vijana katika maeneo yake. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge hiyo ni *credit* kwako, kwa sababu naona unawatumikia wananchi wako wa Mkoa wa Rukwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema awali asilimia kumi ni mgao katika mapato ya ndani, na asilimia kumi hii inatofautiana kutoka Halmashauri moja na kwenda Halmashauri nyingine. Kwa mfano, Halmashauri ambayo *collection* yake kwa mwezi ni shilingi milioni 200, unapozungumzia asilimia kumi maana yake unazungumzia shilingi milioni 20. Lakini tujue kwamba kiwamba kiwango hiki ni *(own source)* mapato ya ndani ya Halmashauri, na katika yale mapato ya ndani kuna mgawanyiko wa aina mbalimbali kutoka mapato ya ndani, kuna mingine kutoka miradi ya maendeleo, kuna vitu mbalimbali. Kwa hiyo, hii asilimia kumi kiundani ni asilimia yenye kutosha kabisa katika mchakato wa *own source,* kwa sababu ile pesa ya ndani bado kuna mahitaji mengine ya miradi ya maendeleo inatakiwa ifanyike katika Halmashauri.

Kwa hiyo, hii asilimia kumi siyo ndogo, isipokuwa lengo kubwa ni kila Halmashauri iweze kujipanga ikusanye mapato ya kutosha kutoka katika vyanzo vya ndani. Kuna Halmashauri zingine kwa mwezi wanakusanya shilingi milioni 500, asilimia kumi ni shilingi milioni 50; ni imani yangu kubwa kama kila Halmashauri imejipanga vizuri wanapofanya *collection* zao mfano hata shilingi milioni100, asilimia kumi yake ni shilingi milioni kumi, wakiamua kuzigawa zile vizuri, wakipanga mpango mkakati vizuri, zitawasaidia kina mama na vijana katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo letu kubwa lilikuwa pesa tulizozipanga katika *own source ten percent* ilikuwa haiendi kwa akina mama na vijana, na ndiyo maana katika Kikao cha Bunge kilichopita nilisema kwamba kipindi kilichopita *own source* peke yake ambazo hazikupelekwa kwa kina mama na vijana zaidi ya shilingi bilioni 39; maana yake ni kwamba Madiwani na sisi tulivyokuwa katika Kamati ya Fedha hatukutimiza wajibu…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhali naomba ufupishe majibu, tafadhali! *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka angalau kidogo tuelezane hili, suala la asilimia kumi halitoki, nilikuwa nakuja asilimia kumi kutoka maana yake ni maamuzi ya wenyewe Wabunge na Madiwani, ndiyo tunakaa katika Kamati ya Fedha tunapanga kwamba asilimia kumi zitoke. Ina maana sisi tukishindwa kutimiza wajibu wetu, zitakuwa bado haziwafikii vijana, kwa sababu *ten percent* inafanywa katika Kamati ya Fedha ya Halmashauri husika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sikudhani Chikambo swali fupi.

**MHE. SUKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ifahamike kwamba pesa hizi zinatengwa kwa ajili ya kusaidia vikundi vya wanawake na vijana na hasa wale wanaojiunga kupitia makundi mbalimbali. Kwa bahati nzuri nimekuwa Diwani katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru vipindi vinne. Pesa hizi hata kama zikitengwa katika Halmashauri nyingi nchini, kunapojitokeza jambo la dharura kwenye Halmashauri, pesa hizi zimekuwa zikitumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe sasa Serikali itoe tamko kupitia Halmashauri zetu nchini, kunapojitokeza Halmashauri imekiuka utaratibu wa kutekeleza pesa hizi kuwafikia akina mama ni hatu gani sasa zitachukuliwa kwa Halmashauri ambazo zitashindwa kutekeleza? Ahsante *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba kiufupi tu niseme ifuatavyo; sasa hivi ni marufuku kwa Halmashauri yoyote asilimia kumi iliyotengwa kutowafikia vijana na kina mama na ninasema hivi sitanii.

Katika bajeti ya mwaka huu kila Halmashauri imepitishwa bajeti yake mara baada ya kutenga ile asilimia kumi; kwa hiyo Mkurugenzi yeyote na Kamati ya Fedha watakaposhindwa kutimiza wajibu huu wa Serikali, tutahakikisha Halmashauri yao tutaiwajibisha kwa sababu imeshindwa kutimiza

matakwa halisi ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo tumepitisha katika bajeti ya mwaka huu wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Edwin Sannda.

**MHE. EDWIN M. SANNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mazingira ya baadhi ya Halmashauri kuwa upya na changa kama ilivyo Halmashauri ya Mji wa Kondoa, vyanzo vya mapato ya ndani, huwa ni vidogo sana na hafifu; je, Serikali haioni umuhimu kupitia Wizara zake husika zenye dhamana kwa vijana na akina mama kuweka walau ruzuku fulani kufikia ukomo ili iweze kukidhi mahitaji ya vijana na akina mama?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu mafupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tumesema kwanza hii asilimia kumi siyo peke yake ndiyo inayowagusa vijana, katika Ofisi ya Waziri Mkuu, kuna Mfuko wa Uwezeshaji wa Vijana, kwa hiyo, tunachokifanya na lengo mi kwamba vijana na kina mama weweze kupata fursa kutoka maeneo mbalimbali, ninajua Halmashauri nyingine ni changa kama ulivyosema Mheshimiwa kwenye Wilaya yako ya Kondoa, Serikali imejipanga ukiacha *own souce* ya *ten percent,* kuna Mfuko wa Vijana kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, hali kadhalika kwa mujibu wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi, katika Ilani yake imezungumza kwamba kutakuwa na mgao wa shilingi milioni 50, lengo kubwa ni kwenda kusukuma nguvu zile za vijana na kina mama katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya shughuli za uchumi.

Kwa hiyo, nadhani kwamba mpango wa Serikali utaendelea kuboresha ili vijana na akina mama waweze kupata nguvu za kujenga uchumi katika nchi yao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mary Mwanjelwa.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali moja tu dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninaipongeza sana Serikali kwa kutenga asilimia kumi kwa ajili ya wanawake na vijana. Serikali sasa hivi haioni kwamba kuna umuhimu kuhakikisha inawashirikisha Wabunge wa Viti Maalum katika Halmashauri zetu, kwa kuzingatia kwamba mara nyingi pesa hizi haziwafikii walengwa. Washirikishwe kisheria na ikiwezekana washirikiane na

Maofisa Maendeleo wa Miji pamoja na Kamati ya Fedha, naomba Serikali itoe tamko. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, maana nilikuwa naona Mawaziri wanataka kusimama wote kwa pamoja.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani tukifanya *reference* wiki hii nilijibu swali hili siku ya Jumatatu, ushiriki wa Wabunge wa Viti Maalum katika Kamati ya Fedha, na nilizungumza kwa upana kwa ku-*qoute* sheria na vifungu vya kanuni. Nilitoa mifano mbalimbali katika maeneo hayo nikasema wadau watakaa wataona kama inafaa basi tuboreshe sheria zetu na kanuni zetu, hili jambo nililiongelea juzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine kwa sababu nimejua kwamba Mheshimwa Waziri wangu wa Afya alitaka ku-*top up* katika eneo hilo nadhani aongezee katika kipande hicho.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nataka tu kuongeza majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba sambamba na Halmashauri kutakiwa kutenga asilimia tano kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake; Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imetenga shilingi bilioni moja katika bajeti ya 2016/2017 kwa ajili pia ya kuwakopesha wanawake. Kwa hiyo, fedha hizi tutazipeleka katika zile Halmashauri ambazo kwanza zimefanya vizuri, kwa hiyo kigezo ni Halmashauri kutenga za kwako, halafu Wizara yangu itaongeza zaidi ya zile ambazo zimetengwa na Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, kupitia Benki ya Wanawake Wizara pia imetenga shilingi milioni 900 ambazo tutazikopesha kwa wanawake wajasiriamali katika Halmashauri mbalimbali nchini. *(Makofi)*

Na. 367

**Kukamilika kwa Ujenzi wa Nyamagana**

**MHE. STANSLAUS S. MABULA** aliuliza:-

Jimbo la Nyamagana ni jimbo pekee lililochangia mradi wa ujenzi wa nyasi bandia kupitia *TFF* shilingi 160,000,000.

Je, ni lini Serikali itawasisitiza *TFF* kuhakikisha kuwa uwanja huu unakamilika kwa wakati na kuendeleza malengo yaliyokusudiwa?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, Mbunge wa Nyamangana kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, uboreshaji wa uwanja wa Nyamagana wa kuweka nyasi bandia ulianza mwaka 2014 ukiwa na thamani ya dola za Kimarekani 737,886 sawa na shilingi za Kitanzania 1,193,161,662. Shirikisho la Kimataifa la Vyama vya Mpira wa Miguu *(FIFA)* lilitoa msaada kwa Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini *(TFF)* kiasi cha dola za Kimarekani 618,946 sawa na shilingi za Kitanzania 1,000,835,682 na Halmashauri ya Nyamangana ilichangia dola za Kimarekani 118,943 sawa na shilingi za Kitanzania 192,330,831.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyasi hizo bandia zimegharimu tozo kiasi cha dola za Kimarekani 100,121.93, sawa na shilingi za Kitanzania 220,268,400 ikujumuisha *import duty* na *VAT*. *TFF* kama msimamizi wa mpira wa miguu kwa niaba ya Halmashauri ya Nyamangana na Serikali, wameshughulikia mchakato wa kutoa msamaha wa tozo hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyasi bandi tayari zimewasili Dar es Salaam tangu tarehe 17 Aprili, 2016. Baadhi ya vifaa tayari vimeshafika katika Uwanja wa Nyamagana na mkandarasi amekwishaanza kazi ya ukarabati wa uwanja huo. *TFF* sasa wako katika mchakato wa kumalizia kusafirisha vifaa vilivyobaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ukweli kwamba ukarabati wa uwanja wa Nyamagana kuufanya uwe wa nyasi bandia unahitaji umakini mkubwa ili uwe mzuri, imara na wenye hadhi ya Kimataifa ni lazima mkandarasi ahakikishe kuwa ubora wa viwango vinazingatiwa. Kwa vile mpango wa ukarabati huo ulitakiwa ukamilike mwishoni mwa mwezi huu, natoa wito kwa mkadarasi huyo kuhakikisha kwamba ukarabati huo unakamilika haraka iwezekanavyo ili uweze kutumika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stanslaus Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Waziri kwa majibu yake mazuri na kwa mara ya kwanza Wizara hii imeonesha uhalisia wake kwa kutoa majibu kwa vitendo nawapongeza sana.

Pamoja na majibu haya mazuri ya vitendo, Halmashauri ya Jiji la Mwanza kama ambavyo imekuwa ikishiriki kwa asilimia kubwa katika kuboresha michezo,

tayari imeshaandaa ramani ya uwanja mzima na imeshaanza kupita ngazi mbalimbali. Ninataka kupata tu maoni kutoka kwenye Serikali kwamba uwanja huu pamoja na kwamba utakuwa umetengenezwa eneo la kuchezea, lakini bado tutakuwa na changamoto kubwa katika eneo la mzunguko mzima kwa ajili ya kupata vyumba vya wachezaji kubadilishia nguo, lakini jukwaa kuu na maeneo ya kukaa ili uwanja ukamilike na kuwa uwanja wa kisasa. *(Makofi)*

Je, ni lini Serikali itakuwa tayari kusaidia Halmashauri ya Jiji la Mwanza kuhakikisha uwanja wa Nyamagana unakuwa ni wa kisasa na ambao unaweza kutumika na mechi za Kimataifa? *(Makofi)*

Swali dogo la pili tayari vifaa vimeshafika, ni lini ….

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stanslaus naomba hilo swali la pili ufupishe kwa sababu la kwanza umelifanya refu.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini *TFF* waithibitishie Wizara watakuwa tayati kukamilisha uwanja huu maana tumesubiri sana na tunahitaji kuutumia haraka tunavyoweza? Nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa jinsi ambavyo amekuwa mstari wa mbele kuhakikisha kwamba uwanja huu wa Nyamagana unakarabatiwa.

Katika kufuatilia tumebaini kwamba Mheshimiwa Stanslaus Mabula alipopata nafasi ya kuwa Meya tu mwaka 2012 Septemba alihakikisha kwamba anaondoa urasimu wa utoaji wa pesa mwezi Disemba, 2012 na mwaka 2013 mchakato wa kuanza kuagiza nyasi bandia ulikamilika, kwa hiyo nampongeza sana na ninaomba Waheshimiwa Wabunge tuige mfano wa Mheshimiwa Mabula. *(Makofi)*

Swali lake la kwanza ambalo ametaka kujua kwamba ni vipi sasa wanaweza wakakamilisha ule mzunguko mzima wa uwanja, nimhakikishie tu kwamba Wizara yangu ipo tayari kutoa ushirikiano *(technical support)* ili kusudi kuweza kuona kwamba ni jinsi gani sasa vile vyumba au eneo lote linaweze likazunguka, ikizingatia kwamba ni lazima kuwepo na *facilities* kama za vyumba za kubadilishia nguo na vyumba vya waandishi wa habari pamoja na vyumba vya matibabu ili kusudi uwanja huu uweze kukidhi viwango vya Kimataifa. Kwa hiyo, kupitia BMT Wizara yangu itatoa ushirikiano wa karibu sana na ninaomba Halmashauri pia iwe karibu na BMT.

Swali lake la pili sasa kwamba ni lini uwanja huu utakamilika, niseme tu kwamba Serikali inafanya kazi kama timu, kwa sababu nimeshatoa wito mkandarasi afanye kazi haraka, ninaomba Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Mwanza washirikane na Halmashauri, washirikiane na *TFF* ili kumsimamia mkandarasi huyu aweze kukamilisha haraka ujenzi wa uwanja huu. *(Makofi)*

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu ya Naibu Waziri lakini nina swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mwaka Shirikisho la Mpira la Ulimwengu *(FIFA)* huwa linatoa *goal project* kwa nchi kadhaa wanachama wa Shirikisho hilo. Tanzania tumekuwa tukipata *goal project* za viwanja mara nyingi;

Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami sasa wakati umefika kuishawishi *TFF* pale walipopata *goal project* basi safari hii uwanja kama huu wa Mwanza wa kuweka nyasi bandia uelekee Zanzibar?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba *FIFA* huwa ina *goal project* na inatoa *support* ya ujenzi wa viwanja kwa kuweka nyasi bandia kupitia *TFF,* napenda kumtaarifu Mheshimiwa Hafidh Ali kwamba uwanja wa Gombani uliopo Pemba tayari umeshapata msaada wa kuwekewa nyasi bandia kupitia ufadhili wa *FIFA*. *(Makofi)*

Hata hivyo hii haizuii kuna vigezo pia ambavyo vinatakiwa kufuatwa ili kusudi *FIFA* iweze kutoa ufadhili huu. Kigezo kimoja wapo ni kwamba uwanja ni lazima uwe wa Halmashauri, pia uwe ni uwanja ambao unaweze kuchezesha mechi za Kimataifa, vilevile wahusika wa uwanja huu wawe tayari kuchangia asilimia 16. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri kwa mpango huu wa hizi nyasi bandia zinazotolewa, je ni mpango wa kila Mkoa na kama ni kila Mkoa, je, ni lini Mkoa wa Simiyu mtatupa uwanja wa namna hii? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na uwanja wa Simiyu vigezo ni kama nilivyovitaja kama uwanja huu ni wa Halmashauri na unakidhi vigezo vya kuwa wa Kimataifa, *goal project* inaweze ikasaidia, lakini utaratibu ni kwamba *TFF* inaandika orodha ya viwanja vitano na kuandika *details* zake na vinapofika *FIFA* wao wanateua kulingana na ushindani wa kukidhi vigezo vya kutoa msaada. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Bashungwa.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Wananchi wa Karagwe tunamkumbuka Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa *push-up* za kihistoria alizozipiga pale Kayanga. Je, Serikali mnaonaje kama mkitusaidia kujenga uwanja wa Wilaya pale Kayanga ili tuweze kumuenzi Rais wetu kwa ule ukakamavu alioonyesha kwa vijana wa Karagwe? Nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bashungwa mnataka kuanzisha mchezo wa *push-up*, Mheshimiwa Waziri. *(Kicheko/Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kweli kwamba *push-up* kwa mara ya kwanza zilipigwa kwenye eneo ambalo Mheshimiwa Mbunge anasema, hii ilithibitisha uwezo wa Rais John Pombe Magufuli wa afya yake, lakini pia ulionyesha kwamba Serikali atakayoiunda ni Serikali ya Hapa Kazi Tu tofauti na wenzetu mgombea wao nadhani hiyo kazi ilikuwa ngumu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Wizara kwa kushirikana na Halmashauri anakotoka Mbunge tunaweze kuzungumza kuona namna ya kushauriana kuweka kumbukumbu hii muhimu ya Serikali ya Awamu ya Tano kwa kazi nzuri inayofanywa. Kwa hiyo, Wizara na Halmashauri ambapo anatoka Mbunge tutakaa pamoja tuzungumze tuone namna ya kuweka hii kumbukumbu muhimu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mheshimiwa Godfrey William Mgimwa, Mbunge wa Kalenga, sasa aulize swali lake.

Na. 368

**Kupeleka Minara ya Simu Jimbo la Kalenga**

**MHE. GODFREY W. MGIMWA** aliuliza:-

Tatizo la mawasiliano ya simu katika Jimbo la Kalenga bado ni kubwa.

Je, ni lini Serikali itapeleka minara ya simu kwenye vijiji vya Kaning'ombe, Ikungwe, Lyamgungwe, Igunda na Ikuvilo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Godfrey William Mgimwa, Mbunge wa Kalenga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua ukubwa wa tatizo la mawasiliano ya simu katika Jimbo la Kalenga. Kwa kulitambua hilo Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote iliainisha vijiiji vya Kata ya Wasa kikiwemo kijiji cha Ikungwe na kuviingiza katika Mradi wa Awamu ya Kwanza (A). Mradi huu unatekelezwa na Kampuni ya Simu ya *TTCL* kwa ruzuku ya dola za Kimarekani 107,968 ambapo mpaka sasa mnara tayari umeshajengwa. *TTCL* itaanza kutoa huduma za mawasiliano huko Kalenga mwishoni mwa mwezi Juni, 2016 baada ya kukamilisha ufungaji wa vifaa vya mawasiliano katika mnara uliojengwa.

Aidha, vijiji vya Igunda na Lyamgungwe kutoka katika Kata ya Lyamgungwe vimeingizwa katika utekelezaji wa miradi ya mawasialiano ya Viettel katika awamu ya pili na awamu ya tatu iliyoanza Novemba, 2015 na kutarajiwa kukamilika Novemba, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, kijiji cha Kaning'ombe katika kata ya Mseke na kijiji cha Ikuvilo katika kata ya Luhota vitaingizwa katika miradi ya mwaka wa fedha 2016/2017 kupitia mfuko wa mawasiliano kwa wote *UCSAF* kulingana na upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Godfrey Mgimwa swali la nyongeza.

**MHE. GODFREY W. MGIMWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuweka minara kwanza niipongeze sana Serikali kwamba imeendelea kupeleka minara katika Jimbo la Kalenga kwa kasi zaidi. Tatizo ninalolipata ni kwamba baada ya kusimikwa ile minara upatikanaji sasa au uanzaji wa kuanza kupata mawasiliano unatumia muda mrefu sana. Ningependa kujua Serikali ina mkakati gani ili mara baada ya kuwekwa ile minara mawasiliano yaanze kupatikana kwa muda unaostahili. *(Makofi)*

Swali langu la pili, narudi tu kwenye majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba amesema vijiji vilivyotamkwa hapa mwishoni vya Kaning'ombe na Ikuvilo vitapita katika utaratibu wa kupitia *UCSAF* lakini katika tovuti ambayo nimekuwa nikiipitia ya *UCSAF* nitoe tu *statistics* kidogo inaonyesha kwamba kwa mwaka 2015 zilitangazwa zabuni175, Kata zilizopata wazabuni 116 hii kwa ni

Tanzania nzima, idadi ya vijiji 156, miradi kuanza ilikuwa ni Mei, 2015. Lakini katika orodha hii yote hakuna vijiji ambavyo tayari vilishaanza kupatiwa mawasiliano ni *zero,* kupitia mradi ya *UCSAF*.

Ningependa kujua Serikali ina mikakati gani kuhakikisha kwamba inaipa pesa *UCSAF* ili kwamba miradi ambayo imeorodheshwa iweze kukamilika kwa wakati? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mgimwa naomba nikiri kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuwahangaikia watu wake, anafanya hivyo katika maeneo mengi ambayo Wizara yetu inaisimamia ikiwa ni pamoja na barabara, mawasiliano hayo ambayo leo ameyauliza na masuala mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie kwamba yale tunayomweleza anapofuatilia ofisini tunamthibitishia kwamba tutayatekeleza. Nimhakikishie kwamba Awamu hii ya Tano ya Serikali ya Dkt. John Pombe Magufuli inatenda inachoahidi. Mkakati wa kuhakikisha minara ambayo inajengwa inaanza kufanya kazi tutaifuatilia, kwa hili aliloliuliza nadhani ameuliza tu kuongezea utamu, tumemwambia kwamba mnara huo utaanza kufanya kazi mwishoni mwa mwezi Juni kama tulivyoongea, ni kweli na tutafuatilia. *(Makofi)*

Kuhusu mirafi ya *UCSAF,* naomba nimhakikishie kama nilivyosema hii Serikali inatenda inachoahidi, katika mwaka huu wa fedha hizo zilizotengwa miradi iliyotangazwa tutahakikisha inakamilika. Lakini usisahau kwamba miradi mingine tuliyoongelea hapa haitekelezwi na *UCSAF* peke yake mingine inatekelezwa na *TTCL* na Viettel ambayo katika tangazo hili miradi hiyo hutaiona.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gulamali swali fupi.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali fupi kwa Naibu Waziri.

Ni lini sasa maeneo ya kata za Mwashiku, Ngulu, Uswaya na Igoweko yataweza kupata mawasiliano kama ambavyo Mheshimiwa Naibu Waziri ameweza kujibu swali la Mheshimiwa Mgimwa? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu mafupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Gulamali ni mfuatiliaji sana, siyo wa masuala ya mawasiliano peke yake, bali ni pamoja na barabara zake zile mbili ambazo viongozi wetu wakuu walitoa ahadi, na nyakati zote wakati akifuatilia hiyo miradi nimekuwa nikimhakikishia kwamba Serikali hii ya Awamu ya Tano inatenda inachoahidi. Mheshimiwa Gulamali nikuahidi katika yale uliyoyafuatilia vijiji hivi sikumbuki kama ulinitajia. Kwa hiyo, nitafuatilia ratiba ya utekelezaji wa makapuni yote yanayotuletea mawasiliano nchini kuona kama hivi vimeshaingizwa katika ratiba na kama vitakuwa havijaingizwa namhakikishia tutaviingiza. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusikia Mheshimiwa Waziri anasema Serikali hii kila ilichoahidi inatenda bado mna maswali? Naona bado mmesimama, Mheshimiwa Khadija Ali. *(Kicheko)*

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika nashukuru kwa kuniona, kwa kuwa tatizo la Jimbo la Kalenga linafanana kabisa na tatizo la Mkoa wa Kusini Unguja;

Je, ni lini Serikali itapeleka minara ya simu kwenye vijiji ambavyo bado havijafikiwa na huduma hii kwenye Mkoa wangu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Khadija Ali anafahamu kwamba tumefungua ofisi Unguja ambayo kazi yake kubwa ni kuhakikisha mawasiliano yanakamilishwa katika vijiji mbalimbali Unguja na Pemba. Naomba nimhakikishie akitembelea hii ofisi atapata uhakika wa eneo hilo analoliongelea ratiba yake ikoje.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Selemani Zedi swali fupi.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, pamoja na kuwepo kwa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* kwa lengo la kuchangia gharama za ujenzi wa minara maeneo ya vijijini, lakini bado *speed* ya ujenzi wa makampuni haya umekuwa mdogo sana, kulikuwa napendekezo kwamba sasa Mfuko wa *UCSAF* ugharamie asilimia 100 ya ujenzi wa minara katika maeneo ya vijijini ambayo hayana mvuto kwa biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefikia wapi katika kuona umuhimu huu wa kwamba Mfuko wa *UCSAF* ugharamie minara ya vijijini kwa asilimia 100 badala ya kuyaachia makampuni ambayo kwa kweli yamekuwa mazito kupeleka minara vijijni kwa sababu hakuna mvuto wa kibiashara?

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, mfuko wa mawasiliano kwa wote unagharamia kuanzia asilimia kumi mpaka asilimia 100; inategemea eneo na eneo. Kama eneo hilo halina mvuto wa kibiashara kabisa mfuko wa mawasiliano kwa wote unagharamia asilimia 100. Kuna tatizo ambalo limejitokeza ni kweli makampuni ya simu yamechelewa kujenga minara ya mawasiliano kwenye maeneo mbalimbali na kwa kulijua hilo sasa Serikali itapiga faini makampuni ya simu yote ambayo yamechelewa kupeleka mawasiliano kwenye maeneo hayo. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Ukerewe swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Stephen Ngonyani.

Na. 369

**Meli ya MV Butiama**

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI (K. n. y. MHE. JOSEPH M. MKUNDI)** aliuliza:-

Ni zaidi ya miaka mitano sasa tangu Meli ya MV Butiama isitishe huduma zake katika Ziwa Victoria kati ya Mwanza na Nansio (Ukerewe) hali inayosababisha shida na usumbufu mkubwa wa usafiri kwa wakazi wa Ukerewe.

(a) Je, ni lini meli hiyo ya MV Butiama itatengenezwa na kuendelea kutoa huduma kati ya Mwanza na Nansio?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuleta meli mpya sasa ikizingatiwa kuwa meli ya MV Clarius imechakaa sana?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Ukerewe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, meli ya MV Butiama ambayo ilikuwa inatoa huduma ya usafiri majini kati ya bandari ya Mwanza na bandari ya Nansio - Ukerewe ilisitisha huduma hiyo mwaka 2010 baada ya *engine* yake kupata uharibifu mkubwa na kukatika muhimili wake *(crankshaft)*. Kufuatia uharibifu huo tathmini ilifanyika na kubaini kuwa injini hiyo isingefaa tena kutumika kwa ajili ya usafirishaji wa aibiria na mizigo na kwamba inabidi iununuliwe *engine* mpya pamoja na *gear box* yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni ya huduma za meli *MSCL* ilikamilisha mchakato wa kupata *engine* stahiki kwa ajili ya meli hiyo na gharama elekezi. Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Serikali kupitia Kampuni ya Huduma za Meli imetenga kiasi cha fedha za Kitanzania shilingi bilioni 3.6 kwa ajili ya matengenezo ya meli ya MV Butiama. Aidha, kulingana na tathmini iliyofanyika matengenezo ya meli hiyo yanategemewa kukamilika ndani ya miezi wa kumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mipango thabiti ya kujenga meli mpya zitakazotoa huduma ya usafiri na usafirishaji katika Ziwa Victoria na maziwa mengine makuu ya Tanganyika na Nyasa. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali imetenga kiasi cha fedha za Kitanzania shilingi bilioni 21.0 ikiwa malipo ya awali ya asilimia 50 kwa ajili ya ujenzi wa meli mpya katika Ziwa Victoria.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na ninamshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana, nina maswali mawili ya nyongeza:-

Kwa kuwa wananchi wa Mwanza na Ukelewe wamepata usumbufu zaidi ya miaka mitano kwa kukosa usafiri; na kwa kuwa ni sehemu muhimu sana kwa wavuvi; ni lini sasa Serikali itawapa usafiri wa dharura wananchi wale ili waone umuhimu wa Serikali yao inavyowasaidia?

Swali la pili, kwa kuwa tatizo la Ukerewe linalingana kabisa na Tanga, wananchi wa Tanga, Pemba, Unguja pamoja na Bagamoyo wanahitaji meli kama hiyo ili iwasaidie; je, Serikali ina mpango gani wa kuwahakikishia wananchi wa Ziwa, umetaja Ziwa Nyasa, umetaja Ziwa Victoria, umetaja Ziwa Tanganyika; lakini je, katika Bahari ya Hindi wananchi wa Tanga, Pemba, Unguja na Bagamoyo ni lini na wao watapata meli ili na wao waepukane na kile kimbunga cha kila siku kufariki kwenye meli? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru Mheshimiwa Stephen Ngonyani, Mbunge wa Korogwe Vijijini kwa namna ambavyo ameniamsha namna ya kufuatilia masuala ya wananchi wa Korogwe Vijijini na mimi vilevile Namtumbo, kwa kweli ninaomba Wabunge wengine wafuate nyayo zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu dharura nadhani Mheshimiwa anafahamu kwamba tuna usafiri ambao sasa hivi upo, isipokuwa hautoshelezi. Kwa masuala ya dharura usafiri unapatikana, nia yetu kubwa ni kuondokana na meli hizi chakavu, tuzitengeneze na tulete mpya. Kwa hiyo, masuala ya dharura siyo tatizo yamekuwa *taken care off*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa swali la pili niliwahi kujibu swali kama hilo katika Bunge hili kwamba katika miaka ya 1980 - 1990 tuliamua kuingiza sekta binafsi katika shughuli za usafiri na kwa upande wa meli tulianzia na upande wa Bahari ya Hindi unafahamu kwamba kuna wasafirishaji binafsi wengi wanafanya shughuli hizo za usafiri. Kama ombi lako maana yake unataka Serikali iondoe hiyo sera ilete sera nyingine tutaliwasilisha Serikalini likajadiliwe tuone hasara na faida yake, kwa sasa naomba tuendelee kupata huduma za meli kutoka kwa wasafirishaji binafsi, *TACOSHILI* tulishaisimamisha miaka ya 1990. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ngonyani hasa sehemu (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi tunavyoongea upo usafiri wa kudumu baina ya Dar es Salaam, Unguja na Pemba. Ipo meli ambayo inaitwa MV Mapinduzi II ambayo ni meli ya kisasa inayosafiri baina ya Unguja na Pemba na tutaongea na Wizara ya Uchukuzi na Mawasiliano huko Zanzibar kuhakikisha kwamba meli hii inasafiri kutoka Pemba kwenda Tanga kama ilivyokuwa hivyo zamani. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi.

Kwa kuwa kulikuwa na ahadi ya Rais Mstaafu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kununua meli katika maziwa makuu matatu kwa maana ya Ziwa Tanganyika, Ziwa Victoria na Ziwa Nyasa, na katika bajeti hii ya Mawasiliano na Uchukuzi kuna ununuzi wa meli moja ya Ziwa Victoria, lakini hivi karibuni Waziri wa Katiba na Sheria alisikika akipongeza uundwaji wa meli mpya ya mizigo na abiria katika Ziwa Nyasa. Je, ni lini sasa meli mpya itapelekwa katika Ziwa Tanganyika ili tuachane na meli ya MV Liemba? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kiongozi wetu wa Serikali ya Awamu ya Nne alitoa ahadi ya kuleta meli mpya katika maziwa yote makuu matatu na ahadi hiyo ilirudiwa na Rais wa Awamu ya Tano Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwamba atatekeleza ahadi hiyo ambayo mwanzo ilitolewa na Mheshimiwa Kikwete.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie hili tulilolizungumzia katika jibu langu la swali la msingi ndiyo kuanza kutekeleza ahadi ya viongozi hawa wakuu, tunaanza na meli ya MV Victoria na unafahamu kwamba wakati kuna meli ndogo inatengenezwa kule Nyasa baada ya hapo tutafuatia na meli katika

Ziwa Tanganyika na hatimaye ahadi hizo za viongozi wakuu zitatekelezwa katika kipindi hiki cha miaka mitano tulichoahidi. Tuanze na hatua moja halafu tutasonga mbele. *(Makofi)*

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru.

Katika Awamu ya Nne, Serikali ya Ujerumani ilileta maombi nchini mwetu kutaka kufanya ukarabati meli ya MV Liemba ambayo ipo toka Vita Kuu ya Kwanza kama *sentiment value* ya Serikali ile walitoa *offer* ya kuitengeneza na kui-*refurbish* na kuifanya i-*comply* na *sea worthiness* kwa asilimia mia moja lakini hawakupewa jibu sahihi.

Je, Serikali mko tayari kukaa nao tena ili sasa *offer* ile iweze kufanywa na meli ile iweze kutengenezwa na ili iweze kutoa huduma kwa uhakika kwa wananchi wa Ziwa Tanganyika?

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kulikuwa na mpango na sasa hivi mpango huo upo, mimi mwenyewe kama mwezi mmoja uliopita nilikuwa na mazungumzo ya kina na Waziri wa Maendeleo wa Ujerumani, mpango huo upo na tunaendelea nao ili MV Liemba ambayo imedumu kwa muda mrefu iweze kufanya kazi kama inavyopaswa. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE**: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Kwa kuwa kulikuwa na mpango ambao ulisemekana kwamba Serikali ilikuwa inanunua meli tatu Korea Kusini na sasa hivi katika majibu ambayo yanatolewa na Serikali ni kama mpango ule umekufa kabisa.

Je, Serikali ituambie ina mpango gani kuhakikisha kwamba hizo meli ambazo zilikuwa zinunuliwe kutoka Korea Kusini zinanunuliwa na kupelekwa katika maziwa yote matatu?

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mhimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa tulikuwa na mazungumzo na Serikali ya Korea na mimi nilikaa miezi miwili iliyopita nilizungumza na Balozi wa Korea na mazungumzo hayo bado yanaendelea, lakini itategemea hasa *Exim Bank* ya Korea itaamua vipi ndiyo tutaendelea na utaratibu huo.

Na. 370

## Nyumba Zilizowekwa Alama ya 'X' Njombe Mjini

**MHE. EDWARD F. MWALONGO** aliuliza:-

Serikali imeweka alama ya "X" ya kijani na nyekundu katika nyumba za wakazi wa Jimbo la Njombe Mjini kikiwemo na Kituo cha Polisi cha Njombe.

Je, Serikali inasema nini juu ya tafsiri sahihi ya alama hizo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Edward Franz Mwalongo, Mbunge wa Njombe Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na Sheria ya zamani ya Barabara ya mwaka 1932 ambayo ilirekebishwa mwaka 1967 *(The Highway Ordinance CAP. 167)* upana wa eneo la hifadhi ya barabara kuu na barabara za mikoa ulikuwa ni mita 45 yaani mita 22.5 kutoka katikati ya barabara kila upande.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii naenda taratibu kwa sababu najua watu wengi sana wana-*interest* nalo na wananchi wasikie. Sheria mpya ya Barabara Na. 13 ya mwaka 2007 *(The Road Act, No. 13 of 2007)* na Kanuni za Menejimenti ya Barabara za mwaka 2009 *(The Road Management Regulations of 2009)* ziliongeza upana wa eneo la hifadhi ya barabara kuu na barabara za Mikoa kuwa mita 60, yaani mita 30 kutoka katikati ya barabara kila upande, hivyo kuna ongezeko la mita 7.5 kila upande wa barabara kulingana na Sheria mpya ya Barabara ya mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na maelezo ya utangulizi napenda kutoa ufafanuzi kwamba, nyumba zilizo ndani ya eneo la mita 22.5 kutoka katikati ya barabara kila upande zipo ndani ya eneo la hifadhi ya barabara kinyume cha sheria, hivyo zimewekewe alama ya "X" nyekundu na zinatakiwa kubomolewa bila malipo yeyote ya fidia.

Aidha, nyumba zilizojengwa katika eneo la kutoka mita 22.5 hadi mita 30 kutoka katikati ya barabara kila upande kabla ya Sheria mpya ya Barabara ya mwaka 2007 zimewekewa alama ya "X" ya kijani katika baadhi ya Mikoa kwa ajili ya utambuzi ili maeneo hayo yakihitajika kwa ajili ya ujenzi au upanuzi wa barabara wamiliki walipwe fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa wito kwa wananchi kutofanya uendelezaji mpya wa nyumba kwenye eneo la hifadhi ya barabara ili kuepuka hasara ya kuvunjiwa nyumba zao bila kulipwa fidia.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Nashukuru kwa majibu ya Naibu Waziri, kwa kuwa suala hili linawagusa karibu Watanzania wote na mimi nitajitahidi kwenda polepole kama alivyoenda yeye polepole. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa nyumba nyingi…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwalongo naomba usiende polepole kwa sababu muda wetu unakimbia sana na watu wana maswali mengi. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa nyumba nyingi katika Mji wa Njombe zimewekewa alama ya kijani. Serikali haioni ipo haja ya sasa kufuta alama hizo ili kuwapa fursa wananchi wamiliki wa nyumba hizo kufanya ukarabati wa nyumba zao na kuzitumia nyumba zao kama dhamana katika taasisi za fedha? *(Makofi)*

Swali la pili, je, Serikali haioni sasa upo ulazima kuleta Sheria Namba 13 ya mwaka 2007 tuifanyie marekebisho ili ibainike bayana kwamba, maeneo ya mjini yawe na upana wa mita 42 badala ya 60 za sasa. Hii itasaidia kutunza historia za miji katika nchi yetu, lakini vilevile itaipunguzia gharama Serikali pamoja na wananchi? Ahsante. (*Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, tumeweka 'X' ya kijani kama ishara kwamba hilo eneo haliruhusiwi kuendelezwa, haliruhusiwi kujengwa nyumba mpya kwa sababu ni eneo la hifadhi ya barabara kwa mujibu wa Sheria ya mwaka 2007. Kwa hiyo, kusema wafute na ianze kutumika kama dhamana siyo sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Watanzania wote wakati tunapitisha sheria hii tulikuwa na malengo ya kuiendeleza nchi yetu kimiundominu, tupate fursa ya kupanua barabara na hatimaye zitupeleke katika karne ya viwanda, tuwe na maendeleo makubwa na huko ndiyo tunakoenda hatuwezi kurudi nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili, suala la kubadilisha sheria, kwanza mimi binafsi na niliongea na Mheshimiwa Waziri wangu naongea kwa niaba yake kwa kweli tulitaka tupanue zaidi kwa sababu sasa hivi tunaenda

kwenye miundombinu, sehemu za mijini kuna *flyovers* na *highways* lazima tuwe nazo ambazo zinahitaji ardhi kubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hiyo ya kubadilisha sheria mimi binafsi siiungi mkono lakini tumechukua ombi lako na tutaliwasilisha Serikalini likajadiliwe ili maamuzi ya Kiserikali yatolewe. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri watu wengi wamesimama, lakini nadhani swali la msingi hapo ni kwamba hawa watu wenye kijani umesema mpaka mtakapohitaji barabara. Kama jibu ni hilo, hawa watu waendelee kusubiri? Kama utaihitaji barabara baada ya miaka kumi, wao inabidi waendelee kusubiri wasifanye chochote kwenye hayo maeneo yao? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Naibu Spika kama ifuatavyo:- *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, alama ya kijani ama nyekundu, maana yake nyumba hiyo haitakiwi kuwepo hapo kwa mujibu wa Sheria ya mwaka 2007. Tunachotaka, wale ambao walijenga kabla ya mwaka 2007 haki yao inayoongelewa hapa ni ya kufidiwa, siyo kuendelea kukaa, ila hatuwaondoi mapema mpaka pale tutakapokuwa na mahitaji ndipo tutakapowafidia. Ila tutakachokifidia ni kile kilichofanyika kabla ya mwaka 2007. Chochote kitakachokuwa kimefanyika baada ya mwaka 2007 kitabomolewa bila fidia.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kabla hujatoka, alama nyekundu ni kwamba wale watu wanatakiwa kubomoa wasiwepo; alama ya kijani maana yake sheria imewakuta. Sasa ndiyo anauliza Mheshimiwa Mwalongo wanatakiwa kusubiri muda gani hao wenye alama ya kijani ambao sheria imewakuta?

Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hii alama ya kijani, hili tutalichukua na tutaliangalia tuone tutafanyaje. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Rita Kabati.

Na. 371

**Tatizo la Fistula kwa Kina Mama Nchini**

**MHE. RITTA E. KABATI (K.n.y. MHE. MGENI JADI KADIKA)** aliuliza:-

Tatizo la fistula limekuwa likiwakumba wanawake wengi sana hapa nchini hususan maeneo ya vijijini hali inayowasababishia kuathirika kiakili na kimwili:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kutokomeza tatizo hili hapa nchini?

(b) Kwa sasa ni hospitali moja tu ya *CCBRT* hapa nchini inayotoa matibabu ya tatizo na iko Dar es Salaam tu; je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka huduma hii katika mikoa mbalimbali au kanda ili wanawake wengi waweze kupata huduma hiyo?

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la fistula linatokana na Mwanamke mjamzito kupata uchungu pingamizi kwa muda mrefu. Tatizo hili linaweza kuepukwa iwapo tutakuwa na huduma bora kwa wajawazito ili kuepuka uchungu pingamizi wa muda mrefu. Ili kuboresha huduma kwa wajawazito, Wizara imekuwa ikichukua hatua mbalimbali ikiwemo kuelimisha jamii kupitia wahudumu wa afya katika jamii na vyombo vya habari kuhusu umuhimu wa kujifungulia katika vituo vya kutolea huduma za afya.

Pili, kupandisha hadhi baadhi ya vituo vya afya ili viweze kufanya upasuaji wa kumtoa mtoto.

Tatu kuwajengea uwezo watoa huduma ya afya ili waweze kumfuatilia mjamzito wakati wa uchungu wa uzazi na ikibidi aingilie kati kabla kufikia uchungu pingamizi na pia kuboresha mfumo wa rufaa ikiwemo magari ya kubebea wagonjwa.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, huduma kwa wagonjwa wa fistula inatolewa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Hospitali za Rufaa za Kanda za Bugando - Mwanza; KCMC -Moshi; na Mbeya Rufaa. Hospitali nyingine ni pamoja na *CCBRT* - Dar es Salaam; Peramiho - Ruvuma; Seliani - Arusha; na St. Gasper - Itigi. Jitihada zinaendelea kuwezesha Hospitali za Rufaa za Mikoa ziweze kutoa huduma ya matibabu ya fistula.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rita Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. RITA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri. Naomba niulize maswali mawili madogo tu ya nyongeza.

Kwa kuwa ugonjwa huu wa fistula umeleta athari sana kwa wanawake wakiwemo hata wanawake wa Iringa pamoja na Njombe, kutokana hasa na ukosefu wa vifaa vya kujifungulia na miundombinu migumu sana ambayo wanawake wamekuwa hawavifikii hata vituo vya afya wala zahanati.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba wanawake kwanza hawajifungulii majumbani na vifaa kuwepo katika zahanati na vituo vya afya hasa vilivyopo katika vijiji vyetu huko ndani kabisa?

Swali la pili, je, Serikali imebaini ni kwa kiasi gani wanawake wameathirika kutokana na ugonjwa huu wa fistula? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu kwanza niseme jambo moja kwa ufupi kwamba ugonjwa wa fistula ni ugonjwa ambao unasababisha kuwepo kwa tundu lisilo la kawaida kati ya uke na kibofu cha mkojo au kati ya uke na njia ya kutolea haja kubwa.

Jambo la pili ambalo ningependa kulifafanua ni kwamba, ugonjwa huu hausababishwi na laana, kurogwa au mwanamke kutembea na wanaume wengi wakati wa ujauzito. Nimeona niliseme hili kwa sababu wanawake wengi wamekuwa ni wahanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu maswali yake mawili ya nyongeza; kwamba tuna mikakati gani sasa ya kuhakikisha wanawake wanajifungulia katika vituo vya afya. Tulieleza wakati tunawasilisha bajeti yetu hapa, la kwanza ni kwamba tutaendelea kutoa elimu kwa wanawake wajawazito kuhakikisha wanahudhuria kliniki wakati wanapokuwa wajawazito na *especially* tutahamasisha wale wanawake wa kuanzia miezi miwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ambalo tutalifanya ni kuhakikisha kwamba tunaweka huduma za upasuaji wa dharura katika vituo vya afya. Nimesikiliza michango ya Waheshimiwa Wabunge wakati wa mjadala huu ambao unaendelea wa bajeti ya Serikali hasa Wabunge wa chama changu,

wanawake wa Chama cha Mapinduzi, wameongea kwa sauti kubwa sana kuhusu umuhimu wa kuboresha huduma za upasuaji wa dharura.

Kwa hiyo, nataka kumthibitishia Mheshimiwa Ritta Kabati kwamba bajeti ya Wizara ya Afya inayokuja itahakikisha tunaweka vichocheo vya kuwafanya wanawake wahudhurie kliniki na nilishasema, tutatoa vifaa vya kujifungulia kwa wanawake 500,000 kuanzia mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, madhara ya ugonjwa huu wa fistula. Yapo madhara ya kiafya, madhara ya kiuchumi na kijamii. Ya kiafya kama nilivyosema, mwanamke anatokwa na mkojo bila kujizuia, lakini pia haja kubwa inatoka katika njia ya uke. Kwa hiyo, hayo ni madhara ya kiafya na asilimia 85 ya wanawake ambao wanapata fistula wanapoteza watoto.

Mhehimiwa Naibu Spika, madhara makubwa ni ya kiuchumi na kijamii. Wanawake wengi wanaachwa na wanaume wao kwa sababu tu wamepata ugonjwa huo wa fistula, lakini wanawake hawa hawawezi kufanya shughuli za kujiletea maendeleo yao kwa sababu wana harufu, hawezi hata kufungua duka la maandazi au kigenge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa ambalo nataka kuwathibitishia wanawake, ugonjwa wa fistula unatibika na matibabu yake yanapatikana katika hospitali zetu. Lengo la Wizara ya Afya ni kuhakikisha wanawake hawapati fistula, lakini kama wakipata basi wapate matibabu. Kwa hiyo, katika Hospitali zetu zote za Rufaa za Mikoa tutahakikisha huduma za upasuaji wa matibabu ya fistula zinapatikana. Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maria Kangoye.

**MHE. MARIA N. KANGOYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tatizo la fistula limekuwa likiongezeka kadri miaka inavyoenda hususan maeneo ya vijijini; je, Serikali ina mpango gani wa kuelimisha wakunga wa jadi ili kupunguza tatizo la fistula na vifo vya mama na mtoto? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Maria Kangoye, Mbunge Viti Maalum (Vijana) kwa kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiri sitawatendea haki Watanzania kama sitakiri kwamba fistula inawapata wanawake walio katika hali ya chini ambao wako vijijini na kwa sababu ya uhaba wa miundombinu wa vituo vya afya, uhaba wa wataalam, pia usafiri wa kutoka pale nyumbani kwenda kituo cha afya na wanawake wa mijini ambapo kunakuwa na msongamano wa watu katika upatikanaji wa huduma za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mheshimiwa Kangoye anataka kujua, Serikali tutawahamasisha au tutawashirikisha vipi wakunga wa jadi ili waweze kuhakikisha kwamba na wenyewe wanashiriki katika kuokoa vifo vya akina mama wajawazito?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli, asilimia 48 ya wanawake wa Tanzania bado wanajifungulia majumbani maana yake wanajifungulia kwa wakunga wa jadi. Kwa hiyo, Wizara ya Afya itaendelea kuhakikisha tunawapa elimu na kuwaelewesha kwamba wasitoe huduma za kujifungulia kwa hawa wanawake wanaowafuata; wao wawe kama ni sehemu ya rufaa. Mwanamke akienda kwa mkunga wa jadi, basi yeye ampeleke au amhamasishe kumpeleka katika kituo cha afya. Ni jambo ambalo tutalifanyia kazi, lakini pia tumekuwa tukitoa mafunzo kwa wakunga wa jadi jinsi gani ya kuwahudumia wanawake wajawazito ili tuweze kuepusha vifo vya akina mama wajawazito.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nilisema, tumeamua kuanza kutoa vifaa vya kujifungulia kwa wanawake wajawazito ili kuwa kichocheo cha wao kwenda sasa kwenye vituo vya afya vya kujifungulia badala ya kujifungulia majumbani. Ni jambo ambalo tutalipa kipaumbele. Niwathibitishie Wabunge wenzangu wanawake, mimi ni mama; nimepita *labour* mara mbili. Kwa hiyo, suala la uzazi salama kwa mwanamke ni suala la kipaumbele kwangu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bahati Abeid.

**MHE. BAHATI ALI ABEID:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo hili la fistula wanawake wanapolipata, huwa wanatumia pesa nyingi ili kupona. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka kwa wanawake wanaopata tatizo hili wakatibiwa bure?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Nimshukuru sana Mheshimiwa Bahati Abeid, Mbunge wa Jimbo la Mahonda kwa swali lake zuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sera yetu ya afya inasema mwanamke mjamzito ndiye anatakiwa kupata matibabu bure; na huduma hizi za fistula *especially* suala la upasuaji zinafanyika baada ya siku 40 baada ya mwanamke kujifungua. Kwa hiyo, niseme tu tumelibeba. Naomba nilipokee, haliko kisera, lakini kwa sababu kama unavyosema ni jambo ambalo linawaathiri wanawake wengi hasa wa vijijini, nitashauriana na wenzangu tuone ni jinsi gani tutatoa matibabu bure kwa wagonjwa wa fistula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana Hospitali ya *CCBRT,* wao wanatoa matibabu bure kwa wagonjwa wa fistula. Kwa hiyo, ni changamoto kwetu sisi wa Serikali pia kuhakikisha kwamba na matibabu hayo bure ya fistula yanapatikana katika Hospitali za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa ni kwamba ule upasuaji unachukua saa sita na daktari anatakiwa ainame kwa saa sita.

Kwa hiyo, tutaangalia ni jinsi gani tutakuja na *incentive package* ya jinsi gani ya kutoa motisha kwa Madaktari wetu bingwa wa magonjwa ya akina mama kuwafanyia matibabu haya bure badala ya kulipia, lakini nawashakuru sana *CCBRT.* *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Wizara ya Nishati na Madini; Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, Mbunge wa Mpanda Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 372

**Kuwawezesha Wachimbaji Wadogo Wadogo wa Madini-Katavi**

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI** aliuliza:-

Dhahabu ni kati ya madini yanayozalishwa na wachimbaji wadogo wadogo Mkoani Katavi; na kumekuwepo na suala la asilimia hafifu ya dhahabu ya Mpanda Kati ya 60% hadi 90%. Uhafifu huu ulitokana na ukweli kwamba sehemu ya asilimia ni madini mengine kama fedha, shaba na kadhalika, lakini katika mauzo wachimbaji wamekuwa wakilipwa thamani ya dhahabu tu.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwawezesha wachimbaji hawa kwa kuwapatia teknolojia sahihi ya kutofautisha dhahabu, shaba na fedha ili kuongeza thamani na pato halisi kwa wachimbaji hao na kuinua Pato la Taifa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, Mbunge wa Mpanda Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa, mbali na dhahabu *(gold ore)* katika maeneo ya Mpanda huwa na madini mengine kama vile fedha, shaba pamoja na madini ya risasi. Kwa upande wa wachimbaji wadogo wa dhahabu nchini, kiwango cha uchenjuaji wa dhahabu huwezesha kuzalisha dhahabu kwa wastani wa asilimia 60 tu. Sababu kubwa ni pamoja na mitambo duni ya uchenjuaji inayotumika; kuanza uzalishaji kabla ya kufanya utafiti wa kujua aina ya mitambo inayotumika, lakini pia kiwango duni cha usagaji mbale.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaona umuhimu sasa wa kuwawezesha wachimbaji wadogo kwa kuwapatia teknolojia sahihi ya kutofautisha dhahabu, shaba na fedha kwa ajili ya mafunzo. Kuanzia mwezi Septemba, 2016, Serikali kupitia Wizara yangu itaanza kujenga vituo vya mfano pamoja na kutoa mafunzo ya uchenjuaji madini hususan dhahabu katika Mikoa ya Geita, Katavi pamoja na Mara.

Kadhalika madini ya chokaa katika Mkoa wa Tanga, madini ya bati katika Mkoa wa Kagera na madini ya chumvi katika Mkoa wa Lindi ikiwa ni pamoja na madini ya vito katika Mkoa wa Ruvuma. Vituo hivi vitasaidia sana kuongeza viwango vya uchenjuaji madini hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sasa pia niwaombe Waheshimiwa Wabunge tuwashauri wachimbaji wadogo katika maeneo yao kutumia taasisi zetu za Serikali ikiwa ni pamoja na *STAMICO* ambalo hushughulikia masuala ya wachimbaji wadogo, Chuo cha Madini Dodoma, Vyuo Vikuu vya Dodoma na Dar es Salaam na Wakala wa Jiolojia Tanzania *(GST)* ili kuwafanyia utafiti na kuwashauri mambo yanayofaa kwa ajili ya uchimbaji na uchenjuaji wa tija.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kapufi, swali la nyongeza.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo kimsingi yana afya, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa mpango huo mzuri wa Serikali ili wachimbaji wadogo waweze kufikia hatua ya kupata mpango huo mzuri, ni lazima wawe na maeneo. Naibu Waziri anasema nini kwa maana ya kutenga maeneo kwa eneo hilo la Mpanda? Hilo ni swali la kwanza. *(Makofi)*

Swali la pili, nafahamu Wizara kwa ujumla wake imekuwa ikisaidia wachimbaji wadogo nchini. Je, ni utaratibu upi unaotumika kwa maana ya suala zima la utoaji ruzuku kwa wachimbaji hawa wadogo? Naliuliza hilo ili iwe faida kwa wachimbaji wote wadogo nchini? Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nipate ridhaa yako nimshukuru sana Mheshimiwa Kapufi. Kwanza nampongeza kuwa mchimbaji mdogo kati ya wachimbaji wadogo maarufu hapa nchini. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Kapufi kama mdau mzuri na ni mchimbaji mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nampongeza sana Mheshimiwa Kapufi kwa kuwawakilisha vyema wananchi wa Mpanda. Mheshimiwa Kapufi nikuhakikishie kwamba wananchi wako ambao ni wachimbaji wadogo, kama ambavyo wewe unachimba nao watafikia kiwango chako cha uchimbaji kama unavyoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nijielekeze kwenye maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kapufi. Ni lini Serikali itawatengea maeneo wachimbaji wadogo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa hivi Wakala wa Jiolojia Tanzania *(GST)* anafanya tathmini kwa mambo matatu; tathmini ya Kijiokemia, tathmini ya Kijiolojia na tathmini ya Kijiofizikia na mwezi wa saba tunaanza kuwatengea maeneo hayo. Zoezi la kuwatengea wananchi maeneo litakuwa ni endelevu; kuanzia mwezi wa saba na kuendelea tutafanya kazi ya kuwatengea maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa Serikali imetenga hekta 12,000 kwa ajili ya kuwatenga maeneo, kadhalika, imetenga shilingi milioni 640 kwa ajili ya Wakala wa Jiolojia kutathmini maeneo ambayo yatatengwa. Maeneo ambayo tutayatenga ni mengi sana ikiwa ni pamoja na Lindi, Geita, Sambaru – Singida, pamoja na Londoni. Maeneo mengine tutakayotenga kule Mpanda ni pamoja na eneo la Dirifu, Katuma, *Society* pamoja na eneo la Katasunga. Maeneo yote ya Mpanda Mheshimiwa Kapufi tutaendelea kuyatenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na suala la pili kuhusu utaratibu wa ruzuku, ni kweli kabisa mwaka 2015/2016, Serikali ilitenga shilingi bilioni 7.24 na mwaka huu kwa ridhaa ya Waheshimiwa Wabunge tumetenga shilingi bilioni 6.68, hii ni kwa ajili ya kuwagawia wananchi kama ruzuku.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongeze kidogo kuhusu hili. Utaratibu tunaotumia kwa sasa, kwanza kabisa leseni lazima ziwe za Watanzania peke yake kwa asilimia mia moja. Hilo la kwanza. Pili, leseni hizo lazima ziwe hai na zinafanyiwa kazi; na tatu, tunawahamasisha sana wananchi wajiunge kwenye vikundi ili ruzuku hii iwanufaishe Watanzania wengi. La nne, tumeongeza sasa badala ya kutenga dola 50,000 kwa msimu huu, tutatenga dola 100,000 kwa kila atakayekidhi vigezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningesema mengi sana kwenye eneo hili, lakini niwahamasishe Watanzania; Mheshimiwa Kapufi na Waheshimiwa Wabunge wengine ili waweze kunufaika na ruzuku hii.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mlinga.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.
Kwanza naomba ni-*declare interest,* na mimi ni mchimbaji mdogo japokuwa sijawahi kunufaika kutokana na mfumo mbovu wa Serikali. *(Kicheko)*

Tatizo lililoko Mpanda Mjini linafanana na lililoko katika Jimbo langu la Ulanga. Je, sasa Serikali haioni umuhimu wa kuwaelimisha na kuwawezesha wachimbaji wadogo wadogo wa Jimbo la Ulanga ili waweze kuyathaminisha madini haya wanayoyapata ili waweze kuyauza katika thamani halisi inayoendana na soko?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona umuhimu, hilo la kwanza. Tunaona umuhimu wananchi wako Mheshimiwa Mbunge kuendelea kuwaelimisha, lakini siyo kuwaelimisha tu, hata kuwapatia ruzuku wakikidhi vigezo. Napenda tu kusema katika Jimbo la Ulanga, maeneo ya Mvomero, maeneo ya Iringa, maeneo ya Singida, yote kwa pamoja tunaendelea kuyatathmini tuwatengee wananchi. Kwa hiyo, pamoja na kutoa elimu, tunawahamisha Waheshimiwa Wabunge wawahamishe wananchi washirikiane na Waheshimiwa Wabunge ili kunufaika na rasilimali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi wa kwanza mwaka huu, Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini amekaa sana na wachimbaji wadogo Wawakilishi wao wa Katavi, Singida pamoja na kwa Mheshimiwa Mbunge wa Ulanga. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mlinga nakuhakikishia tutaendelea kusaidiana na wananchi wako kuwaelimisha waweze kunufaika na mapesa haya.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Martha Mlata, swali fupi.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na kuitaja Singida, naomba atusaidie kwamba makampuni yale ambayo yanachukua leseni halafu wanakaa nayo muda mrefu bila kufanyia kazi na hivyo kuwafanya wachimbaji wadogo wasiende kufanya uchimbaji kwenye maeneo yenye madini kama Londoni, Sambaru, Muintiri, Sekenke pamoja na Mkalama. Ninaomba atoe tamko hapa kwa makampuni hayo na ni lini atatekeleza? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia sasa na kuanzia huko nyuma na tunaendelea kufanya hivyo. Naomba nichukue nafasi hii kutoa rai kwamba wachimbaji wote ambao hawayafanyii kazi maeneo yao, Serikali itayachukua na huo ni utaratibu wa kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Madini kifungu Na. 36(1), Sheria Namba 14 ya mwaka 2014 inakataza mwekezaji yeyote kushikilia maeneo bila kuyaendeleza. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mlata kwamba wananchi wa Sekenke, Sambaru, Londoni, Muintiri na wananchi wengine wote tunawapatia maeneo kutokana na wawekezaji ambao hawayaendelezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili niwahakikishie na niwaombe sana Watanzania kwamba sasa tunatekeleza sheria. Maeneo yote ambayo yalikuwa hayafanyiwi kazi na wawekezaji na hasa wawekezaji wa nje, lakini hata wawekezaji wa ndani ambao walikuwa hawayaendelezi, sasa sheria inaanza kuchukua mkondo wake. Maeneo tutayachukua, tutayatumia kwa ajili ya wachimbaji wadogo waweze kupata maeneo ya uhakika kwa ajili ya kujipatia kipato.

Kwa hiyo, namshukuru Mheshimiwa Mlata, kama ambavyo siku zote anafanya; na Kampuni ya *Ashanti Mining* ambayo iko kwake, tunafanya mazungumzo nayo ili ikiwezekana na yenyewe iweze kuachia maeneo kwa ajili ya wananchi wa Singida. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Eeh, hii Wizara imebadilishwa jina hii, nadhani ni Wizara ya Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa, haya.

Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi, sasa aulize swali lake.

Na. 373

**Watanzania Kushiriki Moja kwa Moja katika Jumuiya ya Afrika Mashariki**

**MHE. OSCAR R. MUKASA** aliuliza:-

Tanzania imekuwa mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa miaka kadhaa sasa, ambapo Watanzania wamekuwa wakijulishwa na Serikali juu ya namna ya ushiriki wa Taifa katika mtangamano huo; ushiriki bora na wenye tija hauwezi kutokana na ushiriki mzuri wa Serikali pekee na mihimili mingine ya utawala bali pia ushiriki wa wananchi kwa ngazi ya mtu mmoja mmoja na kwa namna ya pekee Mikoa inayopakana na nchi za Jumuiya hiyo ukiwemo Mkoa wa Kagera.

(a) Je, kuna mkakati gani wa Serikali kumjengea mwananchi mmoja mmoja na taasisi mbalimbali kushiriki katika Jumuiya hiyo?

(b) Kama mkakati huo upo; je, ni kwa vipi wataufahamu?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje. Utusaidie na kutaja sasa jina la hiyo Wizara inaitwaje sasa hivi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba jina la Wizara sasa limebadilishwa na imekuwa ni Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi, lenye vipengele (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi wanachama za Jumuiya ya Afrika Mashariki zinatambua umuhimu wa kuwashirikisha wananchi katika kujenga Jumuiya yao ili kuweza kufikia malengo yanayokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 7(1)(a) ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki inabainisha kuwa Jumuiya ni ya wananchi, hivyo nchi wanachama zina wajibu wa kuhakikisha wananchi wanajengewa uwezo ili waweze kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa mtangamano wa Afrika Mashariki kwa kuzitumia fursa za Jumuiya hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia hilo, Wizara iliandaa Mkakati wa Mawasiliano kwa Umma ulioanza kutekelezwa tangu mwaka 2012. Mkakati huu unatoa mwongozo wa utoaji elimu kwa Umma kuhusu Mtangamano wa Afrika Mashariki kwa makundi mbalimbali na pia ni nyenzo ya kupata mrejesho kutoka kwa wadau.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu kuanza kutekelezwa kwa Mkakati huo, wananchi wamefahamishwa kufahamu mkakati huu kupitia ziara za mipakani, vipindi vya televisheni na redio, vipeperushi, machapisho, makala, mikutano na wafanyabiashara, semina, maonesho mbalimbali kama vile Wiki ya Utumishi wa Umma, Saba Saba, Nane Nane, Maonesho ya Wafanyabiashara Zanzibar na Siku ya Mara pamoja na kuweka mabango kwenye mipaka ya Namanga, Horohoro, Holili, Sirari, Mutukula, Rusumo na Kabanga.

Aidha, mkakati huu ambao upo katika mfumo wa kitabu, umesambazwa kwa wadau kwenye shughuli mbalimbali za elimu kwa Umma zinapofanyika na unapatikana katika tovuti ya Wizara, pamoja na Kituo cha Habari cha Wizara kilichopo katika jengo la *NSSF - Water Front,* ghorofa ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa sote ni wadau wa mtangamano wa Afrika Mashariki, Wizara inaomba kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge kuwaelimisha wananchi katika Majimbo yao pindi wanapoongea nao ili waweze kuzitambua na kuzitumia fursa zitokanazo na mtangamano huo, kwani ni eneo mojawapo linaloweza kuwaongozea kipato na kupunguza tatizo la ajira lililopo nchini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Oscar Mukasa, swali la nyongeza.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Naibu Spika nashukuru na namshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania inashiriki kwenye mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kama Taifa, lakini iko haja ya kutafuta namna ambavyo Wilaya na Halmashauri ambazo zinapakana na nchi jirani zinazoshiriki kwenye Jumuiya hii kuzitumia fursa ambazo wigo wake unaishia kwenye Wilaya zinazopakana na nchi hizo.

Kwa kuwa Biharamulo inapakana na Rwanda kijiografia na kimiundombinu; na kwa kuwa wananchi wa Biharamulo kwa kushirikiana na Mbunge wao wameshazitambua fursa lakini wanahitaji nguvu ya kidiplomasia ya ngazi ya kitaifa kuhakikisha tunazichukua; je, Waziri yuko tayari kuleta nguvu ya uchumi wa kidiplomasia Biharamulo kuzungumza nasi ili tuzitumie?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; je, Waziri yuko tayari kuambatana na mimi akiwa pamoja na wataalamu wa diplomasia ya uchumi kutoka Wizara yake ili tukae na wataalam wa Biharamulo tuzitumie fursa hizo? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo Mifugo na Uvuvi kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba Wilaya na jamii ambazo zipo mipakani zina nafasi kubwa zaidi ya kushiriki katika fursa zinazopatikana kwa mtangamano wa Afrika Mashariki na ni kweli kabisa nimweleze Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara iko tayari kabisa kuangalia ni namna gani inasaidia jamii na Wilaya zinazopakana na nchi za jirani ili kuweza kutumia fursa hizo. Naomba nimweleze tu kwamba, hilo siyo kwamba ndiyo linaanza sasa, ni kwamba kama nilivyoeleza katika swali la msingi, tayari Wizara inatoa elimu na ufahamu kwa wananchi kutambua fursa zilizopo ili waweze kuzitumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuhusu Wizara kuandamana naye ili kufika Jimboni na kuangalia hizo fursa, naomba nilichukue hili, nitamshauri Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje ili waangalie namna ya yeye au Naibu Waziri na timu yake waweze kwenda kwa Mheshimiwa Mbunge ili waweze kuangalia namna ya kutumia hizo fursa kwa ukaribu zaidi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefikia mwisho wa kipindi cha maswali na majibu. Nitaleta kwenu matangazo tuliyonayo halafu tutaendelea.

Tunao wageni waliopo Bungeni asubuhi hii; kundi la kwanza ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge halafu na wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Tutaanza na wageni wa Waheshimiwa Wabunge.

Wapo wageni 83 wa Mheshimiwa Angellah Kairuki, ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambao ni watumishi kutoka Ofisi ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa, wakiongozwa na Ndugu Charles Magaya ambaye ni Kaimu Mkurugenzi Mkuu Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka. Wote wasimame kwa pamoja na karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 12 wa Mheshimiwa Elias Kwandikwa ambao ni wanafunzi wanaosoma Chuo Kikuu cha Dodoma kutoka Ushetu, Mkoani Shinyanga, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni watano wa Mheshimiwa Cosato Chumi ambao ni familia yake wakiongozwa na mdogo wake ambaye ni Ndugu Andrew Hansy, karibuni sana watoto wetu na mdogo wetu. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 11 wa Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa na Mheshimiwa Joseph Mbilinyi kutoka Chama cha Kuweka na Kukopa *(UWAMU SACCOS)* ya Uyole Mkoani Mbeya, wakiongozwa na Ndugu Rose Mlaya ambaye ni Mwenyekiti wa *UWAMU SACCOS,* karibuni sana wageni wetu.

Pia wageni watatu wa Mheshimiwa Oran Njeza, ambao ni walimu kutoka Mbeya Vijijini, karibuni sana walimu wetu. *(Makofi)*

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Doto Biteko ambaye ni mpiga kura wake kutoka Bukombe, Mkoani Geita, ambaye anaitwa Ndugu Shadrack Katendele, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Innocent Bashungwa, ambaye ni Diwani kutoka Karagwe, huyu ni Mheshimiwa Sabi Rwazo, karibu sana Mheshimiwa Diwani. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 13 wa Mheshimiwa Angeline Mabula ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni waliotutembelea kwa ajili ya mafunzo na hawa ni wanafunzi 120 na walimu watano kutoka Shule ya Sekondari *St. Marys Duluti* iliyoko Mkoani Arusha, karibuni sana vijana wetu. *(Makofi)*

Tunao pia wanafunzi wanne kutoka Chuo cha Maabara Nkinga kilichopo Mkoani Tabora, karibuni sana. *(Makofi)*

Hao ndio wageni waliotufikia asubuhi ya leo, lakini ninayo matangazo mengine.

Waheshimiwa Wabunge, mnatangaziwa kuwa Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Uongozi, leo Jumatano tarehe 15 Juni, 2016 kutakuwa na Mkutano saa 7.00 mchana. Kikao hicho kitafanyika katika Ukumbi wa Spika, Wajumbe mnaombwa kuhudhuria kikao hicho bila kukosa na kwa wakati.

Tangazo lingine ni la kikao cha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii na hawa wanatangaziwa kwamba mara baada ya Bunge kuahirishwa saa 7.00 mchana kutakuwa na kikao cha Kamati katika Ukumbi wa Msekwa ‘D.’ Kwa hiyo, Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii mnaombwa kuhudhuria bila kukosa. Tangazo limeletwa na Mwenyekiti.

Pia, lipo tangazo lingine; Waheshimiwa Wabunge mnatangaziwa kuwa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi, Muhimbili Sehemu ya Madawa Asilia, wanafanya maonesho ya bidhaa na huduma zitolewazo na Chuo hicho.

Maonesho hayo yanafanyika nje ya Ofisi ya Bunge kando kando ya barabara iendayo Dar es Salaam. Hivyo Waheshimiwa Wabunge mnaalikwa kwenda kuona bidhaa na huduma zitolewazo na chuo hicho. Waheshimiwa Wabunge wote mnaalikwa, kwa hiyo, mwende mkatembelee maonesho hayo.

Pia lipo tangazo la ibada, yaani Misa Takatifu ya Kanisa Katoliki. Waheshimiwa Wabunge mnatangaziwa kuwa Wabunge ambao ni Wakatoliki na wasio Wakatoliki leo tarehe 15 Juni, 2016 saa 7.00 mchana mara baada ya kuahirisha shughuli za Bunge kutakuwa na Misa Takatifu kwa Wakristu wote, wote mnakaribishwa. Tangazo limeletwa na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Mtakatifu Thomas More ambaye ni Mheshimiwa Joseph Selasini.

Tangazo la mwisho linatoka kwa Mheshimiwa Leonidas Tutubert Gama ambaye ni kocha maarufu wa mchezo wa kuvuta kamba. Anawatangazia wale wote waliojitokeza na kujiorodhesha kushiriki mchezo wa kuvuta kamba kwamba leo saa 7.00 mara baada ya kuahirisha Bunge anaomba mkutane katika Ukumbi wa Msekwa kwa dakika chache tu ili mkubaliane mambo muhimu ikiwa ni pamoja na ratiba ya mazoezi na mechi za majaribio za kuvuta kamba. Mpaka sasa timu imeshafikia watu 39, nadhani hapo nasubiriwa mimi niwe namba 40. *(Kicheko)*

Kwa hiyo, Waheshimiwa wa timu hii mnaombwa mkutane na kocha wenu Mheshimiwa Gama. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuyasema hayo, tunaendelea na ratiba. Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA - KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka wa fedha 2015 na Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017**

**na**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2016/2017**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na kujadili hoja ya Waziri wa Fedha na Mipango. Tutaanza michango yetu na Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga, atafuatiwa na Mheshimiwa Martha Umbulla na Mheshimiwa Peter Serukamba, ajiandae.

**MHE. KISWAGA B. DESTERY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabla sijaanza kuchangia nianze kuweka rekodi sawa sawa. Hapa ndani kwa sababu kuna Wabunge wenzangu wakati mwingine wanasema kwamba Mawaziri waache siasa. Nataka niongee tu jambo hili; kwanza siasa ni taaluma; na sisi tuliopo wote hapa tumeingizwa kwenye siasa. Siasa ni ngumu sana, lakini ni nzuri sana, tatizo ni tunavyoitumia tu kama wenzetu wanavyoitumia vibaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kupata Ubunge ni kazi kweli kweli na suala la kupata Urasi ni kazi kweli kweli! Sisi ambao tumepita kwenye mchakato huu tunajua joto lake. Kwa hiyo, hata wote tunapokuwa humu tumebeba mizigo; wa kuteuliwa, sijui wa kutoka *group* gani, inategemea mizigo hiyo ina uzito gani; lakini uzito wa Jimbo ni uzito kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema kwamba duniani kote hakuna mtu anayehitaji kulipa kodi. Hata vitabu vya dini vimezungumza sana suala la kulipa kodi na aliyekuwa akitoza kodi wakati wa Yesu alikuwa ni mtu ambaye anachukiwa na Umma wote. Kwa hiyo, Serikali kukusanya kodi isiogope, ni jambo la kawaida, ndiyo uhai wa Serikali. Naiomba sana Serikali hii isirudi nyuma, ihakikishe inakusanya kodi ili wananchi waweze kupata huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na suala la maji. Suala la shilingi 50 kuongezwa kwenye dizeli na petroli ili iende kugharamia maji, ninasikitika sana, kwamba Serikali imeona kwamba ikiongeza shilingi 50 italeta mfumuko wa bei. Nataka kuuliza au mmeshatuuliza? Sisi Wabunge humu ndio watumiaji wa mafuta. Tumeshakataa kuongezwa hii shilingi 50? Sisi tumeshakubali tuongezwe shilingi 50 kwenye petroli pamoja na dizeli ili kugharamia Mfuko wa Maji Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sera yetu inasema mita 400 wananchi waweze kupata maji. Kwa namna hii tunayokwenda, hatutaweza kuifikia hiyo sera na mwaka 2020 tutapata taabu kweli kweli kurudi humu Bungeni, kwa sababu wakina mama wanateseka kila asubuhi, kila saa kumi na moja wanakwenda kuteka maji. Tuwahurumie! Wanapoteseka akina mama na sisi akina baba tunateseka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siku moja nimewahi kusema asali ni tamu sana lakini wako watu hawaitumii asali, lakini kila mmoja anaguswa na maji; awe mtumia gari, anaguswa na maji aoshee gari lake. Kwa hiyo, naishauri Serikali hii ya Awamu ya Tano, Serikali ya kazi; kwa sababu unaweza kuwa na Serikali

sikivu, ikawa inasikia tu, isifanye kazi. Sasa hii ni Serikali ya kazi, ifanye kazi kuongeza shilingi 50 ili akina mama waweze kupata maji ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaongea haya kwa sababu nimetoka Jimboni, hali ni mbaya, akina mama wanasumbuka na mimi nina hali mbaya! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ungenionea huruma ukanipatia chupa ya maji hapa ili niweze kuongea vizuri huku nakunywa maji. Naomba hili, wala halipaswi kujadiliwa, iongezwe shilingi 50 kwenye mafuta, wala tusijadili hili; kama haitaongezwa, kama kuna kushika shilingi, mimi nitashika shilingi kwa sababu ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeangalia kwenye fedha za ujenzi wa zahanati. Ilani yetu inazungumza kwamba kila Kijiji kiwe na zahanati; kila Kata iwe na vituo vya afya. Humu tuliomo ndani humu na wengine tunachagua mahali pa kwenda kupata matibabu, lakini mwananchi wa kawaida, maskini, hana hata mahali pa kwenda kupata matibabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zahanati ni jambo la muhimu sana kujenga ili kuhakikisha wananchi wetu wanapata huduma hii. Sasa kama Ilani yetu inazungumza kwamba tuwe na zahanati kila kijiji, tuwe na kituo cha afya, wananchi wameshaandaa maboma ya kutosha, wanasubiri fedha za Serikali ili Serikali iwaunge mkono; tupelekeeni fedha hizo ili kupunguza matatizo ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali imekuja na mpango wa kupunguza kodi kwenye mazao, lakini nimeangalia kwenye zao la pamba; kilichoondolewa kile siyo tija kwa wananchi. Umeondoa mwenge, umeondoa kikao ambacho ni fedha ambazo zinalipwa na jina, ni hela kidogo sana hizo. Tunazungumzia shilingi 400,000 kwa jina; hiyo inaongeza nini kwenye bei ya pamba?

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo kodi mbalimbali *cess* za Halmashauri, kuna *CDTF,* mfuko wa kuendeleza zao la pamba; hizi zote inapashwa Serikali ifidie ili mkulima aweze kupata bei nzuri. Tusipofanya hivyo, zao la pemba linakwenda kufa. Sasa mnapozungumzia viwanda, kwa mazao yapi? Mnapozungumzia viwanda, kwa sababu viwanda vinavyoongeza ajira ni viwanda ambavyo malighafi yake ni pamba. Hili Mheshimiwa Waziri wa Fedha aliangalie ili tuweze kuona ni jinsi gani tunaweza kuwasaidia wakulima wa pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ziko kodi ambazo Mheshimiwa Rais alikuwa anasema ataziondoa; kodi zenye kero, lakini naona kama hatujaziondoa hivi.

**MBUNGE FULANI:** Kabisa.

**MHE. KISWAGA B. DESTERY:** Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wana shida, akina mama ntilie, sokoni wauza nyanya na michicha wana shida. Tungeangalia jambo hili kwa mapana yake, upo ushuru hauna tija, hata Halmashauri haiongezei kitu chochote. Naomba anakapokuja kumalizia hapa atuambie, hizi kodi ambazo Mheshimiwa Rais aliahidi, ushuru wenye kero, utaondolewa kwa namna gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie tu kuongeza usajili wa bodaboda. Hili ni kundi ambalo ni maskini sana, lakini ni kundi ambalo linarahisisha usafiri wa wananchi wetu vijijini ambako gari hazifiki. Yapo maeneo barabara haziko; wanaotusaidia ni hawa watu wa bodaboda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tunapoongeza usajili maana yake tunataka kuwapunguza hawa watu. Kama tungeacha kodi ilie ile, ingechochea kuingiza bodaboda nyingi zaidi, ikachochea hao bodaboda kununua mafuta mengi zaidi na kuongeza uchumi wa nchi hii. Naomba hili nalo liondolewe; halina sababu na halina tija sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wamezungumza suala la *CAG,* na mimi naendelea kusema nilikuwa Mwenyekiti wa Halmashauri, chombo hiki ni muhimu sana; chombo hiki ni cha kitaalam. Mheshimiwa Profesa Muhongo anasema haya ni mambo ya kitaalam.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama haya ni mambo ya kitaalam halafu tunayapunguzia fedha, itakuwa ni aibu. Halmashauri zitakuwa na hali mbaya na Wizara zitakuwa na hali mbaya. Naomba fedha ziongezwe ili tuweze kuhakikisha udhibiti wa fedha hizi tunazozipeleka, zinakuwa na uhakika zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yako mambo duniani huwa hayajadiliwi. Suala la mafao kwa Wabunge ni jambo ambalo duniani halijadiliwi. Ku-*maintain* Jimbo ni sawasawa na kujenga kiwanda cha kati. Wabunge hawa wabishe. Ku-*maintain* Jimbo ni sawa na kujenga kiwanda cha kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba hili liondolewe mara moja, halina mjadala, halina nafasi ili kuhakikisha kwamba Wabunge hawa sio *pensionable*. Mbunge hapa akienda kupigwa dafrao, unaweza kumshangaa, ni hali ngumu. Naomba hili kwa kweli lisiingizwe, wala lisijadiliwe na liondolewe mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naendelea sasa kuipongeza Serikali, kazeni buti kukusanya kodi ili huduma za wananchi zipatikane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Martha Umbulla, atafuatiwa na Mheshimiwa Peter Serukamba na Mheshimiwa Doto Biteko ajiandae.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru kupata nafasi hii na mimi nichangie hoja iliyoko mbele yetu. Na mimi nichukue fursa hii kwanza kukupongeza wewe binafsi kwa umahiri wako na ushupavu wako wa kuliongoza vyema Bunge letu, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja iliyoko mbele yetu ni mwelekeo wa utekelezaji wa bajeti ya 2016/2017 na katika kuliangalia hilo, ni lazima tuangalie utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2015/2016 ili tuweze kujifunza tulikosea wapi na vipi tujisahihishe ili tuweze kwenda vizuri kwa bajeti yetu ya mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika vipaumbele vilivyowekwa katika bajeti ya 2015/2016 mimi nimevichukua viwili ili niweze kuvichambua tuone ufanikiwaji ulikwenda kwa kiwango gani? La kwanza kabisa, kipaumbele chetu cha kwanza ilikuwa kupunguza umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la kupunguza umaskini, tukiangalia katika jamii zetu, kwa mabilioni na matrilioni ya fedha tulizowasomea wananchi mwaka 2015, ni kwa kiwango gani umaskini umepungua baina ya jamii yetu ya Watanzania. Hali bado ni mbaya sana vijijini, wananchi wetu bado hawana milo mitatu, wananchi hawana nyumba bora za kuishi, wananchi wetu bado hawana vyanzo vya uhakika vya fedha na kwa hiyo, ni vizuri kutafakari, ni kwa namna gani umaskini utapungua katika nchi yetu hasa kwa bajeti hii ya mwaka 2016/2017. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kujipima hivyo, ni vizuri pia tukaangalia changamoto zilizojitokeza, changamoto kubwa ambayo imejitokeza katika kupunguza umaskini baina ya jamii zetu, kubwa ambalo limeonekana ni upatikanaji wa rasilimali fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona Serikali imeweka mfumo thabiti wa ukusanyaji wa fedha katika bajeti ya mwaka huu na zaidi sana ni hili la kutumia *electronic machines.* Mfumo huu bado una changamoto kubwa sana. Pamoja na kuweka mikakati na adhabu zitakazotolewa kwa ajili ya watakaokiuka kutoza kutumia mashine hizo, bado mimi nina wasiwasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika vituo vya petroli, kwa mfano, wakikwambia mashine hii ni mbovu ama iko *out of order* na ni kweli utakavyodhihirika hivyo, bado utakapomchukulia hatua mfanyabiashara ambaye mashine yake hiyo ni mbovu, utakuwa hujamtendea haki. Kwa sababu utakuta ni ukweli na umempa adhabu na kutakuwa na msururu wa watu kutaka huduma na watakapokosa huduma ya kupata petroli na dizeli wataleta lawama tena kwa Serikali. Kwa hiyo, nadhani tuangalie ni namna gani tutaboresha mfumo mzuri wa ukusanyaji kodi ili tuweze kutekeleza miradi yetu ya maendeleo katika Vijiji vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine nililotaka kuishauri Serikali ni kwamba bajeti iendane na tathmini halisi ambayo tumeiona katika utekelezaji wa kipindi kilichopita. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuona kwamba pamoja na jitihada za kupunguza umasikini ametenga shilingi milioni 50 kila kijiji. Dhamira yake ni njema na itakapotekelezwa itakwenda vizuri. Utekelezaji watatengeneza wataalam, lakini bado ametenga fedha hizo ili kuona ni namna gani umasikini utapungua katika jamii zetu. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, kipaumbele cha pili, kilikuwa upatikanaji wa huduma za jamii. Kilio kikubwa cha Waheshimiwa Wabunge tangu waanze michango humu tumeona ni kilio cha maji. Maji bado ni tatizo kubwa katika jamii zetu na kwa hiyo, kwa bajeti ya mwaka 2016/2017 ni vizuri kuendelea kubuni mikakati bora ya kuhakikisha kwamba wananchi wanapata maji. Sasa utaratibu uliopo, naipongeza pia Serikali kwa kutenga hiyo asilimia ndogo ya kuongeza kwenye tozo ya mafuta ya shilingi 100. Nina uhakika shilingi bilioni 250 zitakapopatikana, shilingi bilioni 220 zikienda kwenye usambazaji wa maji vijijini itasaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ni mkatakati mzuri na mimi nauamini kwa sababu tozo ya kwenye mafuta na petroli ni tozo yenye uhakika, kwa sababu huduma hiyo ipo kila siku na tumeona kwenye miradi ya *REA* pia. Tozo zilizowekwa kwenye *REA* imetusaidia kusambaza umeme vijijini na kwa hiyo, hiki ni chanzo ambacho kinaweza kikatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma nyingine ya jamii ni suala la elimu. Nampongeza tena Mheshimiwa Rais kwa kuleta mfumo wa elimu bure, nina hakika tathmini mwisho wa siku itakwenda vizuri katika kuboresha elimu katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije katika suala zima la huduma za afya. Huduma za afya ni kipaumbele kingine cha pili baada ya maji. Suala la afya hasa kwa kabrasha hili ambalo limetolewa na TAMISEMI kwa Mkoa wangu wa Manyara, ni masikitiko makubwa sana. Nimeona katika taarifa hii iliyotolewa na

TAMISEMI na hasa ikishirikiana na Wizara ya Afya; Mkoa wa Manyara katika mlolongo wa kuodhoresha zahanati na uboreshaji na ukarabati wa vituo vya afya, nimesikitika kuona Wilaya ya Simanjiro imewekewa zahanati moja tu, wakati Mikoa mingine na Wilaya nyingine zina zahanati mpaka 10 hadi 15. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hivyo tu, Wilaya ya Kiteto kubwa kama hiyo, imewekewa zahanati tatu tu. Tena cha kusikitisha fedha ambazo zitakwenda kukarabati majengo hayo ni *Capital Development Grants* ambazo mara nyingi wala hazipatikani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inasikitisha kwa Mkoa wa Manyara, sijui mikoa mingine imetumia mbinu gani kuhakikisha kwamba wamewekewa fedha za kutosha, lakini naiomba Wizara na Serikali na hasa maeneo husika kwamba waangalie hili. Wilaya ya Mbulu ina Majimbo mawili, lakini zahanati na vituo vya afya vilivyoorodheshwa hapa na vya Jimbo la Mbulu Mjini; tunaishukuru Serikali kwa hilo kwa sababu na mimi natokea huko, lakini ni vizuri kuiona Mbulu Vijijini kwani hakuna hata zahanati moja iliyoorodheshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeliona kabrasha hili nikadhani kwamba ni makosa yamefanyika, naamini kwamba wahusika watakwenda kuiangalia vyema na kuhakikisha kwamba kila Wilaya inanufaika na usambazaji ama upatikanaji wa huduma za afya ikiwepo kujenga zahanati na vituo vya afya katika kila kijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kidogo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Eeh, naomba kuendelea.

**NAIBU SPIKA:** Kengele ni ya pili hiyo Mheshimiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Peter Serukamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Doto Biteko na Mheshimiwa Dkt. Hadji Mponda ajiandae. Mheshimiwa Peter Serukamba nimeletewa taarifa hapa kwamba Mbunge wa Kibaha Mheshimiwa Hamoud wa Kibaha amekupa dakika zake tano. Kwa hiyo, Katibu tafadhali uzingatie hilo.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami naomba nikupongeze, nimpongeze Waziri wa Fedha na watendaji wote na nashukuru kwa nafasi hii uliyonipatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumwomba Waziri wa Fedha. Rais alipokuja Kigoma moja ya jambo ambalo alituahidi ni suala la tozo kwenye zao la kahawa ambalo lina tozo 26. Alisema hizi tozo lazima ziondoke. Namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kujibu, atuambie kwa nini hakuona umuhimu wa kutoa tozo hizi kwenye zao la kahawa? Ni kwa nini tunaomba tozo hii zipunguzwe? Ni kwa sababu bei ya soko la kahawa imepungua duniani. Namna ya kuwasaidia wakulima wetu ni kupunguza tozo hizo ili waweze kufaidika na zao la kahawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni suala la maji kwenye Jimbo la Kigoma Kaskazini. Tatizo la maji ni kubwa sana, lakini tuna *Lake Tanganyika.* Namwomba sasa Waziri wa Fedha aje na mipango atuambie lini tutaanza kuyatumia maji ya *Lake Tanganyika*; siyo kwa Kigoma Mjini, ni kwa ajili ya Jimbo la Kigoma Kaskazini pamoja na Mkoa mzima wa Kigoma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpongeze Waziri wa Fedha, anapeleka asilimia 40 kwenye maendeleo. Kwa vyovyote vile haya ni mageuzi makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetafakari sana asilimia 40 maana yake nini? Asilimia 40 Mheshimiwa Waziri wa Fedha, maana yake unaenda kutengeneza umeme, majenereta utayanunua nje, kwa hiyo, tuta-*save* fedha zetu, tutatoa dola kupeleka nje kupata umeme. Tutatoa dola kutengeneza reli, maana itabidi tuchukue kwanza shilingi, tutawalipa wakandarasi, kwa vyovyote vile watakuwa wa nje. Kwa hiyo, hela itakwenda nje; tunanunua ndege, fedha itakwenda nje. Maana yake ni nini? Tuna-*save* kama nchi kwa shilingi yetu; itabidi tununue dola kununua hizi *services.* Ili tuweze ku-*strike a balance* lazima na sisi tuwe na eneo ambalo litatuingizia dola nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ndipo ambapo wachumi wetu tungewaomba watusaidie. Ninayo maeneo makubwa matatu ambayo nataka niwashauri watu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la kwanza ni suala la *tourism.* Wanaoshindana na sisi kwenye utalii ni Kenya, Uganda, Rwanda, Mauritius na *South Africa*. Wenzetu hawajaweka *VAT* kwenye utalii, maana yake tunaifanya Tanzania iwe *destination* ambayo ni gharama na utalii mtu hawezi kuja.

Mheshimiwa Waziri wa Fedha, tukiweka *VAT* uwe na uhakika katika watu ambao wataumia zaidi ni Wazanzibar na uchumi wa Zanzibar. Kwa sababu uchumi wa Zanzibar unategemea *tourism* na *tourism* ya Zanzibar iko *packed* pamoja na utalii wa Kaskazini. Mtu angependa aende Zanzibar, aende na Serengeti; aende Mikumi aende na Zanzibar. Naombeni hili jambo tuliangalie kwa umakini mkubwa sana. *(Makofi)*

Sehemu ya pili ambayo itatuingizia dola ambayo lazima wachumi wetu tukubaliane, ni suala la kwenye masoko ya mitaji. *Dar es Salaam Stock Exchange* tuliamua kuwapa *incentive* kwenye *capital gain* ili watu wengi wapeleke, waende waka-*list* pale. Waki-*list* kwenye *DSE* maana yake ni nini? Maana yake ni mitaji tutapata *liquidity,* maana yake ni *job,* ndiyo tutafanya uchumi uchangamke.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Gavana wa *BOT*, ame-*liberalize account* ya nje ndiyo maana sasa *DSE* kuna watu wanatoka nje wanakuja kununua *share;* lakini ukiweka hiyo kodi maana yake watu wataondoka *Dar es Salaam Stock Exchange*. Hata anachotaka kukipata, hakitafanikiwa.

Kwa hiyo, nakuomba sana Mheshimiwa Waziri, walioamua kuweka zile *incentives* kwa ajili ya soko letu lichangamke, naamini walifikiri vizuri. Haiwezekani tuziondoe leo sisi, nakuomba sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hiyo tu, hata kukusanya hiyo kodi ni ngumu sana; maana *capital gain tax* ni wakati gani? Mimi nina *share* 200 nimeuza, pale nikizidisha ndiyo unakuja unakata, kwa sababu watu wote hatuuzi *share at a time*. Kwa hiyo, unachotaka kukipata unaweza usikipate mwisho wa siku. Kwa hiyo, suala hilo litakuwa ni gumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la tatu, jana Mbunge mwenzangu wa Kahama amelisema, sijui kama nitafanikiwa kulieleza kama alivyolieleza. Ametuambia jambo jipya, lakini limekuwepo, mwaka 2011 Kamati ya Madini na Nishati walilisema kwamba umefika wakati tufungue soko la dhahabu Tanzania. Tunalifunguaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tuweke mazingira kwamba kila anayekuja na madini yoyote Tanzania, halipi hata shilingi moja. Halipi kodi yoyote, lakini atakayetaka kuyatoa madini hapa Tanzania, tusichukue kiasi kikubwa, unaya-*export* 1% tu.

Mheshimiwa Waziri wa Fedha ngoja nikwambie kitakachopatikana; tukiamua kufanya hivyo, unayo hakika kwa mwezi tutapata siyo chini ya tani 20 za dhahabu peke yake. Watu watakaokuja kununua hapa, ile dhahabu moja kilo moja ni dola 40,000. Maana yake ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, unapozi-*export* maana yake unachukua dola 40,000 unazidisha kwa hizo kilo 20,000 utapata karibia dola milioni 800; ukizidisha kwa hela ya Tanzania ni *1.6 trillion*. Maana yake ni nini? Asilimia moja ni shilingi bilioni 16. Kwa hiyo, kwa mwaka una hakika utapata shilingi bilioni 200. Shilingi bilioni 200 ni Wizara ngapi umezipa fedha? Ni nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa watu watakaokuja hapa, watanunua vyakula vyetu, tutapata kwenye *VAT*, tutapata kwenye hoteli zetu, watanunua kwenye masoko yetu. Naombeni wachumi wetu wakati wa kutumia mambo ya kwenye vitabu, tuanze na mambo ambayo ni *practical,* tuyasimamie, tutabadilisha nchi yetu. Ndiyo maana tunataka kuweka kodi kila eneo kwa sababu tunataka kufikiria maeneo yale yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nasema ile 48% ambayo tutaipeleka kwenye maendeleo, tutafute namna ya kuirudisha ndani. Namna ya kuirudisha ndani Mheshimiwa Waziri wa Fedha, tunaomba twende kwenye *tourism,* tuanzishe soko la dhahabu, lakini pia tuwe na *incentive* kwenye *Dar es Salaam Stock Exchange* ili watu wengi waweze kuja hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ningependa nichangie baada ya kutoka hapa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ni suala la viwanda. Bajeti yako inaimba neno "viwanda." Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ukisoma historia ya watu ambao wameendelea juzi tu kwenye viwanda, kuna mambo lazima tukubali kuyakosa. Ni aidha upate viwanda ama upate kodi. Ukianza na kodi hatuna viwanda; tukubaliane! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *leather industry,* kwa maana ya *Leather Industry in Ethiopia.* Wanasema imefanikiwa kwa sababu *one,* hakuna kodi kwenye *capital goods;* hakuna kodi kwenye *construction materials;* kuna *cheap electricity;* kuna *cheap labour.* Wamepewa miaka sita kutolipa *income tax.* Wamepewa *holiday! (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unachotafuta kwenye viwanda, kitu cha kwanza ni ajira. Watu wetu wakishakuwa na ajira watakuwa na *purchasing power.* Kwa hiyo, kodi yako utaipata, ni *indirect tax,* utaipata tu! Cha pili, ni bidhaa ziwepo sokoni. Kodi ni sehemu ya tatu unapoongelea kwenye ule mnyororo wa viwanda. *Target* ya kwanza ni ajira, bidhaa, ndiyo unakuja kodi na unakuja kuangalia *GDP* yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Wizara ya Fedha, tuliangalie hili eneo. Kama hatujajiandaa, tutasema sana kwenye vitabu, lakini tunaweza tusifanikiwe na nia yetu ni kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la *sunflower. Sunflower* imeongezeka, ilianza kidogo, sasa hivi imefika tani 180,000; maana yake *industry* inakua. Sasa tukiweka kodi kwenye *crude oil* maana yake unasema hakuna haja nilete *crude oil,* acha nilete *refined oil* ili nilipe 25% niuze; lakini utakuwa umepoteza ajira za watu wangapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vitu vingine tunavifanya ili kulinda viwanda, ili kulinda ajira, hili ndiyo la msingi kama Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nilitaka niongelee suala la *PPP*. Suala hili linasemwa sana kwenye vitabu, lakini kwenye matendo halionekani. Namwomba sana Waziri wa Fedha, sheria ipo, kanuni zipo, tuanze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwaulize Waheshimiwa Wabunge wenzangu, hivi kweli karne hii leo tunaweka bajeti kununua ma-*generator* ya umeme, wakati ukitangaza, utapata watu wengi tu wa kununua majenereta ya umeme. Kwa nini tuweke hela ambayo tungeipeleka kwenye afya, elimu na maji? Ni jambo ambalo ukiwaita wawekezaji watakuja, unachotakiwa kuweka ni *tarrifs* ambazo watu wako watafaidi kama Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuweke mazingira ya kusema, unataka kuja kuleta umeme Tanzania? Eeh, lazima uwe na Mtanzania mwenye 30% mpaka 40%. Haya tukiyafanya, tutaenda mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna Mashirika ya Serikali, mimi nitatoa mfano wa shirika moja tu. Mafuta ya ndege Tanzania, Puma ndiyo wana-*manage* 90%, lakini eti tunampa mtu mwingine aagize ndiyo amletee Puma na sisi tuna *share* kule 50%. Hivi nani ambaye hajipendi? Lazima tufike maeneo mengine tufanye maamuzi kwa sababu tuna *interest* kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi tumemwona Waziri wa Fedha anapokea *dividends.* Maana yake ni nini? Kwamba, tukiwapa biashara kubwa, tutapata fedha nyingi kama Taifa. Tukipata fedha nyingi, tutachangia kwenye uchumi wa nchi, tutachangia kwenye maendeleo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba watu wa Serikali, tusaidieni. Yale maeneo ambayo tuna *interest* kama Taifa, tusione aibu kutumia makampuni yetu. Tusione aibu hata kidogo, kwa sababu tukiogopa tunafanya nini? Tutakuwa tunaongea huku, mkono huu tunafanya kitu cha ajabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, cha mwisho nataka niongee suala la *Kurasini Logistic Centre.* Nimesoma hapa suala la Kurasini. Suala hili ni jema sana, lakini nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge, ukisoma kwenye Mpango wa Miaka Mitano, Waziri wa Fedha anasema kwenye mpango ule kwamba kuna kampuni za Kichina zitakuja kufanya biashara pale Kurasini; jambo jema, tutapata bidhaa za bei rahisi; lakini mnajua maana yake? Maana yake tumewaua Wakinga, tumeua Wachaga, Kariakoo tumeiua. Maana yake hawawezi ku-*compete. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wale watakaoleta mizigo yao kutoka kule China watapewa *export guarantee,* watapewa *incentive* na nchi zao, anakuja anauza bei ambazo umeweka wewe; wewe utakuwa na gharama. Sisi tutakuwa ni *expensive;* watu wote watakwenda pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, najua *argument* ya baadhi ya watu wanasema, ukifungua *Logistic Centre* ile kitakachotokea nchi zote zilizotuzunguka zitakuja kununua Tanzania. Sawa nakubali, lakini zikinunua Tanzania, yule anayeuza ni Mchina, sio Mtanzania! Maana yake fedha zile zinakwenda China. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukubaliane jamani, moja ya mambo ambayo tusipokuwa waangalifu tukiwaondoa hawa wafanyabiashara wa katikati, tunaua *economy* yetu. Tukubaliane, hatuwezi kuendelea bila Watanzania wengi kuwa matajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii habari ya kufikiria Watanzania wakiwa maskini ndio tutaendelea, haiwezekani. Tutapata kodi nyingi wakiweko wafanyabiashara wengi zaidi. Tuweke mazingira ya kukusanya kodi, lakini tuweke mazingira ya kulinda biashara za watu wetu. Tulete mazingira ambayo kule ambako tunafanya biashara kama Serikali, tuhakikishe tunawapa biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tusipofanya hivyo, Mungu ametupa jiografia nzuri sana Tanzania; maeneo haya tuliyopewa kama nchi tuyatumie kibiashara. Tanzania tuna amani, Tanzania tuna mvua, Tanzania tuna maji, tuna mito, tuna *lakes,* tuna *everything!* Sasa kwa nini tusitumie jiografia yetu hii kwa ajili ya maendeleo yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba wachumi wetu wakae tufikiri; tusidhani tutakuwa tunafanya mambo kama tunavyofanya miaka yote, mambo yamebadilika sana. Naiomba sana Wizara ya Fedha itusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho na mimi niliseme, nimesikitika kidogo. Mheshimiwa Waziri wa Fedha anasema, katika mikoa maskini ni Kigoma, Mwanza na mingine aliyoisema. Hapa tuulizane Waheshimiwa Wabunge; hivi kweli jamani Mwanza ni maskini kuliko Katavi? Mwanza ni maskini kuliko Lindi? Mwanza kweli kuliko Pwani! Maana Pwani ni nchi katika nchi ambazo zimefanya vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka Mheshimiwa Waziri wa Fedha, atuambie vigezo vyake vya kupima umasikini ni vipi? Ni idadi ya watu au ni nyumba? Ni kitu gani kinapima umaskini? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwanza ambako wana ng'ombe; Mwanza ni wavuvi; Mwanza kuna dhahabu; inawezekanaje wawe maskini kuliko watu wa Lindi? Inawezekanaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiniambia Kigoma, Mwanza, nitaelewa. Kigoma maskini nakubali; lakini hata mimi ukiniambia Kigoma ni maskini sikubali sana; ndiyo Mkoa pekee hatujawahi kupewa chakula toka uhuru wa nchi hii. Halafu watu hawa eti ndio maskini. Tunakuwaje maskini? Kwa hiyo, naomba *data* zetu tuziangalie upya. Naamini liko tatizo kwenye kuandaa hizi *data* zetu za watu wa Mipango. Kabisa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa ni suala la pensheni. Nimwombe Waziri wa Fedha, suala la pensheni…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Peter Serukamba, dakika zako 15 zimeisha na zile ulizokuwa umepewa pia umeshazimaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Doto Biteko, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Hadji Mponda na Mheshimiwa Ali Hassan King ajiandae.

**MHE. DOTO M. BITEKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii, na mimi nichangie Bajeti Kuu ya Serikali. Kabla ya kufanya hivyo, naomba tena nimshukuru Mungu kwa nafasi hii, ambaye amenipa uhai niweze kusimama tena mbele yako ili niweze kusema machache.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikupongeze sana wewe binafsi kwa namna unavyoliendesha Bunge letu. Wewe umekuwa kamanda wa makamanda; tumeona hapa makamanda wanakukimbia kila ukitokea; na hiki ni kiashiria kwamba wewe hutishiki, uko imara. Na mimi nakuhakikishia tu kwamba sisi Wabunge wenye nia njema tuko pamoja na wewe. Endelea kutuongoza kwa kufuata kanuni zetu na taratibu tulizojiwekea, bila shaka na Mungu atakubariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa bajeti aliyoiwasilisha. Bajeti hii bila shaka inatutatulia changamoto nyingi, lakini yako mambo ambayo nadhani yanahitaji kuboreshwa kidogo; na kwa maoni yangu ndiyo haya yaliyonifanya nisimame. Nianze na sekta ya elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya elimu imetengewa jumla ya bajeti ya shilingi trilioni 4.8 na unafahamu kwamba kwenye Azimio la Dakar tulikubaliana kwamba kila nchi itenge 6% ya *GDP* yake ipelekwe kwenye elimu. Ukiangalia hapa, pesa ambazo tunapeleka kwenye elimu shilingi trilioni 4.8, fedha nyingi

kati ya hizo tumesema, zinazokwenda kwenye maendeleo ni shilingi bilioni 897.7 na shilingi bilioni 427.6 zinakwenda kwenye matumizi mengineyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizi za maendeleo zilizotengwa; 50% yake inakwenda kwenye mikopo ya wanafunzi. Kwa maoni yangu naona inaondoa dhana ya maendeleo, inaingia kwenye dhana ya matumizi mengineyo. Na mimi ninadhani, hizi fedha ambazo zimepekwa kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi, zilipaswa zitoke kwenye kifungu cha maendeleo zije kwenye kifungu cha matumizi kwa sababu zenyewe zinakwenda kutumika kwa ajili ya kuwapatia mikopo wanafunzi. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri aje atueleze kwa nini fedha hizi zinapelekwa kwenye maendeleo badala ya matumizi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumezungumza miaka mingi, na mimi kabla sijawa Mbunge nilikuwa nafutailia Bunge hili. Kwa muda mrefu tumekuwa tukihangaika na kuifanya Idara ya Ukaguzi kuwa Wakala wa Ukaguzi wa Elimu Tanzania. Elimu ya Tanzania hii dawa yale iko kwenye ukaguzi; elimu ya Tanzania ili iwe bora lazima kuwe na mtu ambaye anaiangalia kila siku. Idara ya Ukaguzi ambayo iko chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, leo Sayansi na Teknolojia; fedha inayopewa ni kidogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nenda kila kona ukaangalie, Idara ya Ukaguzi wana hali mbaya ya kifedha. Magari yao hata matairi hayana; magari yao hata mafuta hayana; uwezo wa kukagua kwa maana ya *capacity* ya wafanyakazi ni kidogo. Leo kwenye bajeti hii ukaguzi wametengewa 20% peke yake; fedha hizi ni kidogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa tunadhani kwamba tunapiga hatua, tunakwenda mbele kwa kuifanya Idara hii kuwa Wakala Maalum wa Ukaguzi wa Elimu nchini ili *quality assurance* tunayoizungumza kila mara iweze kuwa na uhakika zaidi, lakini leo ninaona tunarudi nyuma badala ya kwenda mbele. Naomba sana Idara hii iangaliwe, wafanyakazi wake, miundombinu pamoja na vitendea kazi, wapatiwe ili tuweze kukagua elimu ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka nilizungumzie ni kilimo. Kilimo kimetengewa shilingi trilioni 1.6 na kimebeba 4.9% ya Bajeti yote ya Serikali ukiondoa madeni. Mwaka wa 2014 walikopesha matrekta 118; mwaka 2015 wamekopesha matrekta 74 peke yake na mwaka huu tunarudi nyuma tena. Tulikuwa tunaamini kwamba kilimo ndiyo sekta ambayo inaajiri Watanzania wengi zaidi, tulipaswa kuweka nguvu zaidi pale kuliko kuiangalia kwa namna ambayo tunaiangalia hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikwambie mwaka huu wa kilimo na msimu huu wakulima wa pamba hawana habari njema wanayoielezea. Mbegu

waliyopewa haijaota. Nenda Bukombe pale, wakulima wanalalamika mbegu waliyopewa 73% tu ndiyo iliyoota, haikuota. Wamepewa dawa za kuua wadudu, hazikuua wadudu, lakini wakulima hawa hawana namna ya kufidiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Bunge hili tuiombe Serikali, wakulima ambao walipelekewa dawa ambazo hazikuua wadudu, wakulima ambao walipelekewa mbegu ambazo hazikuota, Serikali ije na *commitment* ya kuwafidia watu hawa kwa sababu, wametumia nguvu kubwa kuwekeza pale; na kilimo hiki ni mara moja baada ya mwaka mmoja. Tusipowapa kifuta machozi watu hawa, nataka nikuhakikishie mwaka mzima watu hawa watakuwa maskini kwa sababu kile wanachokitarajia hawatakipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie vilevile kwenye eneo la wachimbaji wadogo wadogo. Wilaya yetu ya Bukombe na Mkoa wa Geita, kama unavyofahamu, ni Mkoa ambao una dhahabu nyingi. Uchumi wa Geita unategemea dhahabu na ndiyo maana hata Mheshimiwa Serukamba alivyosema katika mikoa maskini, *indicators* au vigezo walivyovitumia kuifanya Geita kuwa mkoa wa pili kwa umaskini Tanzania hata mimi ilikuwa inanisumbua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuomba sana na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, fedha za ruzuku kwa ajili ya wachimbaji wadogo wadogo tuzipeleke. Shilingi milioni 900 hizi tulizozitenga zisiishie kwenye makaratasi, ziende kwenye *reality,* tuwapalekee wachimbaji wetu wadogo wadogo waweze kuchimba kisasa ili waweze kujikwamua kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Geita vijana wengi uchumi wao na hasa wa Bukombe, wanategemea uchimbaji wa dhahabu. Ukienda huko kila mmoja anakuuliza ni lini mnatuletea maeneo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimemsikia Mheshimiwa Naibu Waziri anasema kuanzia mwezi wa saba. Ninaomba mwezi wa Saba iwe kweli, wachimbaji wadogo wadogo waanze kuchimba. Tusianze tena kuambiwa bado tuko kwenye michakato. Jamani wamesubiri michakato muda mrefu, sasa hivi wanahitaji kuona matokeo ya kuchimba na wanapatiwa eneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kidogo ufugaji wa nyuki. Ufugaji wa nyuki ni eneo ambalo kwa Wilaya ya Bukombe limeajiri Watanzania wengi sana. Wako watu zaidi ya 6,000 wameajiriwa kwenye sekta ya ufugaji wa nyuki, lakini watu hao hawana mtu wa kuwasaidia, wanafanya kwa mizinga ya kienyeji. Nimeangalia takwimu kwenye Hali ya Uchumi wa nchi, kuanzia mwaka 2010 sekta ya ufugaji wa nyuki inashuka. Mwaka 2010 tani 428 tu; mwaka 2011 tukashuka, tukavuna tani 343; mwaka 2012 tukashuka, tukavuna tani 103; mwaka 2013 tukashuka, tukavuna tani 83. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wafuga nyuki hawa wakipewa fedha kidogo tu kwa ajili ya kuwa na mizinga ya kisasa, kwa ajili ya kufuga nyuki kwa namna ya kisasa, nataka nikuhakikishie, inatoa ajira kubwa sana kwa Watanzania na hasa wananchi wa Bukombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Uyovu, ukienda Namonge, kule kote wananchi wa kule wanategemea ufugaji wa nyuki ili waweze kupata mapato yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuomba sana, mazingira haya wezeshi tuyafanye kote. Nchi yetu, amezungumza Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwenye bajeti yake kwamba kazi tuliyonayo sasa hivi ni kutengeneza mazingira wezeshi ya wawekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nasoma kwenye taarifa moja ya urahisi wa kufanya biashara duniani; nchi yetu ni ya 139 kwa urasimu. Ukitaka kufungua biashara Tanzania, unahitaji siku siyo chini ya 19 ili uweze kufungua biashara. Mazingira haya ambayo siyo wezeshi hayawezi kuwavutia wawekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeangalia vilevile kwenye *compliance,* hivi tunawalindaje wawekezaji kama nchi? Nchi yetu ni nchi ya 64. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu tuna kazi kubwa ya kufanya, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha arekebishe haya, tuweze kuwasaidia Watanzania…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Hadji Mponda atafuatiwa na Mheshimiwa Ali Hassan Kingi, Mheshimiwa Omary Mgumba ajiandae.

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu katika mada iliyopo mbele yetu. Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kunipa uwezo wa afya leo kusimama hapa mbele na mimi nitoe mchango katika mada hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wamekupongeza na mimi nitakuwa mchoyo wa fadhila. Pongezi hizo ni kweli unastahili, za haki na za dhati kabisa kwamba nafasi uliyokalia hapa unaiweza. Sisi tuko pamoja nawe, tunakuomba usiyumbe, endelea kurekebisha Bunge hili kama mhimili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu katika bajeti hii nitajikita zaidi kwa mambo yafuatayo na nitaanza na mambo ya mapato. Changamoto kubwa ni kwamba bajeti tunapitisha lakini inafika wakati tunashindwa

kutekeleza bajeti hii kwa sababu ya mapato. Kamati ya Bajeti toka kipindi cha Mwenyekiti Chenge wametoa maelekezo, wametoa ushauri lakini Serikali ni muda sasa bado hawatilii maanani vyanzo vipya vya mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachofanyika Serikali yetu inaendelea na vile vyanzo vya kawaida na matokeo yake yanatupelekea tunapofika nusu ya mwaka wa kifedha tunarudi tena tunakaa chini tunaanza kupitisha bajeti na matokeo yake tunashindwa kutekeleza miradi mingi ambayo tumeiweka kwenye bajeti. Kwa kuwa kipindi hiki tunaweza tukajifunza, basi muanze kutekeleza angalau yale ambayo Kamati wamependekeza, ndani ya miezi sita pengine mnaweza mkaleta matokeo mapya zaidi mkayafanyia kazi katika bajeti ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kingine hapa nimekiona kidogo, natoa angalizo kwamba, wanataka waongeze wigo wa walipa kodi. Angalizo langu wigo huo wanapotaka kuupanua wasije wakagusa hawa wananchi wa kawaidam maana wanasema wanataka wachukue sekta zisizokuwa rasmi, kwa mfano wenye maduka madogo madogo ambao wengi wako vijijini, wenye miradi ya Sh. 70,000 mpaka Sh. 100,000 kama watawaingiza hawa kwamba ndiyo wanaongeza wigo wa walipa kodi, hili ni angalizo, Serikali watakuwa wanawaonea kwa kuwa hawa kwa lugha nyingine ni wajasiriamali ambao wanajitahidi na tunatakiwa Serikali tuwaunge mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii imeleta neema na imeleta matumaini katika kutatua kero za wananchi. Bunge hili toka tunaanza kikao hiki cha bajeti watu wanazungumzia kero mbalimbali kama migogoro ya ardhi, miundombinu, sekta ya afya na sekta ya maji. Nitatoa mfano katika Jimbo la Malinyi, tuna migogoro ya ardhi ambayo inatokana na matumizi ya ardhi ile kati ya watumiaji wake (wafugaji na wakulima).

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro mingine Serikali wenzetu ndiyo wameitengeneza. Kwa mfano, mgogoro ule wa Pori Tengefu la Bonde la Mto Kilombero. Ile hifadhi ya Pori Tengefu la Mto Kilombero ndiyo chanzo kimojawapo cha migogoro kati ya wakulima na wafugaji katika maeneo ya Wilaya ya Ulanga na Wilaya ya Malinyi. Tumewaomba na wamekubali lakini ni muda mrefu sasa bado hawajaanza kutekeleza ombi letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi ombi letu ni rahisi sana kwamba lile Pori Tengefu la Bonde la Kilombero kuna ile *buffer zone,* eneo lile lina *range*, linatoka kutoka kilomita moja mpaka 12, eneo lile ni pana sana. Matokeo yake wamekuja kuingiza mpaka vijiji 18 na vitongoji 22, wananchi wale wanaishi kihalali katika maeneo yale, wanashindwa kujiendeleza na matokeo yake kwa sababu ya uhaba wa ardhi tunaingia kwenye migogoro kati ya wakulima na

wafugaji. Kwa kuwa tayari wameshakubali, naomba basi katika bajeti hii na naiona kweli wametekeleza basi migogoro hii ifikie mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, mvua ya mwaka huu imekuwa nyingi na imeathiri sana miundombinu. Mojawapo ya miundombinu ni barabara zetu ambazo wananchi wengi wanazitumia. Nikitolea mfano ni barabara ya kuanzia Ifakara – Lupilo - Malinyi, Kilosa Mpepo - Namtumbo - Songea. Kwa kuwa barabara hii sehemu kubwa ni vumbi au barabara ya kawaida mvua zimeathiri sana. Naomba bajeti hii kama tutaipitisha, najua barabara sehemu nyingi zimeharibika lakini tunaomba kipaumbele kipelekwe kwenye barabara ambazo zimeathirika sana ikiwepo hiyo ambayo nimeitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, angalizo lingine naiomba Serikali kwamba, hii bajeti tunapoipitisha basi fedha hizi zipelekwe katika muda muafaka. Maana tumeshuhudia bajeti zilizopita kwamba tunapitisha bajeti lakini uwasilishwaji au upelekaji wa fedha umekuwa unasuasua. Kama tutapitisha halafu fedha haziendi kwenye bajeti *impact* yake itakuwa ni ndogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wamegusia suala la bajeti finyu au fedha chache zilizotengwa kwa ajili ya Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali. Waheshimiwa Wabunge, sasa tuko kwenye mchakato wa kupitisha bajeti na kazi yetu nyingine inayofuata ni kuangalia ni namna gani fedha hizi za wananchi ambazo tumepitisha zinatumika na taasisi ambayo itatusaidia sana, jicho letu ni hili moja tu, ni jicho la *CAG*. Kwa bajeti ambayo wameitenga au fedha ambazo zimewekwa hapa ni kidogo sana. Naomba nimkumbushe Mheshimiwa Waziri wa Fedha wakati anaomba bajeti yake ya fedha, kitabu chake kile cha hotuba ukurasa wake ule wa 94, naomba ninukuu, alisema:-

*"Wizara hii ya Fedha itaendelea kuimarisha uwezo wa kitaalam kwa wakaguzi wake, maana yake hawa CAG, na kuendelea na ujenzi wa majengo ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ili kuimarisha uhuru wa wakaguzi kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na tija zaidi ili kukidhi matakwa ya viwango vya kimataifa vya taasisi za ukaguzi pamoja na maazimio ya kimataifa ya Lima na Mexico ambayo Tanzania imeridhia".*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wapi na wapi, walichotenga kinatofautiana na kile walichokisema, hakuna *reflection* na alichosema Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake. Nitoe mfano, bajeti ya mwaka huu ambayo wametengewa shilingi bilioni 32, ukiangalia mwaka wa fedha uliopita walitengewa shilingi bilioni 63, sasa wapi wanakoelekea wakati taasisi hii *CAG* wetu ana ithibati katika uwanja wa kimataifa. Kwa mgao huo maana yake tunamrudisha nyuma. Hiyo fedha niliyosema shilingi bilioni 32 ni matumizi ya kawaida lakini matumizi ya maendeleo ukijumlisha na matumizi ya kawaida

yanafikia shilingi bilioni 44.7 ambapo mwaka jana wa kifedha *CAG* alipewa shilingi bilioni 74.2.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali wametoa maelezo hapa kwamba watakapofikia mwisho wa miezi sita (*mid year review)* mwaaangalia kama *CAG* fedha haitoshi wataweza kumwongezea. Mimi kwa uzoefu mdogo niliokuwa nao Serikali inaongea kwa maandishi. Tunaomba Serikali ili kweli tumpe nguvu *CAG* hapa watakapoishia watoe maandishi kama ni kweli wako *committed,* watakapofanya *mid year review* watajazia hii fedha ambayo imetengwa kwa ajili ya *CAG* ili aweze kukamilisha majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie, wenzangu wamechangia kuhusu kodi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Ali Hassan Kingi atafuatiwa na Mheshimiwa Omary Mgumba na Mheshimiwa Neema Mgaya ajiandae.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na kufika hapa katika Bunge lako hili Tukufu. Pili, nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii, lakini cha tatu nikupongeze sana kwa umahiri wako, ujasiri wako wa kukalia Kiti hicho. Kwa sababu hawa wenzetu wao mpaka sasa hivi kitu kinachowatoa humu ndani ni wewe siyo kwa sababu labda umewafanyia kitu kibaya ni kwa sababu umefuata kanuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mshairi mmoja anasema, mpewa hapokonyeki, aliyepewa akapewa. Wewe ukifanya chuki bure unajisumbua. Mola ndiye atoaye, mambo yote kamiliki. Kwa yule amtakaye ambaye humbariki na yule asiyemtaka basi kupata hatodiriki. Kwa hiyo, hawa wao watasema nje lakini wewe hapo umekaa umetulia kama jina lako lilivyo. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Naibu Spika, cheo ni jaha na jaha anayetoa ni Mungu. Jaha mpaji ni Mungu binadamu hana lake. Sasa wao kwa upande wao wanalia na hii jaha ya cheo na jaha hii ambayo mtu akipewa na Mungu, hata shetani alipopewa Nabii Adam, Mwenyezi Mungu anahadithia kwenye vitabu vya dini, anasema kwamba alivyowaambia malaika wamsujudie Adam, walisujudu isipokuwa ibilisi. Ibilisi yeye alikataa halafu akafanya kiburi. Kwa hiyo,

wanachofanya hawa ni kiburi tu. Ibilisi akafukuzwa mbinguni akaambiwa toka, akatoa ahadi kwa Mungu nitakwenda huko ardhini kuwaposha waja wako. Hawapo huku, sasa wako Kahama, Mwanza, kwa ile ahadi yao kwamba watakwenda kuwapotosha Watanzania. Watanzania tunawaomba wawaelewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kumaliza uchaguzi tuliambiwa kwamba siasa zimehamia Bungeni kama wanavyozungumza watu wengine lakini sasa tazama, majimbo yale ya Wapinzani kule meupe, wote hawapo humu ndani. Hii ni sawasawa na hadithi moja ambayo niliwahi kuhadithiwa na wazee wangu kule, hadithi hiyo inazungumzia habari ya fensi ya ndoa. Katika fensi ya ndoa kuna bibi harusi huyo akipanda mumewe kitandani anatoka, akiingia mumewe chumbani katoka, kwa sababu anaogopa hajajiandaa na harusi, kwa hiyo watu wawaelewe. Kwa hiyo na hii iliyokuwa humu ni fensi ya ndoa, unapoingia watu wanaondoka, kwamba bibi harusi anamwogopa bwana harusi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ni-*conclude* maneno kuhusu hawa, tusiwasemeseme sana kwa sababu kuna mshairi mmoja wa kiarabu anasema, *Al junun funun alwak khalfan waheed*. Wenda wazimu una matawi mengi sana na matawi ya wendawazimu hawa wenzetu wameyadandiadandia tumeyaona. Kwa hiyo, haya yote wanayokuja nayo, wameshakuja nayo mengi na hili moja katika matawi ya wendawazimu ambayo wamedandia. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa wenzetu ndiyo hatuwaoni humu Bungeni lakini sisi tutajadili kwa niaba yao. Sasa nije katika kuchangia bajeti yetu hii. Matumizi ya Serikali siku zote huwa yanapangwa kwa fedha. Fedha zinazopangwa badala yake huwa tunatazama yale mambo yaliyotarajiwa kwenda kufanyika lakini mambo yanayotarajiwa kwenda kufanyika tunatarajia yatokezee kwa 100%. Inawezekana fedha zikatumwa 100% lakini kazi isifanyike kwa 100% kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa *gap* hii tutaijua au itazibwa kutokana na ukaguzi unaofanywa na Mkaguzi Mkuu wa Serikali. Kwa hiyo, kuna kila umuhimu wa kuwa na taasisi hii ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali. Madhara yake kama itakuwa ukaguzi haukutosheleza ina maana kwamba mwaka unaofuata wa fedha tunaweza tukapeleka fedha tena katika miradi ileile na fedha ile isiweze kufanya kazi vizuri kwa sababu haiangaliwi, kwa hiyo, hili ni jambo muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zilizotengwa katika ofisi hii ni ndogo na nasema ndogo kwa sababu gani? Fedha zilizotengwa mwaka jana katika hizo *OC*, sizungumzii mishahara na *development*, nazungumzia *OC* za kufanyia kazi zilikuwa ni shilingi milioni 49 lakini mpaka kufikia Machi, 2016 fedha zilizotoka ni

shilingi milioni 39, lakini fedha zilizotengwa kwa ajili ya mwaka huu wa fedha ambao tunaujadili hapa ni shilingi milioni 18.5 ya *Other Charges*. Shilingi milioni 44 humo kuna *development* na *P.E.* Kwa hiyo, hizi fedha tuna-*justify* kwamba ni kidogo kwa sababu ni asilimia 37 ya fedha zilizotoka mpaka Machi. Kwa hiyo, ukija kutazama kwamba zinatarajia kufanya kazi kwa mwaka mzima tutakuja kuona upungufu wa fedha hizi ni kiasi gani. Najua Serikali itakuja na *mid year review* lakini katika *mid year review* hili nalo tulione kama ahadi ya Serikali ilivyosema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna kitu kimoja ambacho ni kizuri. *Audit* inapofanyika ina *stage* nyingi, kuna *stage* ya *planning.* Katika *stage* hii ya *planning auditor* anapanga wapi atafanya *audit* ile, anapanga *resources*, anapanga *expert's* watakaohitajika wa-*audit* eneo fulani lakini pia anapanga na *time consuming* ambayo atatumia. Sasa katika hatua hizi za mwanzo *auditor* anahitaji kufanya hayo mambo kama *resources* zitakuwa hazitoshi ina maana kwamba ingekuwa ana-*audit private office* siyo Ofisi ya Serikali asinge-*accept* hii *engagement* kwa sababu *resources* zisingemtosheleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kingine muhimu katika kufanya *audit, auditor* wetu ana heshima kubwa sana Kimataifa. Katika kulinda *reputation* yake Kimataifa ni lazima *auditor* wetu afanye kazi vizuri na apelekewe fedha za kutosha ili aweze kufanya kazi kwa umakini na umahiri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia bajeti ya maendeleo ni kubwa, imeongezeka kwa asilimia 100. Kwa hiyo, tunatarajia fedha za maendeleo zikakaguliwe kwani zimeongezeka kwa asilimia 100. Kitu kingine Halmashauri zetu zimeongezeka kutoka 100 na zaidi hadi kufika 181. Ina maana kwamba kuongezeka kwa Halmashauri ni *indication* kwamba hata fedha za *audit* zingeweza kuongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, isitoshe, tumesema kwamba Serikali imeamua kulipa madeni, lakini kabla ya kulipa madeni hayo inayakagua ili kupitisha kwamba deni gani linafaa kulipwa. Kwa hiyo, madeni haya ya Serikali yanayokaguliwa pia nayo yataongeza kazi ya *auditor* kwa hiyo ilipaswa fedha za *auditing* ziwe nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Serikali imeamua kufuta *retention,* makampuni ambayo yatafutiwa *retention* yatakuwa hayako radhi, hayataweza ku-*submit* kila kitu kikawa kiko safi. Kwa hiyo, Serikali ilipaswa iangalie suala hili ili *Auditor General* aweze kufanya mambo hayo ya ukaguzi. Pia taasisi kama Mahakama ya Kuzuia Ufisadi, TAKUKURU, Bunge tunategemea taarifa za CAG ili tuweze kufanya kazi. Kwa hiyo, hivi vyombo vinaweza vikakosa taarifa ya thamani katika kufanya kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine nije katika deni la Taifa. Wengi wamezungumzia deni la Taifa lakini deni la Taifa ni himilivu tunakubali lakini tunasema hivi, tukope tufanye zile kazi tulizoziainisha na tumalize kazi zile tulizokopea. Kama hatukumaliza, *project* zikiganda katikati *interest rate* inalipwa ina maana kwamba tunalipa fedha zetu au tumelipa fedha zimeganda, wananchi wanalipa *interest* na miradi inakuwa haijakamilika. Kwa hiyo, naomba suala hili tuweze kuliangalia vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini eneo lingine ambalo naweza kuchangia ni eneo la Bodi ya Taifa ya Ukaguzi ambayo ilitajwa katika Mpango. Bodi hii ya Taifa ya Ukaguzi tukifuata nchi za wenzetu huwa wanazitumia Bodi zao za Wahasibu na *Auditors* ili kuweza kutoa hata mitaala ya sheria za kodi ambazo zimetoka.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Omary Mgumba atafuatiwa na Mheshimiwa Neema Mgaya, Mheshimiwa Yahaya Massare ajiandae.

Mheshimiwa Omary Mgumba nimepata ujumbe kutoka kwa Mheshimiwa Leah Komanya kwamba anakupa dakika zake tano. Nataka tu kujiridhisha kama Mheshimiwa Leah Komanya hajachangia hoja hii ya Waziri wa Fedha na Mipango.

**MBUNGE FULANI:** Hajachangia.

**NAIBU SPIKA:** Hajachangia bado?

**MBUNGE FULANI:** Bado.

**NAIBU SPIKA:** Endelea Mheshimiwa Omary Mgumba kwa dakika 15.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kutoa mchango wangu katika mada yetu hii iliyokuwa mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukuke fursa hii kuipongeza Serikali kupitia Wizara ya Fedha na wataalam wao kwa kuleta bajeti nzuri kwa sababu ni bajeti ya kwanza ya Serikali ya Awamu ya Tano. Bajeti hii ndiyo inatoa mwelekeo wa Serikali ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli na imeonesha

anapita kutokana na maneno yake aliyokuwa anaahidi wakati wa kampeni. Aliahidi viwanda na kweli bajeti inatafsiri hivyo, inaanza kujiandaa kwa ajili ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia niseme hii bajeti kubwa imejielekeza hasa kwenye miundombinu na elimu, miundombinu ni asilimia 25 na elimu asilimia 22, jumla 47. Hivi ni vitu muhimu sana katika maendeleo ya viwanda kwa sababu vikwazo vikubwa kwa wawekezaji wengi ilikuwa ni miundombinu sasa bajeti inaenda kutibu hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, naomba kwanza nipate…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mgumba samahani kidogo, tumeangalia hapa taarifa zetu zinaonesha Mheshimiwa Leah Komanya alishachangia dakika zake 10. Kwa hiyo, Mbunge mwingine ambaye hajachangia na ameomba kuchangia hoja hii labda ajitokeze ili ampe dakika zake 5 Mheshimiwa Mgumba lakini kwa sasa utawekewa dakika 10, endelea.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nichukue fursa hii nipate tu ufafanuzi kutoka kwa Waziri wakati akija kuleta majumuisho yake hasa kutokana na hotuba yake kwenye ukurasa wa 57 hasa kwenye ushuru wa mafuta ya kulainisha mitambo kutoka Sh. 665 hadi Sh. 699 kwa lita. Kwa sababu kwa ufahamu wangu ushuru wa sasa hivi ni senti 50 kwa lita na kama ushuru ndiyo huu ulioandikwa hapa Sh. 665, ni ushuru mkubwa sana. Kwa hiyo, namwomba tu alete ufafanuzi wakati anakuja kufanya majumuisho yake ipi ni sahihi, hii iliyoandikwa kwenye kitabu au ni hii inayotumika sasa hivi huko *field* 0.5 *cent* kwa lita moja ya mafuta ya kulainishia mitambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, naomba ufafanuzi pia kwenye takwimu, nimesoma kwenye kitabu hiki cha Hali ya Uchumi cha mwaka jana hasa kwenye ukurasa wa 149, uzalishaji wa mazao ya mafuta. Nimeona kwenye ufuta, alizeti, kwa mfano alizeti Tanzania tunazalisha tani milioni 2,878,500, karanga tani 1,835,933, ufuta tani 1,174,589. Nichukulie kwenye ufuta tu, hata nchi zinazoongoza ulimwenguni kama ni Myanmar kule na China hawajafikia kiasi hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe tu Mheshimiwa Waziri na timu yake wakae vizuri waangalie hasa hii Idara ya Takwimu au hizi mlikozipata kwa sababu hizi *data* ziko kwenye mitandao na zinaenda, zinaweza zikapotosha wawekezaji wakaja hapa halafu malighafi hakuna au tunaweza kupanga mipango yetu kwa kuamini kwamba malighafi ipo kumbe hamna. Tunazo *data*

za kutoka *Custom* kwenye Ofisi yake, mwaka jana usafirishaji wa ufuta kwenda nje ya nchi ni tani 133,000 kutoka mwezi Juni mpaka mwezi Desemba. Naomba tu wazipitie vizuri wakalete *data* halisi ambazo zinaweza zikawa kichocheo kwenye uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda ufafanuzi wa mwisho, kama nilivyosema mwanzoni hii bajeti ni ya miundombinu. Kwa bahati mbaya sana sijaona kwenye bajeti hii miundombinu ya kwetu kule, barabara hasa ile ya Bigwa - Kisaki kwa kiwango cha lami. Mradi ule ulikuwa ugharamiwe na *MCC* na hao *MCC* sasa hivi wamejiweka pembeni. Kwa ajili ya mradi ule na miradi mingine Tanzania iliyokuwa inagharamiwa na *MCC* sijui sasa Serikali imejipangaje kwa ajili ya kutekeleza pengo hili lililoachwa na hawa jamaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kwa sasa nijielekeze kwenye mchango wangu. La kwanza ni kuhusu Mfuko wa Maji. Wabunge wengi wamezungumzia suala hili kwa sababu maji ni uhai. Nami lazima nijikite hapa kwa sababu tuna tatizo kubwa sana la maji katika Jimbo langu la Morogoro Kusini hasa katika vijiji kama vya Mkuyuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa maji uko miaka 15 haujawahi kufanyiwa ukarabati na vijiji vile ambavyo vilikuwa vitongoji sasa hivi vimekuwa vijiji kama vijiji vya Kivuma, Kibuka na Mwalazi wanategemea maji ya mradi huo huo ambao uliwekwa tanki la 10,000. Tukiomba tunaambiwa kwamba vijiji vingine havijapata maji wakisema ni lazima wamalize vijiji vingine ndiyo waje kwenye ukarabati wakati sasa vile vitongoji vimeshakuwa kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kibuka kilikuwa Kitongoji cha Mkuyuni sasa hivi ni kata inategemea mradi wa kijiji hicho hicho. Kwa hiyo, nimwombe Waziri akubaliane na mawazo mengi ya Wabunge kuongeza hii Sh. 50 katika lita ya *petrol* na *diesel* ili twende kutatua tatizo la maji vijijini. Sauti ya wengi ni sauti ya Mungu, Wabunge wote wana kilio cha maji na Sh. 50 kuongezwa. Wabunge kazi yetu ni kuishauri Serikali namwomba Waziri apokee ushauri huu ili tukatatue tatizo la maji na vituo vya afya na zahanati kwa sababu mzigo huu wananchi walishabeba muda mrefu sana kwa kuchangia zahanati na vituo vya afya huko vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nataka kuchangia ni kupunguza tatizo la msongamano Dar es Salaam ili kufungua fursa za uchumi na kuharakisha maendeleo ya uchumi. Tatizo la msongamano Dar es Salaam linaathiri sana uchumi wa Taifa letu kwa sababu watu wanatumia muda mrefu kufika kazini na wanatumia muda mchache kufanya kazi. Tatizo hili nilishawahi kusema siku moja, ni lazima tufungue vituo vikubwa vya kibiashara na bandari kavu nje ya Dar es Salaam na ukisema nje ya Dar es Salaam basi Morogoro ina sifa mojawapo ambayo baadhi ya mikoa mingine haina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Morogoro ni mkoa ambao umepitiwa na reli zote mbili, reli ya kati na reli ya TAZARA. Tunaweza kutumia reli hizi ili kuingiza na kutoa mizigo bandarini kwa kutumia treni badala ya magari yote kutoka mikoani na nchi zingine zikapakia mizigo pale Morogoro. Pamoja na juhudi kubwa za Serikali kutatua changamoto ya foleni Dar es Salaam lakini kwa kuanzisha bandari kavu Morogoro tutakuwa tumepata suluhu ya kudumu kumaliza changamoto hii lakini pia tumeinua hali za uchumi wa sehemu hizo zingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka kuchangia katika sekta hii ni suala la kilimo. Kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa letu na wengi wamechangia umuhimu wa kilimo, unaajiri asilimia 70 ya watu wetu, pato la Taifa asilimia 25, hela za kigeni zaidi ya asilimia 30 inatoka kwenye kilimo, chakula asilimia 100, malighafi asilimia 65 lakini bajeti hii imejikita zaidi kwenye miundombinu badala ya kutatua uchumi wa watu wengi walikojiajiri kwenye kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwamba niliona kwenye Mpango kwa ajili ya kuendeleza sekta ya kilimo katika suala la Mkulazi, lakini sikuona kwenye Mpango wa 2016/2017, nilijua sasa kilimo ndiyo kitapewa kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kushauri katika hili…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Omary muda wako umekwisha.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Neema Mgaya utakumbuka ulitoa dakika zako 5 kwa Mheshimiwa Hussein Bashe, dakika 5 zilizokuwa zimebaki alipewa Mheshimiwa Turky. Kwa hiyo, wewe una dakika 10 za Mheshimiwa Turky kwa sababu Mheshimiwa Turky alishachangia.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. Vilevile namshukuru Mungu kwa kuweza kunipa afya bora na kuweza kusimama mbele ya Bunge hili Tukufu kuchangia hotuba hii ya bajeti kuu ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuzungumzia suala la afya, nasikitika kusema kwamba sijaona mkakati mahsusi wa kujenga zahanati pamoja na vituo vya afya. Tuko katika mkakati wa kuhakikisha kwamba tunapunguza vifo

vya akinamama wajawazito. Najiuliza tunawezaje kupambana na vita hii ilhali hatuna *facilities* za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nasema hivi? Katika bajeti hii nimeona Hospitali za Mikoa ndiyo ziko chini ya Wizara lakini kiuhalisia watu wengi wapo kwenye Kata na kwenye Halmashauri zetu. Watu waliokuwa kwenye Kata, kwenye vijiji vyetu macho yao yanakuwa yanatazama zahanati zao na vituo vyao vya afya ambavyo viko kwenye Kata na kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua Kanuni ya 106 inasema kwamba Mbunge hataruhusiwa kupendekeza mabadiliko yoyote katika makadirio na mapato ya bajeti ya Serikali, lakini naiomba Serikali kwa bajeti inayokuja iweze kuliangalia vizuri suala la zahanati na vituo vya afya viwekwe katika Serikali Kuu ili tuweze kuviboresha na kuvijenga kwa ufanisi mkubwa ili kuweza kutatua tatizo lile la vifo vya akinamama wajawazito ambapo wengi wao wako kwenye Kata huko kwenye Halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niishauri Serikali, ni vyema kuweka pesa nyingi katika Mfuko wa Maji kwa sababu tatizo la maji ni kubwa sana Tanzania na anayeteseka katika matatizo ya maji ni sisi wanawake. Akinamama wa mkoani kwangu kule, akinamama wa Kata za Saja, Kijombe, Wanging'ombe, Mkongobaki, Nkomang'ombe, Ludewa Mjini, Ludewa Vijijini pamoja na Njombe Mjini kuna shida sana ya maji kwa muda wa miaka mingi. Ni vyema Serikali itambue umuhimu mkubwa wa kuweka pesa nyingi katika Mfuko wa Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, naomba nizungumzie suala la utalii. Wenzetu wa Kenya wametoa kodi katika suala la utalii lakini sisi Watanzania tumeamua kuweka kodi katika suala la utalii. Kiuhalisia sisi Tanzania mshindani wetu mkubwa katika suala la utalii ni Mkenya. Wenzetu Wakenya wana ndege ya moja kwa moja kutoka Europe na America kwenda Kenya na mtalii anapotumia ndege hiyo anapata ahueni ya pesa katika tiketi karibu asilimia 45 ya *air ticket*. Hiyo ni *advantage* kwa wenzetu wa Kenya kwa sababu watalii wengi watakuwa wanataka kwenda Kenya kwa ajili ya ku-*save* hizo *costs* za *air ticket* na mambo mengine. Kabla hatujaweka asilimia 18 bado utalii wetu wa Tanzania ulikuwa wa gharama kubwa ukilinganisha na wa Kenya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile mtalii kabla hajaamua kuja *vocation* huwa analipa *in advance,* mwaka mmoja kabla au miaka miwili kabla. Kwa kuweka kodi hii kutatokea usumbufu kwa wale watalii ambao tayari walishalipa hela zao kuja kutalii kwa mwaka huu wa fedha 2015/2016 na ikiwezekana 2017. Kwa mkanganyiko huo, kuna uwezekano mkubwa wa watalii wengi kuahirisha na kutaka pesa zao warudishiwe kwa sababu wanaona kwamba mimi

nilishajipanga bajeti yangu ya *vocation* ni kiasi hiki na sasa hivi naambiwa kwamba niongeze asilimia 18 ya pesa ambayo ilikuwa haiko kwenye bajeti yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara iangalie suala hili la utalii katika masuala mazima ya ushindani wa utalii baina yetu sisi na watu wa Kenya, huenda tukasababisha watalii wengi waache kuja Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna ile wanaita msafara wa nyumbu wanaokuwa wanazunguka Kenya na Tanzania, *migration* ya wanyama. Nina wasiwasi wanaweza watalii hawa wakawa wanasubiri wanyama wakifika Kenya ndio waende badala ya kuja kuangalia kwetu Tanzania wakati sisi tuna *advantage* kubwa wakati wanyama wanasafiri miezi ya saba ndiyo kipindi ambacho nchi nyingi za Ulaya wanakuwa wako kwenye *holiday* na wanatumia muda huo kuja kutalii Tanzania. Naomba Serikali iangalie ili tusiweze kupoteza mapato katika suala la utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika bajeti zilizopita imeonesha kabisa kwamba utalii unachangia asilimia 25 ya mapato ya Tanzania. Kwa nini leo tuisumbue sekta hii na twende katika kushusha mapato hayo? Naomba Serikali iangalie kwa umakini kwa sababu asilimia 25 ya kuchangia kwenye mapato ni asilimia kubwa sana, tuiangalie kwa umuhimu wa kipekee ikiwezekana hii kodi tuitoe ili tusiweze kukosa watalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nizungumzie suala la kiinua mgongo. Najua Serikali ina dhamira njema ya kuongeza mapato katika bajeti yetu, lakini nashangaa katika *category* ya watu tisa akiwemo Makamu wa Rais, *Prime Minister, Chief Justice, High Court Judges,* Maspika, *Supreme Court Judges*, *Regional Commissioners* na hawa Wakuu wa Wilaya, kwa nini wame-*single out* Mbunge tu ndiyo akatwe kodi ya kiinua mgongo ilhali katika hilo *group* hao watu wote nao wanatakiwa waingizwe kwenye kukatwa makato haya. Kama kweli Serikali ina nia ya dhati na hawa watu wengine wote wakatwe au labda kama kuna kitu kimejificha tunaomba Wabunge tukijue hicho kitu ni kitu gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge tuna mzigo mkubwa, Wabunge tunahudumia watu wengi huko vijijini kwa hela hiyo hiyo, Wabunge tunapeleka watu hospitalini, tunahudumia misiba, harusi, wagonjwa, kwa kipindi hiki cha Ramadhani Wabunge ndiyo hao hao ambao wanasaidia kule watu wengine ambao hawajiwezi katika masuala mazima ya kuhakikisha kwamba wanafuturu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iwaangalie Wabunge kwa jicho la huruma na hatuna nia mbaya kwamba hatutaki kuchangia mapato kwa sababu katika mishahara yetu tunakatwa kodi. Naomba sasa watuangalie na sisi ili tujue ni jinsi gani ya kurudi humu ndani na tuendelee kuwahudumia wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Neema Mgaya mpaka Katiba Inayopendekezwa itakapopigiwa kura kwa sasa hatuna ma-*Judge* wa *Supreme Court*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Yahaya Omary Massare atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Jasmine Tisekwa, Mheshimiwa Dkt. Diodorus Kamala ajiandae.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nami nichangie katika mjadala huu wa bajeti ya Serikali. Nikupongeze sana wewe, kama walivyokupongeza wajumbe wenzangu wa Baraza hili la Kutunga Sheria kwa maana ya Bunge, kwa ujasiri wako na weledi mkubwa wa kuliongoza Bunge hili Tukufu kwa kufuata Kanuni ambazo Bunge hili limejitungia ili kujiendesha. Kwa mwanamke kijana kama wewe umeonesha umahiri mkubwa na ni mfano mzuri wa kuigwa kwa viongozi waandamizi wa nchi hii, nakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Waziri wa Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Mpango kuanzia kuteuliwa kwake na Mheshimiwa Rais kuwa Mbunge lakini kuwa Waziri wa Wizara nyeti, Wizara ambayo ndiyo mhimili wa Serikali. Pia nimpongeze mdogo wangu Mheshimiwa Dokta Kijaji naye kwa kupata fursa hii adhimu ya kulitumikia Taifa hili kwa nafasi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze pia Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa utendaji mzuri. Mheshimiwa Rais amekuwa akifanya kazi nzuri sana pamoja na changamoto za hapa na pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nianze kwa kuchangia kuhusu Wizara yenyewe ya fedha, lakini bajeti nzima ya Serikali. Waziri amekuja na mpango mzuri sana hapa, suala la kutokupandisha bei katika tozo za mafuta, niipongeze sana Serikali kwa kuliona hili kwa sababu *impact* yake huwa ni kubwa na inapelekea mfumuko mkubwa wa bei. Kwa kufanya hivi, maana yake sasa tutabaki katika mpango ule ule, kwa hiyo tutakuwa na changamoto chache.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka tu nikumbushe Waziri au Serikali iangalie sana maduhuli ambayo yanakusanywa na Serikali hii kupitia maeneo mbalimbali (mapato yasiyokuwa ya kodi). Kuna eneo ambalo tukiliangalia kwa

makini sana linaweza likachangia sana, eneo la misitu ya asili lakini eneo hili la misitu ya kupandwa na Serikali. Kuna mashamba makubwa ya Serikali, utaratibu mzuri ukitumika na kuhakikisha wazawa wananufaika na mashamba yale, basi yana mchango mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka mitano iliyopita miongoni mwa maeneo ambayo yalichangia katika Wizara ya Maliasili ni pamoja na sekta hii ya misitu. Mashamba ya Lunguza, Mashamba ya Mtibwa lakini misitu ya asili kama itavunwa kwa utaratibu mzuri bila uharibifu wa mazingira, Serikali ina chanzo kizuri sana cha mapato. Niiombe sasa Serikali napo hapo ipaangalie kwa macho mawili, ipatendee haki ili Serikali inufaike na rasilimali zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika huduma za jamii Serikali imekuwa ikifanya vyema sana. Katika afya kuna mpango wa kujenga zahanati kila kijiji, lakini kuna kujenga kituo cha afya kwa kila kata, mpango huu umekuwepo kinadharia sana. Wakati umefika na wakati muafaka, kwa sababu ahadi yetu sisi Wabunge, Mheshimiwa Rais wetu wa Chama cha Mapinduzi tulikuwa tukimuunga mkono kwa kuwaambia wananchi kwamba sasa Serikali inayokuja itakuwa na mpango wa kujenga zahanati kila kijiji lakini kila kata kitajengewa kituo cha afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji tuone hapa na Serikali ije itueleze sisi Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano kwamba inajipangaje kuhusu kutekeleza ahadi hizi ambazo humu katika makabrasha ya bajeti haionekani vizuri, sijui wana mpango gani. Tusije tukaenda kwa mpango ule tulikuwa na dhamira ya kujenga maabara kila shule ya sekondari matokeo yake zile nguvu zikasukumwa kwa wananchi moja kwa moja. Ni jambo la hatari na mpaka leo kuna baadhi ya maabara hazijakwisha kwa sababu kulikuwa hakuna mafungu isipokuwa mkoa mmoja tu wa Dar es Salaam ambapo Serikali ilitenga bajeti na ika-*facilitate* ule mpango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye elimu, tumeliona hili la elimu bure. Niipongeze Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa utekelezaji wa jambo hili ambalo maswali kwetu sisi kama wawakilishi wa wananchi yamepungua sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna changamoto kubwa sana katika suala hili la huduma za jamii ikiwemo maji. Wabunge wengi wamezungumzia maji ni tatizo katika maeneo yao lakini na mimi niseme wazi kwamba miongoni mwa majimbo ambayo maji ni tatizo Jimbo langu la Manyoni Magharibi maji ni tatizo kubwa. Ile mita 400 kule kwetu hata ukifanya mkutano ukiwaambia mita 400 watakushangaa sana labda useme angalau tupunguze kutoka kilomita saba, nane zilizopo sasa kufuata maji mpaka angalau kilomita mbili, sasa tunafanyaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri sasa Serikali ikajipanga isaidie Wabunge ambao majimbo yao ni magumu, tuongeze mafungu pale ili maji yaweze kupatikana na tutakapofika katika chaguzi zingine tuweze kuwa na kauli nzuri na kuhakikisha chama hiki ambacho ndiyo chenye Serikali kinarudi na Wabunge wengi zaidi kuliko tuliopo sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa mikoa maskini ni Mkoa wetu wa Singida. Mkoa wa Singida na mikoa ya katikati kwa ujumla, Mkoa wa Dodoma na mikoa mingine ambayo tunapakana nayo watu wake ni hodari sana katika kilimo lakini tumekuwa na changamoto ya kilimo hiki cha kutegemea mvua. Niiombe sasa Serikali ifike mahali tuwe na mpango madhubuti, tutoke katika kilimo hiki cha kutegemea mvua ili tuweze kutengeneza miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, *water table* ya maji ipo karibu tukiyachimba na kuyapandisha yale maji kwa miundombinu safi na kuanzisha kilimo cha umwagiliaji, haya majanga yanayotukabili watu wa mikoa ya katikati likiwemo baa la njaa yataondoka kabisa. Niiombe sasa Serikali ije na mpango wa kuondokana na kilimo hiki cha mvua tuweze kutegemea kilimo cha umwagiliaji ambacho kitakuwa na tija kwa nchi yetu na jamii yetu kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Serikali yangu pia kwa kuondoa mageti haya ambayo yalikuwa yana shida kwa wakulima wetu. Pia nizungumzie hili pia la ujenzi wa reli ya kati pamoja na matawi yake. Jambo hili ni jema na likienda na mpango huu kwa hakika uchumi utaendelea kwa sababu miundombinu ikiwa mizuri basi uchumi unakuwa ni rahisi na unakuwa mwepesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wamezungumzia sana kuunganisha *RAHCO* na *TRL*, *RAHCO* ni mmiliki wa miundombinu, *TRL* aendeshe reli. Ikiwa mwendesha reli akamiliki miundombinu ni hatari sana. Tuendelee kubaki na utaratibu tulionao leo, *RAHCO* aendelee kumiliki miundombinu kwa niaba ya Serikali, lakini *TRL* libaki kama shirika linaloendesha miundombinu ambayo ni mali ya Serikali. Ni jambo la hatari kama tutafika mahali tutabinafsisha Shirika la Reli na miundombinu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Jasmine Tisekwa atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Diodorius Kamala, Mheshimiwa Mussa Ramadhan Sima ajiandae.

**MHE. DKT. JASMINE T. BUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi katika Bunge lako hili Tukufu. Kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kusimama na kuongea, nilikuwa naendelea ku-*observe* majadiliano yanavyokwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu na kumpongeza sana Mheshimiwa wetu Rais kwa jinsi anavyopambana katika kuondoa umaskini, kupambana na rushwa, mafisadi na kadhalika ili kuona kwamba sasa nchi yetu itafikia mahali ambapo ile keki itagawanywa mpaka kule kwa wanyonge. Pia nichukue nafasi hii kumpongeza mama yetu Mheshimiwa Samia kuwa mwanamke wa kwanza kuongoza Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kazi tunaiona, nawapongeza Mawaziri wote kazi zetu tunaziona na mnatosha lakini pia kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa kurudi mjengoni na wengine mara yetu ya kwanza kama hivi. Niwapongeze wapiga kura wangu wa Mkoa wa Morogoro pamoja na wanawake UWT Taifa kwa kuniamini kuweza kuwawakilisha bila kusahau *support* ninayoipata kutoka kwa familia yangu ikiongozwa na mume wangu mpendwa Profesa Tisekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, napenda sasa niweze kuchangia hii bajeti. Nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na timu yake yote akiwemo Mheshimiwa mdogo wangu Dkt. Ashatu Kijaji, nafahamu uwajibikaji wake na weledi wake, kwa hiyo nawapongeza sana. Bajeti hii inaleta matumaini hasa kwa kutenga asilimia 40 kupeleka kwenye masuala ya miradi ya maendeleo, hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na wajumbe wote ambao wamejadili suala hili hasa kwa kuwapongeza jinsi walivyopanga mikakati ya kuweza kukusanya kodi na kuongeza wigo wa kodi, nawapongeza sana. Pia nashauri sasa tuangalie zile kero ambazo zinaambatana na kodi na tozo za aina fulani ambazo wananchi bado wanazilalamikia kama Serikali muweze kuangalia kwa undani na kwa macho mawili ili kuondoa misuguano ambayo inaweza ikatokea kati ya Serikali na wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichangie kwa kusema kwamba sasa hivi Watanzania sera yetu ya maendeleo tunaelekea kwenye uchumi wa viwanda baadaye kufikia uchumi wa kati. Viwanda peke yake bila ya kuwa-*empower* wananchi wake hasa wananchi waishio vijijini haviwezi vikawa endelevu. Kwa nini nasema hivyo? Ni lazima tuweze ku-*empower* maendeleo vijijini na kwa wananchi wa vijijini kwa sababu asilimia 75 ya wananchi wako vijijini, rasilimali nyingi za Taifa zipo kijijini, nguvu kazi ipo vijijini lakini umaskini uliokithiri upo vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kuna sababu zote za msingi kuhakikisha miradi hii ya maendeleo ambayo imeelekezwa vijijini zile fedha ambazo zimepangwa basi fedha hizi zote zipelekwe ili kuendeleza vijiji vyetu. Tukifanya hivyo tunaweza sasa kuwa-*empower* hawa wananchi wetu na kuweza kuwa na *purchasing power* kwa sababu ukiwa na kiwanda *parameter* mojawapo lazima ku-*create* soko la ndani na la nje. Kama watu wako ni maskini ina maana hivi viwanda *sustainability* yake kidogo inaweza ikawa kwenye *question mark*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuangalie suala la usawa wa kijinsia. Miradi ambayo imeelekezwa kule vijijini au mijini ile yote ambayo imelenga kupunguza matatizo ya wanawake (*reproduction roles* zao) mfano maji, afya, elimu na kadhalika ipewe fedha kama ilivyokuwa imepangwa. Kama tunavyoona 51% ya *population* ya Tanzania ni wanawake, ukiwaacha watumie saa tabi au sita kwenda kuchota maji, kuhangaika kwenda kwenye kituo cha afya hawataweza kushiriki katika uzalishaji. Kwa hiyo, huyu mwanamke ili aweze kuwa *productive* kwa sababu wako wengi na waweze kujikwamua kiuchumi tufikie ile *fifty fifty* mwaka 2030, lazima hawa wanawake wapunguziwe ile mizigo ya *reproduction roles. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda nizungumzie suala la shilingi milioni 50. Hii shilingi milioni ya kila mtaa naona kwamba imeelekezwa sana kwa wajasiriamali na *SACCOS*. Mimi naona hii *approach* tunayoitumia siyo sahihi sana kwa sababu tunasahau hili kundi la maskini wa kipato cha chini watakuwa hawana msaada.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini Sh. 5,000 inaweza ika-*transform* maisha ya huyu maskini ambaye hana kitu. Kwa sababu kule kijijini huyu mtu maskini wa kipato cha chini ambao wanaishi *under poverty line* kwa mfano anaweza akawa na nguvu, yupo *physically fit*, ana ardhi lakini hana jembe, hana mbegu. Kwa hiyo, huyu mtu ukamkopesha Sh. 5,000 akanunua mbegu, akanunua jembe *that means next season* tayari umeshamwezesha lakini sasa tukijikita kwenye wajasiriamali tukawasahau hawa, hatutafika mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine nasema sasa ili kupunguza milolongo ya kodi na tozo kwa wananchi wetu tutumie rasilimali zetu kwa mfano utalii, madini na kadhalika. Sisi kule Morogoro (Kisaki) tuna *hot spring* eneo kubwa, *kilometers and kilometers* lakini halitumiwi. Kwa mfano, ukienda Swaziland walikuwa na ka-*spot* kamoja ka *hot spring* wamejenga pale hoteli, *swimming pool,* hela zinatengenezwa. Sisi kwetu ukienda kwenye zile *hot spring* unakuta vibanda vya waganga wa kienyeji vimejazana pale. Kwa hiyo, tutumie rasilimali zetu ili tuweze kupunguza hizi tozo ambazo mara nyingi ni kero kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Kitengo cha *Monitoring and Evaluation* lazima kipewe kipaumbele kwa sababu *on desk work* mtu anakuja anatengeneza mikakati bila *research,* tathmini, hatutafika mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nizungumzie upande wa *environment*. Sikubaliani na kusema mifuko ya *plastic* sijui *microns* 50 sijui nini, nashauri ipigwe marufuku, inailetea hasara Taifa letu. Mafuriko haya mengi ukiangalia ni kwa sababu ya mifuko ya *plastic*. Huyu mzalishaji mwenye kiwanda anapata *super profit* lakini Serikali inapata *super loss* kwa sababu kila mwaka lazima itengeneze miundombinu ya barabara, umeme na kadhalika. Kwa hiyo, mimi naona hapana, ikatazwe kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mwisho napenda nimalizie kwa kusema kwamba, mimi nashangaa sana, Waheshimiwa Wabunge, wachumi, wasomi na kadhalika kazi yao kusimama kwenye *media* na kubeza Serikali. Hii bajeti tunayoipitisha ni ya Serikali lakini kila Mtanzania lazima awe na bajeti yake ku-*top up* kwenye bajeti ya Serikali. Mimi nashangaa kwa mfano ukienda Bangladesh, Profesa Yunus alichukua dola zake 27 kwa kila mwanamke wale waliokuwa wanatengeneza *furniture* mpaka ikazaa *Grameen Bank* ambayo na yenyewe ikazaa na vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii Profesa mzima aliyebobea anaenda eti kwenye *media* kuanza kulaumu Serikali, wewe Mbunge unasimama unalaumu Serikali eti mpaka nipewe nafasi ya kwenda Ikulu, wewe *role* yako ni nini kama Mbunge, kwa sababu wewe ni kiongozi! Wewe *role* yako ni nini kama Profesa kwa sababu wewe ni kiongozi, wewe *role* yako ni nini kama mwananchi wa kawaida kwa sababu sasa hivi mpaka Mheshimiwa Rais aende akawafanyie watu usafi kwenye kaya zao, inakuja hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nasema bajeti ya Serikali lazima iwe *supported* na sisi wananchi kwa umoja wetu. Watu hapa ni mabilionea badala ya kuweka hela benki chukueni hizo pesa wagawieni kama alivyofanya huyu Profesa Yunus wa Bangladesh kwa riba nafuu. Kwa sababu bajeti ya Serikali hata siku moja haiwezi kutosheleza kuleta maendeleo ya nchi yetu, ni sisi. Vita dhidi ya umaskini ni vita na kila mwananchi lazima awe askari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nasema, naomba bajeti hii fedha zipatikane ili kuweza kuleta maendeleo. Naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Diodorus Kamala atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Ramadhan Sima, Mheshimiwa Felister Bura kama muda utatosha atafuatia.

**MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba nianze kwa kukupongeza kwa kazi nzuri unayofanya. Pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jinsi walivyowasilisha vema bajeti ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kitabu cha Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2016/2017 ukurasa wa tisa mpaka wa kumi inabainisha kwamba kuna mikoa mitano ambayo inaongoza kwa umaskini. Nimesikia wenzangu walivyosema, sina sababu ya kukataa jinsi hiyo mikoa ilivyobainishwa kwa sababu nitaingia kwenye ubishi wa kiuchumi na wachumi siku zote huwa hawana jibu moja, kwa hiyo kwa sasa hilo naliacha. Nakubaliana na jinsi Mheshimiwa Waziri alivyowasilisha mikoa mitano lakini hoja yangu ni kwamba baada ya kuwa nimeiona hiyo mikoa mitano nikisoma kitabu cha bajeti sioni sasa kwa nini Mheshimiwa Waziri aliwasilisha hiyo mikoa mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilifikiri baada ya kuibainisha basi bajeti hii ingekuja na mikakati maalum ya kusaidia hiyo mikoa mitano. Kwa kuwa sijaona, nitajaribu kubainisha baadhi ya maeneo ambayo tukitumia hoja hiyo hiyo kwamba tunayo mikoa mitano maskini sana, mambo yapi tusifanye ili kuendelea kuifanya hiyo mikoa kuwa maskini zaidi. Najua yapo mambo mengine ambayo yanaweza yakafanywa lakini nijikite kwenye bajeti yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, katika ahadi tulizotoa kwa wananchi, maana ukiangalia mikoa hii baadhi yake inalima kahawa na wengine wanalima pamba, lakini kahawa kwa mfano tuna aina ya kodi 26 ambazo tulibainisha kwamba kodi hizi zitapunguzwa au kufutwa kabisa. Bajeti hii mapendekezo pekee ya kodi inayopendekezwa kufutwa ni ada ya kukaanga kahawa kwa ajili ya kuuza soko la nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, ile ada inayofutwa ni moja kati ya 26 zilizopendekezwa kupunguzwa au kufutwa. Kwa hesabu ya haraka haraka maana yake ni kwamba, hapo Mheshimiwa Waziri atakuwa ametekeleza asilimia tatu ya kile tulichoahidi. Kwa hiyo, mapendekezo yangu ni kwamba zile kodi 25 zilizobaki ingekuwa vizuri na zenyewe zikafutwa na zifutwe sasa katika bajeti hii kwa sababu hivyo ndivyo tulivyoahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukiangalia haraka haraka, je, wenzetu waliotuzunguka ndani ya Afrika Mashariki wanafanya nini? Uganda wao wana kodi ya asilimia moja tu katika zao la kahawa na ndiyo maana utakuta Watanzania wengi wanapenda kahawa yao wauze kupitia Uganda kwa sababu kule kuna unafuu wa kodi lakini sisi tuna kodi 26. Ukiangalia kwa nini tusifute kodi hizo hupati sababu. Vietnam kwa mfano wao wana asilimia moja tu kwenye zao la kahawa ambayo inakuwa *charged* kwenye *point of exit,*

Uganda wana asilimia moja, sasa sioni sababu kwa nini na sisi tusifanye hivyo na tufanye hivyo katika bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, wataalam wa uchumi wanatuambia mkulima wa Tanzania hasa wa kahawa yeye anatozwa wastani wa asilimia 70 ya fedha yote inakwenda kwenye kodi, lakini kwa Tanzania *corporate tax* ni asilimia 30 na akiwa amepata hasara halipi kodi hiyo, lakini kwetu sisi mkulima asilimia 70. Huyu mkulima apate faida, apate hasara, asilimia 70 ipo palepale. Kwa hiyo, nadhani hilo eneo tunaweza kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ukiangalia hii ada ya kukaanga kahawa inayopendekezwa kufutwa inamnufaisha nani? Ada hiyo inayanufaisha makampuni makubwa yanayofanya biashara ya kuuza kahawa nje na siyo wakulima wadogo wadogo. Kwa hiyo, nadhani kuna haja ya kulitazama hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tulipopitisha sheria hapa ya kuruhusu haya makampuni makubwa kuingia kwenye ushindani wa kununua kahawa, tulitoa angalizo na sheria iko wazi kwamba hawa tuliowaruhusu kununua kahawa kushindana na Vyama vya Ushirika, wasishindane na Vyama vya Ushirika kwenye *grass roots.* Tuliwaambia wakitaka kununua kwenye *grass root,* basi kule Moshi wasiende kushindana, wasifanye mambo mawili. Huwezi ukawa unanunua kwa mkulima, halafu unakwenda Moshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilichotokea hadi sasa ninavyozungumza, wanunuaji hawa wakubwa, kina *OLAM* na wengine wananunua kwenye *grass roots,* wakienda mnadani wanakwenda kununua kahawa yao tu waliyonunua, kwa hiyo unaua ushindani na inaleta tatizo kubwa kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo napenda kuizungumza haraka haraka, maana tuna mikoa mitano ambayo tunaambiwa ni maskini sana na sina ubishi lakini tufanye nini sasa. Kuna ugonjwa wa mnyauko fizari. Huu ugonjwa wa mnyauko fizari umeleta janga la kitaifa kwa sababu kwa muda mrefu Mikoa ya Kigoma, Kagera na mingineyo tumekuwa tukijitosheleza kwa chakula lakini baada ya huu mnyauko fizari kuanza hatuwezi kujitosheleza kwa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli nafikiri kutaja tu mikoa hii inaongoza kwa umaskini haitoshi, ningefurahia kama Mheshimiwa Waziri angetangaza kwamba kuna janga la kitaifa la kupoteza migomba, kwa hiyo tunakuja na mkakati maalum. Tunajua wataalam wetu wa kilimo wamejitahidi kutafuta ufumbuzi, ufumbuzi peke yake waliopata ni kufyeka, kwamba migomba ikipatwa na ugonjwa wa mnyauko fizari dawa ni kufyeka tu, kwa hiyo wanatembea na mapanga. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani dawa si kufyeka tu, hata kama ni kufyeka Mheshimiwa Waziri anaweza akaja na *physical*, bajeti inaweza ikasema tutakuja na panga la kufyeka lakini wakati huo huo tuna milioni moja, tunasema tukifyeka hapa kwa sababu umekumbwa na ugonjwa wa mnyauko fizari tunakupa fedha ya kukuwezesha kuishi kwa miezi sita, miezi saba, mwaka mmoja mpaka hapo utakapoanza kuvuna. Watakuita wenyewe wakulima kwamba njoo ufyeke hapa, lakini kama unatembea na panga tu na kama akili yetu inaishia kwenye kutembea na panga tu na kufyeka, basi tujue tutazidi kuongeza umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine la msingi kuna Benki ya Maendeleo ya Wakulima. Benki hii ya Maendeleo ya Kilimo yenyewe inasema kahawa si zao la *food security.* Napenda nitoe hoja hapa kwamba kahawa ni zao la *food security* kwa sababu mkulima akiweza kuvuna vizuri atauza atapata chakula. Kwa hiyo, ni uwezo mdogo wa kufikiri kusema kwamba zao la kahawa halihusiani na *food security,* si kweli. Kwa sababu ukishasema hivyo maana yake Vyama vya Ushirika vinalazimika kuendelea kukopa kutoka *CRDB* asilimia 18 ili viende kununua kahawa na vinakwenda kushindana na wanunuzi wengine wanaokopa nje kwa asilimia tatu na kuendelea, huwezi kushindana namna hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa harakaraka naomba nimtahadharishe Mheshimiwa Waziri, anafahamu kwamba alipokutana na wenzake katika Afrika Mashariki wamekubaliana kwa Kenya, vile viwanda vinavyozalisha ngozi na mambo mengine, wanapozalisha wa-*offload* kwenye soko la Kenya.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, unapo-*offload* bila kulipa italeta madhara makubwa kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, natarajia Mheshimiwa Waziri atanipa ufafanuzi akiwa anajibu hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na Mheshimiwa Mussa Ramadhan Sima kama muda utabaki Mheshimiwa Felister Bura ataendelea.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nichukue fursa hii kukushukuru sana, lakini nikupongeze kwa ukakamavu ambao unauonesha hapa Bungeni, Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji mzuri na ama hakika Watanzania sasa wanasubiri kuona mabadiliko ambayo tumewaahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja kwenye hoja, nianze na reli ya kati. Tunajenga reli ya kati kwa *standard gauge* lakini liwe jambo jema sana tuzingatie vituo vyote. Nafahamu pale Singida itapita Manyoni, Itigi na kuendelea mbele, lakini reli ya kati ilikuwa inakwenda mpaka Singida Mjini. Sehemu pekee ambayo ndiyo sehemu ya kibiashara iko pale mjini. Kwa hiyo, niombe Mheshimiwa Waziri katika vituo vyake asiache kituo cha Singida Mjini, almaarufu reli yetu ile tulikuwa tunaiita Kamnyampaa maana yake ndiye mzee mwenyewe yule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la pili, kwenye bajeti tumezungumzia ongezeko la kodi ya mitumba kutoa 0.2 mpaka 0.4. Ni lazima tuwe wakweli, Watanzania bado hatujawa na maandalizi ya kutumia viwanda vyetu vya ndani, ya kutumia nguo zilizoko ndani badala ya kutumia mitumba ambayo ni bei rahisi. Leo hii ukitazama vizuri sisi wote tunatumia sana mitumba kuliko nguo za dukani. Tukiongeza kodi maana yake tunaongeza thamani ya mitumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Mheshimiwa Waziri amezungumza kuna tatizo la kiafya na mambo mengine. Mpaka tunafikia umri huu kwa kweli wajibu wa Serikali ni kuwaelimisha Watanzania juu ya afya kuliko kuongeza kodi. Kama hiyo haitoshi, tumezungumzia ngozi, kwamba Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji itakuja na mpango madhubuti wa ku-*deal* na sekta ya ngozi, ni mpango gani huu? Tunazungumzia sekta ya ngozi wakati hatuna viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda hivi vinavyozungumzwa hapa vyote hivi vinatengeneza *wet blue, ni temporary turning,* ndivyo viwanda tulivyo navyo. Viwanda vinavyofanya *finishing*, utazungumzia Himo na Moshi *Tanneries* kule, viwanda viwili haviwezi kukidhi haja ya kutengeneza bidhaa kwa Watanzania wote milioni 50. Tunazungumzia sekta ya ngozi ambayo leo ngozi inaoza kwenye ma-*godown*, tuna tani karibu 5,000 zinaoza, halafu tunasema tutakuwa na mpango madhubuti. Nilitarajia mpango madhubuti ni kufungua milango, tuondoe ile kodi ya zaidi ya asilimia 80 ya *exportation* ili hawa watu waweze kuuza ngozi yao East Africa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeua kiwanda cha Mwanza *Tanneries* kwa sababu ya ukaribu wa ziwa, kitu ambacho siyo kweli. Hebu twende tukaangalie ile Jinja *Tannery*, ni mita 200 tu pale lakini kiwanda kinafanya kazi, leo tunaendelea kuua viwanda. Kwa hiyo, niombe Mheshimiwa Waziri, kwenye suala hili la ngozi, huu mkakati madhubuti unaozungumzwa ni vizuri ungeletwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni miongoni mwa wajumbe wa Kamati ya Viwanda na Biashara na nimeshiriki kwenye kikao cha wadau, wachuuzi wa ngozi na wale wenye viwanda vya ngozi, hakuna majibu thabiti yaliyotolewa ni namna gani tuna-*deal* na viwanda vya ngozi. Leo hii ngozi inaoza, ngozi imeshuka bei imefika mpaka Sh.100, inatupwa, lakini tunasema tumempa Waziri sasa aje na mkakati. Mheshimiwa Waziri wa Fedha, hakuna mkakati na kama upo uletwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la mafuta, tumeweka asilimia 10 kwenye *importation* ya *crude palm oil,* lakini mafuta yaliyoko ndani leo bado *VAT* inatutesa. Nilitarajia kuiona Serikali sasa inaondoa *VAT* katika bidhaa inayosindikwa. Tumendoa *VAT* katika bidhaa ambayo haisindikwi lakini mkulima yule yule ambaye analima alizeti, anaipeleka kiwandani, ikishatoka pale inalipiwa kodi asilimia 18, maana yake utakuwa hujamsaidia. Kwa hiyo, niombe sana tuondoe *VAT* pia kwenye mafuta yetu haya ya alizeti ambayo tunayatumia sasa, tutakuwa tumemsaidia mkulima wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu wa Kenya kwenye mashudu wameondoa *VAT* na sisi tunategemea sana haya mashudu yatusaidie. Niombe na sisi tuondoe *VAT* kwenye mashudu. Hii nayo itasaidia wakulima wetu wadogo wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini na mimi nichangie kwenye zile shilingi milioni 50 ambazo Serikali inazitoa vijijini. Kuna mambo mawili hapa, tunazungumzia shilingi milioni 50 vijijini lakini hatuzungumzii shilingi milioni 50 kwenye mitaa. Kama sababu kwamba vijiji vina mamlaka ya kisheria, yawezekana mnatutofautisha hapo, mimi nina mitaa 50 na vijiji 20, sasa tunakwenda kuleta mgawanyiko katika jamii ambayo inaongozwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Kama sababu ni kwa sababu vijiji vina mamlaka ya kisheria, basi ni vizuri sasa na mitaa hii ipewe mamlaka hayo hayo na wenyewe wapewe mgawanyo huo sawa, *unless otherwise* tuzungumzie shilingi milioni 50 vijijini kwenye vijiji na mitaa, hapo tutaelewana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini shilingi milioni 50 hii, wenzangu wamejaribu kuchangia nami naomba nishauri, tujifunze katika yale mabilioni ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, tusije tukazalisha mgogoro ambao hatukuutarajia. Tumekwenda na nia njema ya kuwakomboa Watanzania, lakini namna ya kwenda kusimamia zoezi hili la shilingi milioni 50 linaweza likawa mwiba mchungu sana kwetu hapo kesho.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niombe, kama tutashindwa kuanzisha *Community Bank* basi ni vizuri tutumie *NMB* kwa maana iko kila halmashauri, tuweke dawati litakalo-*deal* na hii shilingi milioni 50 li-*act* kama *Community Bank.* Tukiweka dawati pale *NMB* tayari usimamizi wa fedha zile utakuwa uko

salama. Sisi wanasiasa tuwe sehemu ya kuwahamasisha watu wetu kuanzisha vikundi na kwenda kufungua akaunti, lakini watakaotoa elimu hiyo wawe ni watu wanao-*deal* na fedha, jambo hili litakuwa limetuokoa na tunaweza kwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie usajili wa pikipiki. Asilimia 50 ya Watanzania leo wanatumia usafiri wa pikipiki. Vijana wetu leo wote unaowaona wamejiajiri kwenye usafiri wa pikipiki. Wanaolipa kodi na wanaochangia matibabu leo ni hao hao waendesha boda boda lakini tumeongeza thamani ya usajili wake kutoka Sh. 45,000 mpaka Sh. 95,000. Nilitarajia kuona utapungua badala ya kuongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumzia Watanzania kupata ajira, wako ambao tayari wamejiajiri. Ni lazima tuwatengenezee mazingira bora ili waweze kuboresha sehemu zao hizo za kazi. Naomba jambo hili pia nalo tulitafakari kwa kina tuone ni namna gani tunaweza kuwasaidia hawa waendesha boda boda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie na *property tax*. Nichukue fursa hii kuipongeza sana Serikali kwa hatua madhubuti ambazo wameamua kuchukua kwenye *property tax*. Yawezekana tukalitazama kwamba halmashauri zetu sasa zinakwenda kufa kwa sababu sehemu hii maalum imechukuliwa na *TRA*, la hasha! Ule mpango ambao tumejiwekea, kwenye Halmashauri yetu katika zile bilioni tatu ambazo tutakusanya ndani ni pamoja na *property tax*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyofahamu kwenye mpango huu kile kiasi ambacho tumekipanga *TRA* kwa maana Serikali itatuletea kama kilivyo, sasa silioni tatizo la *property tax* hapa, kwa sababu kama tumekubali kukusanya shilingi milioni 100 kwenye *property tax* Serikali inatuletea zile shilingi milioni 100, imetupunguzia mzigo. Kwa hiyo, nichukue fursa hii kuipongeza kwa dhati Serikali kwa hatua hii ambayo wamechukua kwa kweli *property tax* itatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nipongeze sehemu nyingine, tumeweka kodi ya asilimia 10 kwenye *importation* ya karatasi. Awali wakati nachangia kwenye viwanda nilisema, *Mufindi Paper Mills* walipewa jukumu la kutengeneza karatasi na si mifuko, lakini wamekuwa wakisafirisha *pulp* na kupeleka Kenya badala yake karatasi huku kwetu inaingia bure. Leo Serikali imeweke asilimia 10, naipongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niunge mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nilimtaja Mheshimiwa ambaye angechangia, lakini inavyoonekana muda hauwezi kutosha kumpa dakika kumi. Nitasoma majina ya wachangiaji wa mchana halafu nitaleta matangazo mawili.

Wachangiaji wa mchana ni Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Issa Ali Mangungu, Mheshimiwa Abdallah Chikota, Mheshimiwa Daniel Mtuka, Mheshimiwa Silafu Maufi, Mheshimiwa Sebastian Kapufi, Mheshimiwa Joram Hongoli, Mheshimiwa Leonidas Tutubert Gama, Mheshimiwa Mansoor Hiran, Mheshimiwa Zacharia Issaay, Mheshimiwa Emmanuel Papian, Mheshimiwa Seif Gulamali, Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve, Mheshimiwa Stanslaus Mabula, Mheshimiwa Mboni Mhita na Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri.

Waheshimiwa Wabunge, ninayo matangazo mawili:-

Tangazo la kwanza ni la kikao cha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria. Mwenyekiti wa Kamati hii, Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa anawatangazia kwamba leo saa 8.00 mchana kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo ambacho kitafanyika katika ukumbi wa Msekwa D. Wabunge ambao ni wajumbe kwenye Kamati hii mnaombwa kuhudhuria bila kukosa.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine ni la kuwakumbusha wajumbe wa Kamati ya Uongozi kwamba baada ya kusitisha shughuli za Bunge kutakuwa na kikao cha Kamati ya Uongozi, kitaanza saa 7.00.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 jioni.

*(Saa 6.54 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae, Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2015 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017**
**na**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimetaja majina kadhaa kabla hatujaenda mapumziko mafupi. Nilisema tutaanza na Mheshimiwa Ferister Aloyce Bura atafuatiwa na Mheshimiwa Issa Ali Mangungu, Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota ajiandae.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa kwanza mchana wa leo. Kabla sijasema jambo lolote, nimshukuru Mungu wangu kwa kunipa uzima, akili timamu na nguvu za kuwahudumia Watanzania wenzangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Naibu wake mdogo wangu Mheshimiwa Dkt. Tulia pamoja na timu nzima ya Wizara ya Fedha kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yoyote hakuna maendeleo bila kodi…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bura, anaitwa Dkt. Ashatu Kijaji. *(Kicheko)*

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nisamehe. Ni mdogo wangu, Mheshimiwa Dokta Ashatu Kijaji, Mbunge wa Kondoa Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yoyote haiwezi kuendelea bila kulipa kodi, kodi ndiyo msingi wa maendeleo. Kwa hiyo, kila mwananchi anatakiwa kulipa kodi kabla hajadai huduma lakini Watanzania tumezoea kudai huduma bila kulipa kodi. Tunadai hospitali, barabara, maji, umeme lakini ni wangapi wanaolipa kodi kwa uhakika? Wafanyakazi ni walipa kodi kwa uhakika kwa sababu pesa zao hawazikamati mkononi, wanakatwa kodi moja kwa moja. Ifike wakati sasa wananchi wa Tanzania tufurahie kulipa kodi ili maendeleo tunayoyataka tuyapate kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, sipingani na azma ya Serikali ya kuanzisha viwanda lakini tunapofikiria kuwa na viwanda tufikirie pia kuwa na malighafi. Tunasema mazao yanaoza; mazao gani yanayooza? Tunasema matunda

yanaoza Muheza, Ukerewe na maeneo mengi lakini je matunda haya yapo mwaka mzima kiasi kwamba tukiwa na viwanda vitano vya kukamua *juice* watapata malighafi ya kutosha? Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha mashamba makubwa kwa ajili ya malighafi kwa viwanda tunavyovipigia kelele? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima Serikali iweke mkakati madhubuti wa kuwa na mashamba makubwa ambayo pia yatazalisha ajira. Kwa hiyo, tuwe na mashamba makubwa tukilenga viwanda ambavyo tunataka kuvianzisha lakini tukisema tunaanzisha viwanda ku-*create* ajira bila malighafi viwanda hivyo haviwezi kufanya kazi. Kwa hiyo, tulitazame suala hili kwa upana wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kwa mkulima ni nani anayejali mkulima huyu kalima nini? Je, katumia mbolea? Je, analimaje? Je, anatumia zana gani? Maafisa Ugani wetu hakuna anayejali na hawatoshi hasa katika maeneo yetu ya vijiji. Kwa hiyo, kuna haja Maafisa Ugani kuwaweka wakulima katika hali ya kujua kwamba sasa malighafi kwa ajili ya viwanda vyetu inatakiwa na wawaelekeze wakulima kulima kwa lengo la kupata mapato zaidi kwa ajili ya kuendeleza viwanda vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kuna suala la kupata mapato, tumesema tunataka kodi ili tuwe na fedha za maendeleo kwa ajili ya Taifa letu. Hata hivyo, kuna suala la ubia kwa maana ya Serikali kuingia ubia na mashirika mbalimbali na watu binafsi lakini utekelezaji wa suala hili ni mdogo sana. Suala la ubia tumeliongea kwa muda mrefu sana katika Bunge hili lakini ni makampuni mangapi yameingia ubia na Serikali? Je, ni mashirika mangapi yameingia ubia na Serikali?

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano mdogo tu, sisi tulipelekwa Malaysia mwaka 2008 ili Wamalay waje wajenge barabara ya Chalinze – Dar es Salaam wakishirikiana na *NSSF* mpaka leo hatujaambiwa tatizo ni nini? Tungepata pesa kwa sababu wale wange-*charge* kodi kidogo kwa ajili ya kuendesha ile barabara lakini mpaka leo suala la ubia linakwenda taratibu mno katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *NSSF* walikubaliana na watu wa Malaysia kwamba watajenga magorofa 25 Ilala Mchikichini mpaka leo hakuna kinachoendelea. Hatuwezi kusema tunataka maendeleo, tunataka ubia wakati utekelezaji wa suala la ubia linaenda taratibu mno tatizo ni nini? Lazima tujue tatizo liko wapi? Hata tunaposema tunafufua viwanda, hawa watu wa viwanda wameulizwa mnakumbana na matatizo gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tujiulize walikumbana na vikwazo gani na tumeandaa akili zetu kupambana na changamoto tutakazokutana nazo katika masuala ya viwanda? Hili suala la *PPP* ni muhimu lazima kuliangalia. Tuwaulize *NSSF* kilichokwamisha ujenzi wa barabara ya Dar es Salaam – Chalinze ni nini? Watuambie kilichokwamisha ujenzi wa nyumba zile ni nini? Tungepata mapato mengi kutokana na suala hili, naomba tuliangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kuna haja ya kuangalia mashirika yasiyo na tija. Ngoja niwape mfano, tangu tuanzishe *RUBADA* wamesha-*deliver* nini kwa Serikali hii? Kuna watu waliomwambia Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere kwamba *RUBADA* tu inaweza kulisha Taifa hili lakini *RUBADA* iko wapi? Mpaka leo *RUBADA* wanapewa ruzuku. Mashirika yasiyo na tija yaondoke sasa kama kweli tunataka kupata maendeleo. Hakuna haja ya kuwapa ruzuku, wanalipwa mshahara, wanalipwa *per diem* za safari lakini hakuna tija, hili ni vizuri tukaliangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo kubwa la fedha *Tanzania shillings* kutotumika katika mauzo au manunuzi, tatizo ni nini? Suala hili tumelisema mpaka tumechoka. Naomba Waziri wa Fedha hebu suala hili lifanyiwe kazi sasa, nchi nyingi zilizoendelea wanathamini pesa zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tozo kwa watalii limeongelewa sana. Wabunge tujiulize kuna makampuni yalirudisha vitalu 13, kwa nini vilirudishwa? Lazima tujiulize kwa nini vilirudishwa ili tujue tanaanzia wapi kuliko kuanza na tozo wakati wenzetu Kenya wameondoa tozo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme lingine, tumechoka sisi wa Dodoma kila siku tunaambiwa Makao Makuu ya Serikali ni Dodoma lakini hatuoni kinachoendelea. Mashirika ya Umma, Ofisi za Serikali, mnajenga majengo Dar es Salaam, hivi mna dhamira ya dhati ya kuhamia Dodoma? Mimi nilileta Hoja Binafsi ili mtuambie kwa nini hamtaki kuhamia Dodoma? Mnatupaka mafuta kwa mgongo wa chupa, hatutaki! Mtuambie kwa nini hamtaki kuhamia Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma hana hata ofisi, Manispaa tutakwenda kumfukuza pale alipo ili mumtafutie pa kufanyia kazi zake. Hamtaki kuhamia Dodoma na hamtaki kumjengea Mkuu wa Mkoa ofisi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Mkungunero linatuumiza, Serikali hamtaki kulizungumza kwa nini? Wananchi waliomba heka chache sana kwa ajili ya kilimo, Maaskari wale wa Wanyamapori hawapiti kwa wananchi, hawapiti pale barabarani kwa sababu kuna uhasama mkubwa na Serikali haitaki kulishughulikia. Ninawasihi hebu suala la Mkungunero lifike mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake wa Mkoa wa Dodoma hawajatua ndoo vichwani na mvua inanyesha miezi miwili tu hapa Dodoma. Ukisema suala la maji, Waziri wa Maji anaturemba tu hatuelewi anachotusaidia. Tunaomba sasa, kama kweli Serikali ina dhamira ya kuhamia Dodoma tuanze kuwasaidia wananchi wa Dodoma, tumtue mwanamke wa Dodoma ndoo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake wanaamka saa tisa, ndiyo maana wanaume wa Dodoma wengine wameoa wanawake wanne, anafanyaje? Yeye ni Mkristo kila siku saa tisa mwanamke yuko barabarani kwenye maji, hatuwezi, jamani mtufikirie katika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Dodoma kuna Wilaya zilizoanza; tuna Wilaya ya Chemba, Wilaya ya Bahi ilianza siku nyingi hakuna maji, hakuna umeme, Mheshimiwa Badwel ameomba mpaka amechoka, Mheshimiwa Nkamia ameomba mpaka amechoka, tatizo ni nini kwa Wilaya za Dodoma? Bahi pale maji ni ya chumvi, huwezi kuoga, huwezi kunywa hata mnyama hanywi, kila mwaka tunaomba maji Dodoma, tatizo ni nini?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kengele ya pili hiyo.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, lakini msisahau kumuongezea *CAG*…

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea. Mheshimiwa Issa Ali Mangungu atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mheshimiwa Daniel Edward Mtuka ajiandae.

**MHE. ISSA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie bajeti hii ya Serikali. Mchango wangu ningeomba niondolewe mashaka na namtaka Mheshimiwa Waziri anijibu mashaka haya kwa sababu tuna-*experience* na jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *property tax* Halmashari zote tatu za Jiji la Dar es Salaam tuliwahi kukusanya mapato kwa mfumo huu lakini *TRA* walichukua chanzo hiki cha mapato, kukawa na ugumu mkubwa sana wa Serikali kurejesha au *TRA* kurejesha zile pesa kwa Halmashauri. Kama wakituthibitishia kwamba sasa hivi wamejipanga na wanaweza kuzirejesha pesa hizi kadri wanavyokusanya sisi tutaunga mkono hoja, hatuna hoja na hilo. Suala la kuchukua chanzo hiki na kuanza kuomba misaada mtakuwa mnatuonea, yaani itakuwa kama tunaomba na hii ipo katika maeneo mengi siyo kwenye *property tax* tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nina mfano wa barua ambayo Halmashauri ya Manispaa ya Temeke inaomba gawio la asilimia 30 kutoka Wizara ya Ardhi ya kodi ya ardhi karibu shilingi bilioni moja tangu mwaka jana mwezi wa nne mpaka leo, hata majibu ya kusema tumepokea barua wameshindwa kutoa. Siyo kwamba tunaomba msaada ni haki yetu, Halmshauri ina majukumu mengi inashindwa kutekeleza wajibu wake hatuna barabara, hatuna maji, hatuna hospitali lakini Wizara imekuwa si sikivu. Kwa hiyo, sisi tunachomba kama *TRA* wanapewa jukumu hili basi hizi pesa zirudi kwa wakati ili zilete maendeleo kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile kuna tatizo kubwa sana ambalo nimeliona la Serikali Kuu kutopeleka pesa za maendeleo kwenye Halmashauri zote nchini. Unakuta *Accounting Officer* pale, Mkurugenzi anasubiri *disbursement* kutoka Hazina miezi sita mpaka nane, matokeo yake inaiba vifungu vingine baadaye inaleta *query* kwa *CAG.* Kama Serikali imejipanga kutatua kero za wananchi basi pesa zipelekwe katika maeneo husika kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo langu la Mbagala ni jpya lakini kongwe kutoka Jimbo la Kigamboni. Jimbo letu tuna tatizo kubwa sana la barabara ambazo zimekuwa hazipitiki, maeneo mengine yamejifunga. Ukitoka pale Zakhem kwenga Kingugi lazima uzunguke, ni eneo la kwenda kama mita 500 unatumia kilometa tatu, barabara mbovu haipitiki na tumekuwa tukiomba lakini haijashughulikiwa. Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi imeizungumzia na Mheshimiwa Rais alivyokuja wakati wa kampeni pale Zakhem alituahidi, naomba Serikali itenge fedha kwa ajili ya kutimiza ahadi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile barabara ya kutoka Mtoni Kijichi kwenda Zakhem eneo la Mbagala Kuu imeharibika kabisa na hii ilikuwa ni ahadi ya Rais wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwamba barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami. Cha kusikitisha ni barabara ya kilometa mbili tu lakini mwaka huu imetengewa robo kilometa itengenezwa na *TANROADS,* huu ni utani. Rais alishaahidi, Serikali ilishasema itatekeleza, naomba Waziri mhusika atilie mkazo mwaka huu barabara ile iweze kuisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni la Hospitali ya Zakhem. Hospitali hii ina mkusanyiko mkubwa wa wagonjwa na inahudumia watu wengi lakini Serikali ilisema italipa fidia ili iweze kuchukua lile eneo lakini mpaka leo imekuwa ni hadithi. Naomba Serikali ije na majibu ya jinsi gani ya kuweza kupanua hospitali ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, lilitoka tangazo la Serikali kusema kwamba Wizara sasa imepandisha hadhi hospitali zile tatu za Mkoa wa Dar es Salaam za Amana, Temeke na Mwananyamala kuwa hospitali za Mkoa.

Huu mwaka wa saba sasa hivi Halmashauri bado zinazihudumia, Serikali imekwepa jukumu lake la kuchukua zile hospitali na kuzihudumia. Sasa tunaomba Serikali Kuu ichukue zile hospitali ili Halmashauri hizi ziweze kujipanga na kupeleka huduma mpaka chini. Wananchi wanapata taabu, tunazungumzia zahanati kila kijiji sisi hatuhitaji zahanati kila kijiji tunataka tuwe na hospitali inayohudumiwa na Halmashauri ipasavyo ili wananchi wetu waweze kupata huduma stahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, katika maboresho ya afya, eneo la Mbande hospitali ile sasa hivi imeelemewa. Tunaomba Serikali iongeze ruzuku kwenye hospitali ile ili ule upanuzi tulioahidiwa uweze kufanyika wananchi waweze kupata huduma za afya safi na za uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna eneo ambalo ningependa sana kulizungumzia kwenye Jimbo langu la Mbagala nalo ni suala la ulinzi na usalama. Serikali ilianzisha Mkoa wa Kipolisi wa Temeke lakini huu sasa ni mwaka wa saba hakuna kituo cha polisi hata kimoja ambacho Serikali imesema sasa baada ya kuanzisha Mkoa wa Kipolisi Wilaya ya Mbagala ina kituo cha polisi, ina kituo cha *OCD* na huduma zingine zinazostahili. Vile vituo ambavyo wananchi walivijenga ndiyo vinaitwa *police post* lakini vinafungwa saa tisa, mwanzo wa uhalifu vituo vinafungwa na unakuta kuna askari mmoja. Mbagala kuna tatizo kubwa sana la uhalifu wote mnafahamu, naomba Serikali ilitazame kwa jicho la huruma eneo la Mbagala.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kuzungumzia maboresho ya Mahakama. Tunasema tutoe haki lakini leo Mbagala ina Mahakama ya Mwanzo moja inayohudumia wananchi karibu 800,000 haki inapatikana vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile ili uweze kupata haki Mahakama ya Wilaya mpaka uende Temeke. Temeke yenyewe ina Jimbo la Temeke, Kigamboni inategemea Temeke, hatuna Mahakama. Leo tungekuwa na Mahakama Tuangoma, Mbande na maeneo mengine ingetusaidia kuharakisha kesi kumalizika kwa haraka. Kwa hiyo, naomba Serikali Kuu nayo ilitazame suala hili na kutusaidia kupata haki katika eneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende haraka haraka kwenye huduma za nishati ya umeme. Kuna mradi wa *REA* ambao ulikwenda katika maeneo ya Chamazi, Kwamzala, Mbande, Kwa Masista lakini wale wakandarasi wametupa nguzo wameondoka mpaka leo wameingia mitini. Sijui Waziri anatujibu nini kuhusiana na jambo hili kwani limekuwa kero kubwa maana Mbagala tupo Dar es Salaam lakini umeme hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna suala la *low voltage*. Jimboni kwangu ikifika saa 12 huwezi kuangalia televisheni, huwezi kuwasha friji kwa sababu umeme ni mdogo mno. Tunasema sasa tunakwenda kwenye uchumi wa viwanda tunakwendaje nao ikiwa tuna *low voltage* Mbagala? Mbagala tuna eneo la viwanda lakini bila tatizo hili kushughulikiwa suala la viwanda litashindikana.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo kuna kero kubwa ambayo wananchi wa Mbande wanailalamikia ni suala la Kilwa *Energy.* Huu sasa mwaka wa saba au wa nane hawajalipwa fidia na wameambiwa wasifanye shughuli zozote katika eneo unapopita ule mradi, hawa wananchi wanakwenda wapi na mbona hawalipwi?

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nimeongea na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati ananiambia wanategemea kupata pesa kutoka *TIB.* Kila siku wananchi wanaahidiwa kama hakuna pesa waambieni hakuna waendelee na shughuli zao za maendeleo. Kama pesa zipo walipeni waondoke pale kuliko kuendelea kuwanyanyasa na kuwasumbua pasipo na sababu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi kero zingine zinawezekana kumalizika. Maana ile *Kilwa Energy* inaanzia Somanga inakuja mpaka Mkuranga pale kwa Mheshimiwa Ulega, inakuja mpaka Mbagala, imekwenda mpaka Ilala ni tatizo. Mpaka watu washike mabango na waandamane ndiyo muelewe kama watu wanakerwa? Naomba Serikali kidogo ijirekebishe na iweze kutekeleza kwa wakati lile inaloahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la nishati kumekuwa na tatizo na Mheshimiwa Waziri katusomea bajeti yake kwamba gesi imepanda. Hata hivyo, gesi hii tunayoitegemea inatoka nje ile gesi ya Mtwara na maeneo mengine tunayoambiwa kila siku inakuja inakamilika lini ili Mtanzania wa kawaida aweze kutumia gesi maana maeneo yetu yale ukikamatwa na mkaa ni kesi. Sasa basi kama ni hivyo tupate nishati mbadala ya gesi, gesi yenyewe haipatikani na mnazidi kuipandisha bei. Naomba kama gesi ya Mtwara na Lindi bado haijapatikana, tupunguze tozo katika gesi wananchi waweze kupikia gesi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa vilevile kuzungumzia suala dogo tu maana najua kengele inaweza kugonga, kuna suala la mradi wa njia sita kutoka Bendera Tatu au pale *BP* mpaka Mbagala. Hii barabara ni muhimu sana kwa sababu wakazi wa Mbagala tunategemea na tunatarajia *DART Phase II* ije lakini ije kwa haraka na njia zile ziweze kupitika. Kumekuwa na msongamano na kumekuwa na matatizo makubwa, jioni kuna foleni, asubuhi kuna foleni. Kwa hiyo, kama mchakato huu upo uanze haraka ili wananchi na wao waweze kwenda na mwendo kasi kama ilivyo katika maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naona kuna tatizo kidogo la ufundi, katika mradi huu *feasibility study* ilifanyika miaka 10 iliyopita ndiyo maana ule mradi uliishia Kimara pale lakini mahitaji kwa Kimara pale siyo peke yake, Mbezi Kiluvya, Kibamba wote walikuwa wanahitaji. Kwa kule Mbagala mradi huu ulikuwa unaishia Rangitatu, *DART* wanataka kulipa fidia mpaka viwanda, kwa nini tuondoe viwanda ikiwa tuna uwezo wa kuusogeza mradi huu? Ileile fedha ya fidia ingetumika wangekwenda mpaka Kongowe eneo la Mwandege pale kwa Mheshimiwa Ulega, lile pori sisi kwetu ni kero, wahalifu wanajificha pale. Ondoeni lile pori wekeni kituo cha mabasi ya kisasa, wanaotoka mikoani wataishia pale, wanapanda mabasi ya mwendokasi wanakwenda katikakti ya mji na maeneo mengine. Ni suala la kukubaliana tu, si lazima kwamba *feasibility study* iliishia Rangitatu basi lazima tuishie Rangitatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile barabara ya kutoka Charambe kwenda Mbande iliwahi kuleta kashfa tangu Serikali ya Awamu ya Tatu na kuna baadhi ya Mawaziri walipelekwa Mahakamani. Barabara ile haina vituo, haina mifereji ya kuweza kuwafanya watu wakapita vizuri na haipitiki wakati wa masika…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa Mangungu, kengele mbili tayari zimeshalia.

**MHE. ISSA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota atafuatiwa na Mheshimiwa Daniel Edward Mtuka, Mheshimiwa Silafu Jumbe Maufi ajiandae.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Niungane na wenzangu kukupa pongezi kwa jinsi unavyoendelea kusimama imara na kuliongoza vizuri Bunge letu Tukufu. Sisi tupo pamoja na wewe na kwenye wengi kuna Mungu na kwenye Bunge hili sisi ndiyo wengi. Kwa hiyo, kaza buti na tunakutabiria kuna mambo mengine makubwa yatakujia mbele yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nichukue nafasi hii vilevile nimpongeze Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Mpango na Naibu Waziri wa Fedha kwa kuja na bajeti ambayo kwa kweli inaonyesha kuna matumaini kwetu sisi Watanzania. Kwa mara ya kwanza tumeona kwamba bajeti yetu ya maendeleo ni asilimia 40, haya ni maendeleo makubwa lakini tumeona jinsi gani bajeti hii inavyopunguza kero za wananchi. Mimi natoka Jimbo ambalo ni

la wakulima wakubwa sana wa korosho, kuna tozo tano pale zimeondolewa, hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nipongeze kwa ujasiri wa kutenga fedha nyingi kwenda Wizara ya Afya, karibu shilingi trilioni moja na bilioni mia tisa ambazo zitasaidia vilevile kulipa deni la *MSD*. Tunapolipa deni la *MSD* tuna uhakika sasa zahanati zetu, vituo vya afya, hospitali za wilaya na hospitali za rufaa za mikoa kutakuwa na dawa, wagonjwa wetu wakienda hospitali hawatarudi na cheti tu, watarudi na dawa. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali yangu ya Awamu ya Tano ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nianze kuchangia hili suala la tozo tano. Kama nilivyosema, niendelee kuipongeza Serikali yangu ya Awamu ya Tano kwa sababu hii ilikuwa ahadi ya Mheshimiwa Rais wakati anaomba kura. Alisema kwenye korosho kuna kodi nyingi na akiingia Ikulu atapunguza na mwaka wake wa kwanza ameanza na hizi tozo tano na hiki kitabu kinasema kwamba hii ni awamu ya kwanza, kazi inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nishauri sasa, Serikali au Wizara ya Kilimo itoe mwongozo, sasa hivi kuna hofu na kuna maneno mengine kwamba kuondolewa kwa tozo hizi kutaathiri mfumo wa stakabadhi ghalani. Kwa hiyo, naomba sasa Wizara ya Kilimo itoe mwongozo kupeleka kule chini kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa, mikoani na kwenye Vyama Vikuu vya Ushirika kwamba utaratibu gani utafuatwa kuhusu masuala ya usafirishaji wa korosho na minada ili tuwaondolee hofu wale ambao wanaanza kueneza maneno mengine kwamba kwa kuondosha tozo basi mfumo wetu wa stakabadhi ghalani utakuwa ni kifo chake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nitoe rai kwa wale wenzetu ambao wapo kwenye mfumo huu, mabadiliko yoyote yale lazima yalete hofu. Kwa hiyo, naomba sana wale ambao wanahusika na mfumo huu wa ununuzi wa korosho wajikite kuangalia *the way forward* na siyo kujadili kwamba tozo hii kwa nini itoke au isitoke, tuangalie mbele sasa baada ya kutolewa hizi tozo nini kifuate ili kuboresha uendeshaji wa mfumo wetu wa stakabadhi ghalani.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala langu la pili ni kuhusu *CAG* kuongezewa fedha. Bajeti ambayo amepewa *CAG* ni shilingi bilioni 44.6, hiki kiasi cha fedha hakitoshi. Ukiangalia kwenye fedha hizo kuna shilingi bilioni 12 ambazo ni za maendeleo lakini vilevile *CAG* ana deni ambalo amevuka nalo la shilingi bilioni nne kwa hiyo ukitoa kwenye hesabu hiyo bado fedha zake zinazidi kupungua. Hata hivyo, kwa maneno yake mwenyewe *CAG* wakati tunafanya *discussion* kule Dar es Salaam alisema kwa fedha hii sasa atashindwa kukagua Halmashauri 94. Sasa hebu piga hesabu, tuna Halmashauri 181, kama atashindwa kufanya ukaguzi kwenye Halmashauri 94, ina maana karibu nusu ya

kazi yake hataikamilisha. Kama Halmashauri 94 hazitakaguliwa unajua ni athari gani ambayo itapatikana kwa sababu fedha zetu nyingi tunazipeleka kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna ahadi ambayo ilitolewa kwamba ataongezewa fedha kwenye *mid-year review* pengine Desemba. Kwa *CAG* kupewa fedha Desemba yeye haimsaidii kiutendaji kwa sababu kwenye ukaguzi kuna *phases* tatu na zinakamilika kabla ya Desemba. Januari mpaka Machi kwa *CAG* ni muda wa kuandika ripoti, kwa hiyo *additional* yoyote ya fedha mwezi Januari kwake haimsaidii kwenye ukaguzi. Kwa hiyo, naomba sana tusimpe fedha wakati wa kuandika ripoti, tumuongezee sasa ili *CAG* aweze ku-*cover* maeneo yake. Kwa sababu punguzo hili la fedha, kwanza hata *scope* ya ukaguzi itaathirika lakini hata ubora. Kama unavyofahamu kwamba chombo chetu hiki sasa kilishapata hadhi ya Kimataifa. *CAG* sasa anakagua taasisi za Umoja wa Mataifa, kwa hiyo, tusimshushe nguvu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende tena upande wa *property tax* ambayo sasa tumesema kwamba itakusanywa na *TRA* badala ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Niwakumbushe tu Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba huko nyuma kulikuwa na *policy paper* ya *Local Government Reform* ilitolewa mwaka 1998, ina maeneo manne, mimi kwa sababu ya muda sitaki kuyataja mengine, lakini eneo kubwa ambalo ilitakiwa tutekeleze ni *financial decentralization,* lazima Mamlaka za Serikali za Mitaa tuzipe uwezo wa kifedha. Dawa ya mtu ambaye hana uwezo wa kukusanya siyo kumnyang'anya, nilitarajia kwamba tungekuja na mbinu za kuziongezea uwezo Mamlaka za Serikali za Mitaa kukusanya lakini kusema hawana uwezo tupeleke *TRA* hiyo kwa kweli siyo *solution.* Tufanye kwa mwaka huu kwa sababu tumeshaamua hivyo lakini naomba sana Serikali yangu Tukufu tuangalie jinsi ya kuziwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa ili ziweze kukusanya fedha za kutosha, zikikusanya fedha za kutosha basi wataweza kutoa huduma ambazo tunazitarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tuwe na wazo la kuzipa Mamlaka za Serikali za Mitaa vyanzo ambavyo ni vya uhakika. Vyanzo vilivyobaki kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa havina uhakika na mapato yake ni ya kusuasua. Kwa hiyo, tuangalie kwenye suala la ugatuaji wa madaraka siyo kupeleka mamlaka tu kule, tupeleke na fedha. Hii inanikumbusha wazo la Mheshimiwa Oliver ambaye alisisitiza sana umuhimu wa kuwa na semina ya ugatuaji, semina ya *D by D* kwa Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Mawaziri kwa sababu sasa hivi inaonekana kwamba tunataka kurudi nyuma tulikotoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Daniel Edward Mtuka atafuatiwa na Mheshimiwa Silafu Jumbe Maufi, Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi ajiandae.

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nashukuru kwa muda huu kupewa na mimi nafasi ya kuchangia bajeti kuu. Nianze moja kwa moja kuchangia bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumzia bajeti iliyotengwa kwa vyombo ambavyo vinatakiwa kusimamia bajeti hii, taasisi simamizi, *oversight institutions,* kwa maana ya TAKUKURU na Ofisi ya *CAG*. Ni kweli wazungumzaji wengi wameongea, Ofisi ya *CAG* ni muhimu, ndiyo jicho, tunajua asilimia 40 imetengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo, lazima kuwe na jicho hili, tumuongezee pesa huyu afuatilie fedha hizi, hii shilingi bilioni 44.7 haitoshi, tunaomba aongezewe fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini TAKUKURU pia, wengi walikuwa wanasema amewekewa hela nyingi, hakuna, hela imepungua. Naomba ku-*declare interest* kwamba mimi nimekuwa Kamanda wa TAKUKURU - Kanda Maalum mpaka nakuja hapa. Mkoa wa Dar es Salaam kwa muda wa miaka mitano, kwa mfano 2012/2013, *OC* ambayo ndiyo inayotumika kwa ajili ya mafuta watu waweze kwenda kufanya kazi, ndiyo kuna *per diem* za watu zipo hapo ili waende kufanya kazi, ndiyo kuna fedha za *stationeries* kwa ajili ya kwenda kufanya kazi ilikuwa shilingi bilioni 16, mwaka 2013/2014 ilikuwa shilingi bilioni 15.5, mwaka 2014/2015 ilikuwa shilingi bilioni 16.5, mwaka 2015/2016 ilikuwa shilingi bilioni 14.2 ikapungua, mwaka huu wa fedha 2016/2017 ni shilingi bilioni 12.03, imepungua sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia hii 40 inakwenda kwenye miradi, watu mambo yameongezeka lakini pia taasisi hii watu wamekuwa wengi, wapo wafanyakazi karibu 2,001, magari yameongezeka, mafuta yanahitajika lakini tunayo shilingi bilioni 12 tu. Kipindi kile kabla sijastaafu kule tulikuwa tunajibana sana kwa hizi shilingi bilioni 16, 15, 16, 14, sasa mwaka huu hata fedha yenyewe imeshuka wanakuja kwenye shilingi bilioni 12 yaani hii hela ni ndogo mno, sijui, namhurumia sana huyu Mkuu wa TAKUKURU sijui atafanya kazi gani. Atafanya lakini kwa kujinyima na hali kwa kweli ni ngumu sana, wanategemea kufungua wilaya nyingine 25, wana-*operate* mikoa yote, wilaya zote za zamani, sijui watafanya nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, rushwa ndugu zangu ni adui wa haki, rushwa tunaona madhara yake ni makubwa mno, taasisi hii iko kila mahali. Rushwa imesababisha migogoro ya ardhi, ni kazi ya ofisi hii, rushwa imeingia michezoni watu wanapnga matokeo ni kazi ya taasisi hii, rushwa imeingia hospitalini, twende mahakamani watu wanabambikiwa kesi vituo vya polisi ni kazi ya ofisi hii, wakandarasi tunapata wabovu yaani kuna vurugu. Nenda sekta ya ardhi akina mama wanadhalilishwa, rushwa ya ngono, ajira, ni kazi ya TAKUKURU kwenda kule. *CAG* ni moja wa *informers* wa TAKUKURU, makabrasha yale yote

yanashughulikiwa na ofisi moja tu. Bado nchi nzima wanapeleka taarifa TAKUKURU, atafanyaje kazi huyu?

Mheshimiwa Naibu Spika, najua hii haiwezi kubadilishwa lakini kipindi kijacho naomba suala hili litazamwe upya. Najua Watanzania wanajua hizi hela zilivyotajwa 72.3 labda ni nyingi, hapana, siyo nyingi, kuna mambo ya mishahara ile ni *fixed,* kuna ujenzi wa Ofisi ya Ushauri ya Afrika kule Arusha, ndiyo imeweka *amount* hii imekuwa kubwa lakini zile za kufanyia kazi ni ndogo mno na kwa kiasi ambacho kimepunguzwa sana mwaka huu, nawahurumia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba taasisi hii ndugu zangu hebu tuisemee, tuitetee, ndiyo mkombozi wetu huyu. Nchi imechanwachanwa vipandevipande kwa sababu ya rushwa. Tunasimika viongozi wabovu kwa sababu ya rushwa, tuimarishe hiki chombo kifanye kazi vizuri. Yapo mambo mengi ambayo chombo hiki kinafanya inabidi tukisemee, ndiyo mkombozi wetu katika nchi hii yaani chombo hiki kikilegalega ambacho ndiyo msimamizi wa mapambano haya hali itakuwa ngumu sana. Hata uchumi wa viwanda tunaouzungumzia sijui tutakwendaje kama hatujaimarisha taasisi hii. Kwa hiyo, tuzisemee taasisi mbili hizi simamizi CAG na TAKUKURU, hawa ni mapacha, lazima tuwatetee, wapewe fungu kubwa hawa ili wafanye kazi. Nilitaka niseme hilo kwa uchungu mkubwa kwa sababu naitazama Tanzania yangu nakata tamaa kwa sababu hivyo vyombo vimepewa hela kidogo sana vitasimamiaje majukumu yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kidogo *property tax,* kuna ugomvi hapa kidogo, *TRA* ni wataalam wenyewe wa mambo ya kodi, ni mahiri kwenye mambo ya kodi lakini pia Halmashauri kuna wataalam wa mambo ya ardhi, wathamini wanaojua thamani za ardhi. Kodi hii huwa ina-*base* kwenye thamani ya jengo pamoja na ardhi, *TRA* siyo wataalam wa mambo ya ardhi, wataalam wako kwenye Halmashauri, kwa hiyo kuna mambo mawili hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nashauri, acheni wataalam wa ardhi wafanye makadirio ya kodi hii, wakabidhini sasa hawa mahiri wa kukusanya kodi maana wao ni kukusanya tu siyo kukadiria. Ndiyo maana kuna mchangiaji mmoja amesema inafika mahali sasa mnatoza *flat rate,* kibanda cha jiko kinakuwa na kodi yake, nyumba kubwa inakuwa na kodi yake, kwenye *evaluation* hatufanyi hivyo wataalam wa ardhi. Jengo moja linakuwa na vijengo vidogovidogo, vinaitwa *art building,* ni sehemu ya jengo kubwa, wataalam wanajua, waachieni wataalam wakadirie kodi hii, *TRA* wenyewe ni wataalam wa kukusanya tu, basi. Naomba hili Mheshimiwa Waziri alizingatie sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie Singida, Mkoa wangu ninaoupenda. Nimesoma hiki kijitabu kidogo kinachozungumzia hali ya uchumi, ukurasa wa 10, Singida ni namba nne kwa umaskini katika nchi hii. Jamani

hatukujitakia, tumejikuta tuko pale Singida, tumezaliwa pale, ndiyo mkoa wetu sisi. Ndiyo mkoa wetu ule…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Silafu Jumbe Maufi atafuatiwa na Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, Mheshimiwa Joram Ismael Hongoli ajiandae.

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kutoa shukrani kwa kuweza kunipatia nafasi hii. Napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kuweza kunipatia afya njema na leo hii kuweza kusimama tena mbele ya Bunge lako Tukufu kuzungumza haya nitakayozungumza muda si mrefu. Nakutakia kila la kheri, Mwenyezi Mungu akupatie afya njema, akupatie wepesi kutokana na kazi nzito unayoifanya. Ujue ya kwamba tunakuombea na tunaendelea kukuombea upate afya hiyo mpaka mwisho wa Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia kuhusu bajeti ya Serikali. Nadhani wataalam tuliokuwa nao waliweza kujifunza katika kipindi kilichopita cha Awamu ya Nne na kufuatana na kasi ya Rais wetu mpendwa Mheshimiwa John Pombe Magufuli kuhitaji kuweka asilimia 40 ya fedha kwenye maendeleo ya wananchi wake basi itawekwa msingi madhubuti kuweza kumhakikishia Rais huyu kusimama kwa miguu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati mbaya nimeona kila Mbunge anayesimama hapa hayuko rafiki na bajeti hii, sijui hii Wizara haikuwa makini kufikiria na kuona hii kasi ya Mheshimiwa Rais itakwendaje ama itaanzaanza vipi katika kuhakikisha kwamba asilimia 40 inapatikana na maendeleo ya wananchi yanapatikana. Kwa nini nasema hivyo? Ni kwa sababu Wizara hii imekwenda tofauti na Kamati ya Bajeti jinsi ilivyotoa mapendekezo yake, hii inaashiria wazi kwamba Wizara haikuona umuhimu wa Kamati hii kufanya kazi kwa niaba yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nastaajabu kwa nini ameileta bajeti hii kwetu na sisi Wabunge wenzetu walikataa mapendekezo yao? Kama kweli aliona thamani ya Wabunge kwamba lazima wapitishe bajeti hii basi angehakikisha mapendekezo ya Kamati ya Bajeti yanazingatiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia suala la afya. Tunafahamu wazi kabisa kwamba afya ya mtoto mama ndiye anayesimamia

siyo hilo tu mama ndiye anayesimamia hata malezi ya baba. Baba akiugua ndani ya nyumba mama ndiye mwajibikaji wa kuhakikisha afya ya baba inakuwa katika usalama na hali kadhalika ya mtoto. Sasa mama huyu tunamwekea mazingira ambayo siyo mazuri kwake, tunaendelea kumuongezea mzigo juu ya mzigo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumzia nini? Nazungumzia zahanati. Ukichukulia mfano wa Wilaya ya Sumbawanga Mjini kuna kata saba zinazozunguka mji ule lakini hazina kituo cha afya, zina zahanati lakini baadhi ya zahanati kwenye vijiji ni maboma ambayo bado hayajakamilika. Halafu Waziri wa Fedha anasema hakuna fedha ambazo zimewekwa kwa ajili ya kukamilisha zahanati hizi, kwa ajili ya kukamilisha vituo hivi ili huyu mwanamama awe na huduma ya afya karibu na yeye mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani Wizara hii kwa sababu inafahamu wazi kanuni sijui sheria ya 106 inayosema kwamba sisi kama Bunge hatuwezi kubadilisha kifungu chochote labda ndiyo maana amekuwa na kichwa cha kusema kwamba hata wakisema hayawezi kubadilika kwa wakati huu. Sisi tunasema ni vyema Wizara ikawa na ushauri mzuri ama ikawa na maelekezo mazuri na kutukubali sisi Wabunge kama ndiyo tunaosimamia Serikali katika kuiongoza nchi hii. Waziri akienda kinyume na ukweli huo hatakuwa rafiki wa Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, kama amekosea kipindi hiki tunaomba kipindi kinachokuja aje na fungu maalum la kuhakikisha miundombinu ya zahanati, miundombinu ya vituo vya afya inakamilika kwa maana ya *theater* ili akina mama waweze kufanyiwa upasuaji wakati wa zoezi la kuongeza idadi ya wananchi wa Tanzania hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu shilingi milioni 50 kwa vijiji ambapo shilingi bilioni 59 zimetengwa. Imesemwa hapa kwamba hazitasambazwa nchi nzima bali watachukua maeneo maalum kama *pilot program*. Mimi nasema Mheshimiwa Rais alisema ni kwa nchi nzima leo hii tukisema tunachukua baadhi ya mikoa iwe ndiyo shamba darasa la hizi shilingi milioni 50 ndani ya vijiji vyao tutakuwa hatujawatendea haki wengine. Ushauri wangu kama ni kutafuta mashamba darasa ya kuona hii shilingi milioni 50 itakwendaje basi ni vyema hizi shilingi bilioni 59 zigawanywe ili kila Jimbo waweze kupata vijiji viwili ama vijiji vitatu viwe ni *pilot program* katika maeneo hayo ili na wale ambao wanawazunguka waweze kujifunza nini makosa ya wenzao kuliko ukisema kwamba *pilot program* inakuwa Tanga mimi niko Rukwa wapi na wapi? Tunaomba tuweke kwa kila Jimbo ili tuweze kupata *pilot area* ya kujifunza sisi wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la asilimia 10 halikuweza kutekelezeka kwa sababu ndani ya Kamati ya Bajeti ama Kamati ya Fedha ya Halmashauri hakuna anayelizungumzia wala hakuna anayelifuatilia wala hakuna mwenye

uchungu nalo. Kwa nini? Ni kwa sababu Wabunge wa Viti Maalum ama Waheshimiwa Madiwani wa Viti Maalum kwenye ile Kamati hawamo na ndiyo wenye uchungu na vijana na akina mama wenzao. Naomba Wizara inayohusika isiwe na kigugumizi itoe tamko rasmi kwamba hawa Madiwani wa Viti Maalum na Waheshimiwa Wabunge waingie kwenye Kamati ya Fedha za Halmashauri wakazungumzie na kufuatilia asilimia yao 10. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndani ya bajeti yetu tumesema Wizara ya Utalii ndiyo ambayo inaleta fedha za kutosha takribani asilimia 25 lakini mazingira yanayotengenezwa kwa huu utalii si rafiki. Badala ya kupata zaidi ya asilimia 25 ni dhahiri katika kipindi kifupi tutapata chini ya asilimia 25 na kwa maana hiyo uchumi wetu utaanguka. Nasema hivyo kwa sababu wenzetu wa Kenya katika bajeti ya mwaka 2016/2017 wametenga shilingi bilioni 90 sisi tumeweka shilingi bilioni 135 lakini si kwa utalii peke yake ni pamoja na Maliasili na Utalii. Kama wakigawana pasu hawa kila mmoja anapata shilingi bilioni 67.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Hii saa inasema uongo sasa. Naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Maufi. Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi atafuatiwa na Mheshimiwa Joram Ismael Hongoli, Mheshimiwa Mheshimiwa Leonidas Tutubert Gama ajiandae.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mahali popote panapohitaji kupongeza isomeke kwamba nimepongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kulisema hilo, naomba nianze na suala zima la vyanzo vipya vya mapato. Nimeipitia hii taarifa ya Kamati ukurasa wa kwanza, nanukuu, imesema hivi, bado Kamati imebaini kuwa Serikali haijaonyesha utayari wa kupokea ushauri hususani eneo la ukusanyaji wa mapato kwa kutumia vyanzo vipya, ni taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, habari ya bia na soda kabla sijazaliwa, nimezaliwa, nimekua, nimesoma ukisikiliza vyanzo vya mapato ni hivyo hivyo hatuwezi tukaja na vyanzo vipya, hatuwezi tukabuni vyanzo vipya! Nchi yetu nzuri ya Tanzania uwepo wake tu wa kijiografia ambao ametujaalia Mwenyezi Mungu hicho ni chanzo namba moja cha mapato. Uwepo wa hapo Tanzania ilipo nasema ni chanzo kikubwa cha mapato. Niwaombe wataalamu wetu katika eneo hilo waangalie suala hili tuna bandari, utalii, ukiniuliza nashangaa kwa nini soda na bia mpaka leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna nchi nyingine utaambiwa chanzo chake cha mapato labda ni suala la maua tu, kuna nchi nyingine chanzo chake cha mapato ni fukwe na kuna nchi nyingine chanzo chake cha mapato ni madini. Sasa turudi kwa Tanzania yetu mbuga tunazo, wanyama tunao, maua tunayo, fukwe tunazo, bandari nzuri tunazo tumekosea wapi, tunashindwa wapi? Niseme tutakuwa tunamsingizia Mwenyezi Mungu kwamba labda Mungu hajatusaidia ametupa fursa zote hizo tunashindwa wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri wasomi wetu tunao, kwa nini tusitumie nafasi hii ya kijiografia? Ndiyo maana watu wengine walikuwa wanasema wangebahatika kuwa hapa Tanzania wangefanya maajabu. Kwa hiyo, niwaombe wataalamu ambao wamepewa dhamana na Watanzania hebu watusaidie kuitoa Tanzania hapo ilipo kwa maana ya kuibua vyanzo vipya vya mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sambamba na hilo la vyanzo vya mapato amani hii na utulivu ambayo Mwenyezi Mungu ametujalia, hali nzuri ya hewa ambayo Mwenyezi Mungu ametujalia kwa nini tusivitumie kama fursa nzuri? Hayo tu tukiyafanyia kazi wala tusingekuwa na sababu hapa ya kuumizana vichwa kuhusu habari ya kiinua mgongo cha Wabunge na mambo mengine ya namna hiyo kwa sababu vyanzo vipo na ni vingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa taarifa inatuonyesha kwamba Pato la Taifa limeongezeka kutoka 7.0 mpaka 7.2. Wananchi wetu wa kawaida ukiongelea habari ya ongezeko la pato wao wanatamani waone kwa macho na washike kwa mikono yao hilo ongezeko. Habari ya ongezeko la pato kwa kupitia maandishi kama hali ya mfuko wake ni korofi hawaipati sura hiyo. Tunasema kwamba nchi yetu tumepiga hatua kwa maana ya ongezeko ya Pato la Taifa basi uchumi usomeke kwenye mifuko ya watu, uchumi usomeke kwa yale wanayoweza wakayaona ndiyo tutakuwa na jambo la kuongea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la maji, napata tabu sana ukirudi hata katika ramani iwe ni ramani ya East Africa ama ya dunia Tanzania yetu imezungukwa na maji nchi nzima kuna *Lake* Tanganyika, *Lake* Victoria, *Lake Nyasa* lakini hata Bahari ya Hindi. Kuna nchi nyingine wanafanya kazi kubwa ya kuyabadilisha maji ya bahari kuwa maji ya kunywa Tanzania hatujafika hapo. Mimi nilikuwa natamani ule mtandao wa buibui jinsi ulivyo Tanzania hii ingeweza kuunganishwa kwa maji kwa sura hiyo. Maji yangeweza kuvutwa kutoka *Lake Victoria* yakafika upande mwingine, yakavutwa kutoka L*ake Tanganyika* yakafika upande mwingine na yakatoka *Lake* Rukwa yakafika upande mwingine. Leo kuendelea kuongelea habari ya maji kwa nchi ambayo imezungukwa na maji sipati picha, vipi hawa watu wengine ambao hawakupata baraka hii ya kuwa na maji?

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitembelea nchi moja wale watu pamoja na kwamba wanapata mvua mara moja ndani ya miaka mitatu wameweza kutengeneza ziwa *(man made lake)*. Huwezi kuamini ni kubwa linawasaidia kupata maji lakini kufanya utalii kwa sababu wanaenda watu pale kufanya utalii wanapata samaki lakini huku chini wanaweza kumwagilia pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa Tanzania hii mimi narudi kwenye maandiko hivi ni nani ameturoga? Ukiangalia jiografia maeneo mengine jinsi milima ilivyokaa wala hauhitaji kufanya kazi kubwa ya kusema sijui utachimba bwawa ni suala la kukinga tu na wataalamu tunao. Ukishakinga hapo unatengeneza mazingira ya kuwa na maji ya kutosha, hatujafika mahali pa kulalamika suala la maji hebu tubadilike tuache kufanya kazi kwa mazoea. Tusiogope kuthubutu kuja na miradi mikubwa ambayo itakuwa ni ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu, tusifanye kazi kwa mazoea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoke hapo nizungumzie kuhusu msamaha wa kodi kwa wanajeshi wetu. Jambo hili linaweza likawa jema lakini naomba niwakumbushe wapo wadau wengine kama askari wastaafu wale nao tunafanyaje ambao walikuwa ni wanufaika wa suala hili? Naomba wakati tukiliangalia hilo nao tusiwasahau. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *CAG* halikwepeki, ni vizuri akaongezewa fedha. Nikirudi TAKUKURU kama ilivyo neno lenyewe ni Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kwa hiyo, si muda wote wanapambana kuna wakati mwingine wanazuia. Kwa hiyo, katika suala la kuzuia wanahitaji fedha, naomba nao wafikiriwe. Lakini baada ya kutoka hapo, naomba nizungumzie suala moja. Nafahamu nafasi ya Watanzania walioko nchi za nje tunafanyaje kwa maana ya ndugu zetu hawa kurudisha mapato nyumbani? Naomba nalo hilo tuendelee kuliangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wakati tukiwa tunaongelea mipango mipana niseme jambo moja, ukienda nchi za watu utakuta vijana wengi wa kutoka Kenya wanafanya kazi huko wanatumia hata nafasi ya Kiswahili kufanya mambo makubwa katika nchi nyingine. Sisi kama Watanzania nafasi ya Kiswahili tunaitumiaje? Kuna sehemu tumesema tufanye kwa makusudi kuhakikisha watu wanakwenda nje wakitumia nafasi hii ya Kiswahili na kwa kuwa huko nje wana uwezo wa kuzalisha na kurudisha fedha ndani, hilo tumejaribu kulifanya?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Joram Ismael Hongoli atafuatiwa na Mheshimiwa Leonidas Tutubert Gama, Mheshimiwa Mansoor Shanif Hiran ajiandae.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia kidogo kwenye hii bajeti ya mapato na matumizi. Nianze kuanza kwa kukushukuru wewe binafsi na kukupongeza kwa kuendelea kukalia hicho Kiti, usiwe na wasiwasi wewe tulia kama jina lako linavyosema, sisi tuko pamoja na wewe kuhakikisha kwamba mambo yanaenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee nimpongeze Waziri wa Fedha na Naibu Waziri wake kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya. Bajeti yao iliyoletwa inaonyesha weledi na umahiri mkubwa wa kazi ambayo wamepewa na Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, inaonyesha kazi hii wanaweza wakaimudu vizuri na watatusaidia kuhakikisha kwamba uchumi wetu unakua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuchangia kidogo kwenye upande wa huduma ya maji. Tumesikia Wabunge wengi wamesema sana hapa kuhusu suala la maji na wametoa mapendekezo mengi sana, tunaomba jambo hili tulitilie mkazo sana na tulifanyie kazi. Wabunge wapendekeza kwamba tuwe na tozo ya Sh.50 ili kwenye shilingi bilioni 125 basi ziongezeke zifikie shilingi bilioni 250 ili wananchi wetu wengi ambao wanaishi huko vijijini waweze kupata maji, tatizo liko wapi? Kama sisi ndiyo tunaopanga na tunawashauri kwa nini tusiongeze hizi Sh.50 kwa lita ya mafuta ili wananchi wengi wanaoishi vijijini waweze kupata maji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vijijini kule sasa hivi tunawahamasisha wajenge vyoo vya kisasa lakini vijiji vingi havina maji. Hata ukiangalia kwenye bajeti ya maji, miradi mingi ya maji mikubwa mikubwa imeelekezwa mijini na hata fedha iliyotengwa kwa maana ya maji vijijini bado zinaelekezwa mijini. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kutoa majumuisho tunataka kujua ni nini amefanya hasa kuhakikisha tozo ya Sh.50 kwa kila lita moja ya mafuta inaongezeka na kuwa Sh.100 na hatimaye tuweze kuongeza usambazaji wa maji vijijini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee kidogo kwenye kilimo, niipongeze Serikali kwa kuondoa kodi hasa kwenye mazao ya matunda na mboga mboga kwa maana ya mazao yale ambayo hayajafanyiwa *processing*, niwapongeze sana. Pia niipongeze Serikali kwa kupunguza kodi kwa baadhi ya mazao ya biashara kama vile chai, kahawa, korosho na mazao mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba pamoja na kupunguza kodi kidogo bado tusipokuwa makini tutafanya Watanzania wabaki kwa kutokuwa na uwezo wa kulima kwa kiasi kikubwa na kuweza kuzalisha kiasi ambacho kitatutosha kulisha hivi viwanda vyetu ambavyo tunaanza. Ni lazima tuhakikishe kwamba hawa wananchi wanawezeshwa ili kuzalisha kwa kiasi cha kutosha, kingi zaidi na kuzalisha matunda ambayo yanakuwa ni bora ili yaweze kupata soko, waweze kupata kuuza kwenye hivi viwanda ambavyo tunatarajia vitakuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutawezaje kufanya hivyo? Ni lazima tuwawezeshe kwa kuwapelekea Maafisa Ugani. Vijiji vingi sasa hivi havina Maafisa Ugani, wananchi wanalima kilimo kile kile cha utamaduni bila kuzingatia kanuni bora za kilimo. Kwa hiyo, tuombe Wizara husika kwa pamoja tupeleke Maafisa Ugani wa kutosha ili waboreshe kilimo vijijini na hatimaye waweze kupata faida kwenye mazao yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nijaribu kuchangia kwenye upande wa elimu. Ni kweli Serikali imepeleka fedha nyingi, tumeona ina mpango wa kupeleka trilioni 4.77 ambayo ni sawasawa na asilimia 22.1. Fedha hizi ili ziweze kufanya kazi ambayo imekusudiwa. Ni muhimu sana hizi fedha zipelekwe kwenye maeneo haya ya shule kwa wakati. La sivyo fedha hizi hazitafanya yale malengo ambayo yamekusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejifunza miaka ya nyuma, fedha zimekuwa zikitengwa kwa ajili ya kuendeshea mashule, lakini zinakwenda kwa kuchelewa, zinaenda miezi ya Tano na Sita; na inapofika tarehe 30 wale Wakurugenzi na Wakuu wa Shule wanatakiwa kurejesha hizi fedha tena Hazina, zinarudi tena bila kufanya kazi. Kwa hiyo, niombe mamlaka husika zipeleke hizi fedha kwa wakati ili zifanye kazi ambazo zimekusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongee kidogo pia kwenye suala la afya. Ni kweli, nitoe pongezi kwa Serikali, tumetenga trilioni 1.99 ambayo ni sawasawa na asilimia 9.2 ya bajeti nzima na hizo fedha tumesema zinaenda kwa ajili ya vifaa tiba, vitendanishi *(reagents)* na miundombinu, kwa hiyo, tuombe hizi fedha ziende kwenye vituo vya afya vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wengi wanategemea sana hivi vituo vya afya, kwa hiyo ni muhimu sana kuviboresha ili kuhakikisha kwamba angalau vituo vyote vya afya vinatoa huduma ya upasuaji pamoja na huduma kwa akinamama. Tunasema wanawake na watoto wengi wanafariki, ni kwa sababu huduma za afya hasa vijijini hazijaboreshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia *statistics* wanaokufa wengi ni wale watu wa vijijini, ni kwa sababu wanakwenda hospitalini kwanza kwa kuchelewa kutokana na kutembea umbali mrefu, wakifika hakuna huduma nzuri, wanatakiwa wasafiri au wasafirishwe kwenda kwenye Hospitali za Wilaya ambazo zipo mbali. Wanafika huko wakiwa wamechelewa, hatimaye watoto wao wanafariki au wanapata *operation* na mwisho wa siku wanapata matatizo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nisemee kidogo kuhusu hii sheria ya magari, kwa maana ya kodi ya usafiri na uhamisho wa umiliki, ambayo ipo Sura namba 124, hasa kwenye upande wa pikipiki. Katika Ilani yetu tulisema tunataka hawa bodaboda sasa kwa hizi kazi wanazozifanya za kusafirisha, ziwe ni kazi rasmi. Nilitegemea kwamba leo hii tungekuwa tunaongelea kupunguza kodi za pikipiki, kwa kuwa hizi pikipiki nyingi wanazozitumia ni zile ambazo wamekodishwa na matajiri. Sasa tunataka hawa waendesha bodaboda waendelee kubaki maskini? Waendelee kuwasaidia watu wengine wenye fedha?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaomba hili ongezeko la kodi kutoka sh. 45/= mpaka 95/= liondolewe ibaki ile ile na ikiwezekana ipunguzwe zaidi ili vijana wetu ambao huko nyuma walikuwa wanafanya kazi za wizi, utapeli na kupiga watu nondo wajiajiri kwenye uendeshaji wa boda boda. Kwa kuwa boda boda zimesaidia kutafuta ajira kwa hawa vijana wetu, basi tupunguze kodi za pikipiki ili nao waweze kununua pikipiki na hatimaye wakapata fedha kwa ajili ya kuendeshea familia zao na maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wamesema pia juu ya kodi ya mitumba. Hakuna mtu ambaye hatambui, wote hapa ni Watanzania na wengi wetu tunatoka vijijini, wananchi wengi wanaoishi vijijini ndizo nguo wanazozitegemea. Mwananchi wa kijijini hutegemei akaenda kununua nguo dukani, anategemea mwisho wa mwezi aende kwenye mitumba apate nguo za kuweza kujisitiri, sasa sisi tunaongeza kodi. Ni vizuri tufanye kwanza utafiti, au wakati huu ambao tunataka kupeleka viwanda vya uzalishaji wa nguo basi kodi ziwe za chini, ili wananchi wengi waishio vijijini waweze kumudu kununua nguo. La sivyo wananchi wetu vijijini watashindwa kununua hata nguo tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. LEONIDAS T. GAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nami nichukue nafasi ya kwanza kabisa, kwanza kukushukuru wewe na kukupongeza sana kwa kazi nzuri unayoifanya. Tunakupa moyo usife moyo, chapa kazi, sisi tutakuunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nichukue nafasi hii nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa. Nataka nimpe moyo, kwa kawaida hakuna anayependa kulipa kodi, wote tunachukia kodi, lakini ni ukweli usiopingika kwamba bila kodi hakuna maendeleo. Kwa hiyo, endelea kuchapa kazi, yale tutakayokushauri, tutakushauri na yale mengine ambayo utaona ni muhimu kuyatekeleza basi yasimamie utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme maeneo mawili makubwa. Eneo la kwanza ni eneo la utalii. Sote tunafahamu kwamba utalii ni moja kati ya maeneo yanayoingizia sana pesa nchi mbalimbali. Na hivi sasa duniani Sekta ya Utalii ndiyo sekta kubwa ya kuingizia fedha nchi nyingi duniani. Bahati nzuri mazingira ya Tanzania ni mazuri sana kiutalii. Tunavyo vivutio vingi vya utalii, lakini naomba niseme kwamba sisi Tanzania pamoja na kuwa na vivutio vingi vya utalii, lakini bado hatujavitumia kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tunatumia sana maeneo mawili kwa utalii. Eneo la kwanza ni eneo la Mlima wa Kilimanjaro na eneo la pili ni la Mbuga za Wanyama, lakini ukienda nchi nyingine duniani, hazina milima wala mbuga za wanyama, lakini zina utalii mkubwa sana. Kwa hiyo, nashauri kwamba tujaribu kujikita kwenye maeneo mengine ya utalii ili kuikuza nchi yetu katika eneo la utalii. Yapo maeneo mengi sana kama tutaamua kujikita tutapata watalii wa kutosha sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mmoja kati ya watu waliopata bahati ya kutembea nchi mbalimbali na nimekwenda kujifunza maeneo mbalimbali jinsi wenzetu wanavyofanya utalii katika maeneo tofauti na yale tunayofanya sisi. Yako maeneo ya upandaji wa milima yenye miamba. Wanasema milima yenye miamba watu wa *technical mountain climbing*. Wanaipanda milima ile na sisi bahati nzuri tuna milima mingi sana yenye miamba, kule Songea tuna Mlima wa Matogoro ambao hauna utalii lakini tunaweza tukaingiza utalii wa kupanda milima yenye miamba tukapata nafasi kubwa sana ya kuingiza watalii nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ipo sehemu nyingine ya utalii wa historia (*Historical Sites)*. Tuna maeneo mengi sana ya kihistoria; kule Songea tuna maeneo ya Majimaji, Vita ya Majimaji ina historia yake kubwa, ukienda Kalenga kuna historia kubwa, kuna maeneo mbalimbali nchini, lakini hatujafika mahala tukayatangaza vya kutosha na tukayatumia kama maeneo ya utalii. Kwa hiyo, ushauri wangu ni kwamba tujikite kwenye maeneo mengine ya utalii, ili kuikuza nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini uko utalii wa mila na desturi. Nilipata bahati ya kwenda nchi inaitwa *Nepal,* kwenye Mji Mkuu wao pale *Kathmandu* kuna maonesho ya mila. Kuna nchi nyingi zinakwenda kuona mila za Kihindi,

historia za Kihindi; wanaingiza pesa nyingi sana kwa sababu ya utalii wa kimila. Sisi Tanzania tuna mila nyingi sana, tuna historia nyingi sana lakini hatuzitumii kwa ajili ya kuingiza watalii ndani ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, yako maeneo mengine mengi, kwa mfano kuna utalii wa Samaki *(Acquarium)* huu utalii umekua sana, ukienda Dubai saa hizi, wana samaki zaidi ya 33,000 kwenye eneo moja ambalo watalii wanakwenda kuwaona. Kuna nchi mbalimbali zina utalii wa namna hii, nenda Canada, Japan, Ujerumani sisi tuna aina nyingi sana za samaki ambazo tunaweza kuzifanyia utaratibu zikawa ni eneo moja la utalii. Kwa hiyo, naomba Serikali hebu ijaribu kuchambua, maeneo muhimu kwa ajili ya kuweka utalii katika vyanzo vingine tofauti ili kuipatia nchi yetu mapato ya kutosha yanatokana na utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, uko utalii wa wanyama; kule Kilimanjaro kuna sehemu inaitwa Ndarakwai, kuna tembo ambaye ukimweleza anakusikiliza, unampa maelekezo yoyote yale, lakini wale tembo hawatumiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Kathmandu* kuna tembo ambao wanafanyiwa utalii duniani, watu wanakwenda kupanda tembo; unapanda tembo anakupeleka kwenye maonesho mbalimbali, kwenye misitu unalipa gharama za utalii. Kwa hiyo, nafikiri bado tuna wanyama ambao tunaweza tukawatumia wakasaidia kuweza kuimarisha na kuukuza utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, vitu muhimu; ndugu yangu Shonza alikuwa ananiambia hapa, kule Mbozi kuna jiwe linaitwa Kimondo ambalo tunaweza tukalitangaza kwa nguvu sana tukaimarisha utalii. Nilikuwa nataka nilisisitize hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni juu ya Mlima Kilimanjaro. Mlima Kilimanjaro una sifa duniani kote na unatuingizia pesa nyingi sana, lakini nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri mlima ule unaingiza watu ambao hata moja ya kumi ya watu wanaotaka kuja kuuona hawaufikii kileleni. Tuna uwezo wa kuupanua ule mlima ili ufanye utalii wa watu wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa kuja Mlima Kilimanjaro ni lazima uupande, katika kuupanda zipo sifa za kupanda. Kwanza lazima upende kutembea, lakini lazima uwe na umri unaoruhusu kutembea. Kwa hiyo, watu wengi wanapenda kuja Mlima wa Kilimanjaro hawana uwezo wa afya, ama umri wake hauruhusu. Kwa hiyo tunachoweza kukifanya, kwa sababu Mlima Kilimanjaro unajulikana duniani, ni kuwahakikishia watalii kwamba watu waweza kuja kuutalii ule mlima hata bila kuupanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimjulishe, Mheshimiwa Waziri, labda niliseme na hilo kwamba nilishakuwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, nilifanya

ziara China. China nilizungumza na kampuni ya Serikali kwamba watujengee mnara. Mnara ambao wangetujengea watu ambao afya au *interest* zao haziruhusu kupanda mlima wangekuja kupanda kwenye mnara huo na tulishakubaliana wajenge mnara wa mita 600, ambapo ukishapanda una uwezo wa kuu-*view* mlima wa Kilimanjaro kwenye kiganja chako; na kwa hiyo unatembelea Mlima wa Kilimanjaro kwa kutumia mnara huo. Kwa hiyo tunaweza tukafanya hivi na tukapata watalii wengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda China iko minara ya namna hii, inajaa watu wengi sana, inatumika kwa utalii wa mjini na inasaidia sana hata kufanya shughuli za utafiti. Bado kwa kutumia mnara huo unaweza ukatengeneza *sky train* ya kukufanya ufike Mlima wa Kilimanjaro bila kupanda kwa utaratibu wa kawaida uliopo sasa. Kwa hiyo, tunaweza kuona hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana hebu Serikali ijaribu kujikita chini kuangalia namna tunavyoweza kuikuza Sekta ya Utalii ndani ya nchi yetu ili iingize mapato zaidi ya hivi sasa yanayoingia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MANSOOR S. HIRAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja ambayo ipo mbele yetu. Naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Kwimba kwa kunichagua awamu ya pili na nawaahidi sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri wa Fedha na Mipango kwa bajeti nzuri ambayo ameileta ya trilioni 29 na nusu; ambapo amepanga asilimia 40 itatumika kwenye miradi ya maendeleo. Nampongeza sana kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitachangia kwenye maeneo matatu. La kwanza, nitachangia kwenye mchango wa Msajili wa Hazina kwa bajeti kuu. Kwenye kitabu cha *volume one,* kwa bajeti ya mwaka wa kesho amepangiwa atachangia trilioni 1.3. Msajili wa Hazina anasimamia Mashirika ya Umma na Taasisi mbalimbali ambazo zina makusanyo ya zaidi ya trilioni 10 kwa mwaka. Sasa kama mashirika haya umma yanakusanya zaidi ya trilioni kumi kwa mwaka, kutoa mchango wa trilioni 1.3 ni kidogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeshauri Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango aangalie upya hili suala jinsi ya kutoza na kukusanya fedha nyingi zaidi kutoka kwenye taasisi zilizo chini ya Msajili wa Hazina ili Msajili wa Hazina aweze kuchangia trilioni tatu au zaidi, kwenye mfuko wa bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwenye kitabu hiki cha *Volume one* tunacho hapa, ni kwamba bajeti ya mwaka huu wa 2015/2016, *Airtel* walichangia Shilingi bilioni moja lakini mwaka ujao *Airtel* hawatachangia chochote, sasa sijui ni makosa au kuna suala lingine, tunaomba Waziri aweze kutufafanulia hilo, kuna tatizo gani pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine; *Tanzania Breweries* mwaka huu wa bajeti wamechangia bilioni 5.7, lakini mwaka ujao hawachangii chochote, sasa sijui *TBL* hawatachanga, labda kuna makosa hapa, tungeweza kuelewa kuna tatizo gani pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukifika kwenye suala la Mashirika ya Umma; naomba niseme Shirika moja la Umma la *Tanzania Ports Authority*. Kwenye taarifa ya Msajili wa Hazina anasema mwaka huu, Mamlaka ya Bandari Tanzania haijachangia chochote wakati taarifa ya Mamlaka ya Bandari iliyoko kwa Msajili inasema mwaka huu wamechangia bilioni 150. Huyo huyo Msajili anasema hawajachangia chochote, huku bandari inasema wamechangia bilioni 150. Sasa ni muhimu tupate ufafanuzi, kwamba hizo fedha zimechangiwa zimekwenda wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, mwaka huu huu tena Msajili wa Hazina amesema Mamlaka ya Bandari Tanzania haitachangia chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme masuala machache kuhusu bandari. Bandari hii, *Tanzania Port Authority* wana bajeti yao ambayo ipo mbele yangu hapa waliyoipeleka kwa Mhazini wa Serikali. Wanaonesha mapato na matumizi, naomba ku-*declare interest* mimi ni mjumbe kwenye Kamati ya Miundombinu. Mamlaka hii ya Bandari, mwaka jana, 2014 walipeleka shilingi bilioni 105 wakawela kwenye *fixed deposit bank*, wanasema ni pesa za ziada wanazitunza pale, huku hawachangii chochote. Mwaka wa jana wamepeleka bilioni 99 zimekwenda kwenye *fixed deposit* zinatunzwa pale wanakula riba, jumla ya Mamlaka ya Bandari Tanzania ina jumla ya bilioni 440, ziko kwenye mabenki hawana kazi nazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa huku kwenye bajeti hizo fedha hazionekani, kwenye bajeti waliopeleka hawaoneshi kama kuna fedha ziko benki. Naomba Waziri wa Fedha afuatilie hili suala, kwamba huku hazionekani hizo fedha ziko wapi? Sasa hili ni Shirika moja nimelisema hapa, tuna Mashirika mengi sana, tunaomba *CAG* afanye kazi ya ziada, azikague tuangalie fedha ngapi ziko kwenye mabenki ambazo hazioneshwi kwenye ripoti. *(Mkofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ningependa kulichangia hapa ni Deni la Taifa. Kila mwaka deni la Taifa linakua, lakini taarifa tuliyoipata kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 16 ni *paragraph* moja tu.

Ningeomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha atupe taarifa ambayo ni pana, ya kina ili tujue kwamba fedha za madeni ambazo tunazitenga kila mwaka kwenye bajeti zinatumika vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka ujao tumetenga trilioni nane kwa ajili ya madeni, mwaka jana pia tulitenga matrilioni ya fedha. Ni muhimu tupate taarifa ya hizo trilioni za fedha ambazo tunazipanga kwenye bajeti zinatumika vipi kwenye kulipa madeni ya nje na ndani, kwa sababu makandarasi na wazabuni wengi sana wa ndani wanalalamika hawajapata fedha. Ni muhimu tujue fedha zinatumika vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, baada ya Serikali ya Awamu ya Tano kuanza kazi, ndani ya miezi mitano wamelipa wakandarasi wa barabara bilioni 698. Naomba walipe na wakandarasi wanaojenga miundombinu ya maji. Naomba maji pia yapewe kipaumbele, wapeleke fedha kwenye maji, wakandarasi wanalalamika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Jimbo langu mradi mmoja wa maji umekaa unasubiri milioni 500, mabomba yamenunuliwa ya plastiki yapo juu yanasubiri kutandazwa chini, yanaoza yanapigwa jua lakini mkandarasi hajalipwa ili amalize huo mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la Deni la Taifa naomba Mheshimiwa Waziri atupe taarifa za kina zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ningependa kulisemea hapa ni Kituo cha Biashara na Huduma Kurasini. Mheshimiwa Serukamba asubuhi alilisemea vizuri, naomba niongeze machache tu. La kwanza huu mradi haueleweki unakwenda kwendaje. Mwaka juzi mwaka 2014 wakati nilipokuwa mjumbe kwenye Kamati ya Bajeti tulienda kwenye ziara pale kwenye mradi tukaenda kuangalia pale Kurasini hatukuelewa. Tuliomba tupate taarifa ya mkataba ambao wamefunga na yule mbia lakini haujapatikana mpaka leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Waziri wa Viwanda na Biashara aliangalie hili suala kwa undani zaidi, kwa sababu sisi Tanzania hatutaki Mchina aje kufanya biashara hapa ya kuuza vitu kwenye maduka. Hiyo kazi tunaweza kuifanya sisi Kariakoo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hii miradi inaonekana kuna tatizo sisi tumeshawekeza bilioni 100 kwenye fidia, sasa huyo atakapokuja kuwekeza pale lazima sisi kama Serikali tuwe na *share* kwenye kampuni hiyo, hatuwezi kuwekeza halafu tukamwachia yeye akafanya peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili kwa taarifa niliyoipata 2014 wakasema wana mpango wa kuleta vifaa kutoka China na kuanza kuuza Afrika Mashariki

na kati. Sasa wale watu wanataka kuanzisha shughuli kama ya Dubai. Unapokwenda Dubai unakutana na *dragon mart Dubai* pale watu wengi wanaifahamu. Wachina wanakaa sehemu moja wanauza vifaa vyao vyote pale, sasa lile suala sisi hapa Tanzania hatulitaki wale wakija hapa Kariakoo itafungwa na wakija hapa watatumaliza kabisa biashara itakuwa hovyo. Kwa hiyo, naomba hili suala liangaliwe upya. Kwanza huyu mwekezaji bado hajaleta chochote hapa kwa hiyo hatujachelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine walisema wanataka kuwekeza kwenye viwanda. Ushauri wangu kama wanataka kuwekeza kwenye viwanda basi wawekeze kwenye viwanda ambavyo sisi hapa nchini hatuna, wasije wakatuwekea viwanda vya biskuti wakati tunavyo wenyewe viwanda vyetu. Waweke viwanda ambavyo sisi Tanzania tuna shida navyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay atafuatiwa na Mheshimiwa Emmanuel Papian John, Mheshimiwa Seif Hamisi Said Gulamali ajiandae.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza kwa kunipa nafasi hii ili nitoe mchango wangu lakini pia niweze kuipongeza Serikali kwa jinsi ambavyo imetoa bajeti ya tofauti ya trilioni saba. Hiki ni kiwango kikubwa sana kwa nchi yetu kama ambavyo tutafikia haya malengo na kwa vyovyote mafanikio yatakuwa makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa mchango mdogo wa kuishauri Serikali. Kwanza tusimamie mapato ili tuweze kufanikiwa katika hali hii ya ukusanyaji. Nilikuwa nategemea pengine tukusanye mapato kwenye forodha, viwanda na pia tuweze kukusanya kwenye makampuni makubwa. Eneo hili tukifanikiwa tukafika hiyo asilimia mwaka huu ni dhahiri kwamba tumefaulu kwa kiasi kizuri na mwakani ni mlango wa kwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie eneo la *CAG*. Hawa wakaguzi wanafanya kazi katika mazingira magumu sana kwa sababu Mkurugenzi anayekaguliwa ndiye anayemwezesha. Nashauri kama itawezekana kitengo hiki cha ukaguzi kiweze kujitegemea katika nchi yetu kutoka ngazi ya Taifa, Mkoa na Wilaya ili tuweze kufikia malengo mazuri. Kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wamelalamikia sana hela ndogo ya *CAG,* kwa kweli kama hatujaweza kumwezesha *CAG* katika dhana nzima ya fedha, watumishi na dhana nzima ya vitendea kazi kwa vyovyote vile tunachokifanya hakipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri kule chini tuna mambo mengi sana. Kuna ya maabara, zahanati pamoja na nyumba za Walimu yameachwa. Kila mwaka tumeshindwa hata kutatua baadhi ya yale maboma. Kwa hiyo rai yangu kwetu sote ni kwamba, fedha zilizoombwa na Halmashauri hizi zifikishwe katika ngazi hizo za Halmashauri na tuweze kufuatilia. Kwa sababu hiyo tunaweza tukafika na huduma itatolewa katika ngazi hiyo ya chini na kutatua kero kwa ngazi ya Jimbo. Kwa jinsi ambavyo miradi mingi ni viporo hata miaka mitano ya sisi Wabunge inaweza kwisha hatujatatua hata kitu kimoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kama ambavyo nilizungumzia hilo, naomba utoaji wa fedha zile ambazo zinapelekwa kwenye ngazi za chini ziweze kufanya vizuri. Pia nchi yetu imekuwa na hali mbaya ya bidhaa feki. Hizi tumebaki kuteketeza kwa sababu tayari baada ya muda tunaona zimeshaingia nchini, ziko ndani ya soko, kwa hiyo kiwango hiki kinaathiri sana uchumi wa jamii na kwa hivyo hali hii inawafanya wananchi washindwe kuelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kama itawezekana wale wanaodhibiti na kuangalia ubora wa bidhaa zinazoletwa kutoka nje na zile za ndani waweze kuwa makini kuangalia ni kwa namna gani ambavyo bidhaa hizi zinadhibitiwa ili zisiwe zinavuruga soko kwa sababu tunapokwenda kuchoma au kuteketeza ni tayari wananchi wanapata hasara kubwa kiuchumi na pia wanadhurika kiafya, kwa sababu kuna madhara ya afya na kuna madhara ya kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali katika ngazi hii ya Halmashauri tungeomba ikafanye semina ya Waheshimiwa Madiwani. Miradi mingi ya ngazi za chini Waheshimiwa Madiwani hawawezi kutambua na kujua miradi hii na thamani yake kifedha. Kwa hiyo, tukiweka fedha za semina na fedha za uwezeshaji katika zile Kamati, hasa Kamati ya Uongozi ni imani yangu kwamba watatusaidia sana katika kukagua miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia bado hatujanufaika katika rasilimali gesi na mafuta kwa kuwa labda ni mwanzo, lakini naomba kwa mwaka unaokuja pia tuone ni namna gani tunanufaika katika rasilimali hizi za gesi na matuta kwa kiwango kizuri ili nchi yetu iweze kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji wanalalamika, ifike baadae huko tufike na wao tunawawezesha, tukikusanya hela vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, si vibaya tukawa na chombo kinachofuatilia ukusanyaji wa mapato katika Taifa letu. Ukusanyaji huu wa mapato sio ukusanyaji mzuri kwa sababu kwa vyovyote vile kuwaachia tu *TRA* wao ndiyo wakusanye na hatuwezi kubaini na kufanya utafiti kwa vyovyote hatutafika. Nashauri tuwe na chombo kinachoweza kufuatilia ukusanyaji wa mapato ili

kiwe kinaielekeza Serikali kufanya kile kinachowezekana. Kwa hiyo, kwa vyovyote vile mara nyingi Serikali yetu imekuwa na wakati mgumu pale ambapo mifumo ya bajeti inapokusanywa na baadaye katika matumizi, hatuna vipaumbele. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kuwe na uwiano wa vipaumbele vya matumizi ya bajeti kwa pale ambapo pesa hizi zimepatikana katika *Central Government* na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi nilipokuwa kule ngazi za Halmashauri nilikuwa nafikiri huku kuna neema, nimekuja huku vilio ni balaa. Kwa hiyo, naomba kama itawezekana kwa vyovyote ngazi hizi za chini ziweze kuletewa hela kwa kuwa wao ndiyo walio karibu sana na wananchi wetu na kwa vyovyote wasingeweza kufanya kazi hiyo na wasingeweza kuona.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine naishauri Serikali iweze kuratibu ahadi za Mheshimiwa Rais ili kwa mwaka tujue ni ahadi ngapi tumetekeleza na ahadi zipi zimebaki na kupitia Mbunge wa Jimbo na Serikali tuone basi yale yatakayotatuliwa chini ya uwezo wa Serikali yanapata kutatuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vyovyote vile katika hali hii ya nchi yetu kutafuta mapato na tunatoka trilioni 22 tunaenda 29 ni kiwango kikubwa sana na hali hii itatufikisha mahali pazuri jinsi ambavyo fedha hizi zikipatikana zitatatua kero za wananchi. Sisi tunaotoka kwenye Majimbo tuna wakati mgumu sana. Wakati wa kuomba kura unasema jamani nitajenga daraja, baadaye uchaguzi ukiisha daraja linakuwa kubwa na uwezo wa kujenga lile daraja unakosekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina ushauri kuhusu fedha za maji. Miongoni mwa maswali mengi yaliyoulizwa na Waheshimiwa Wabunge ni juu ya miradi mingi ya maji nchini. Nizungumzie uzoefu wa Jimbo la Mbulu au majimbo yote mawili ya Mbulu. Wataalam wanateua wazabuni ambao hawana fedha, hawana uwezo na kwa hivyo baadaye wale wazabuni wanashindwa kutekeleza ile miradi na tusitarajie kwamba hiyo miradi ya maji itakamilishwa kwa Juni, 30 hii siyo rahisi hata siku moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba kwa vyovyote Serikali iratibu, ipitie miradi upya, itoe maelekezo kwa ngazi za Halmashauri ili waweze kuvunja mikataba inapobidi, kwa sababu katika Jimbo la Mbulu tuna miaka miwili wananchi hawajapata huduma, lakini pia miradi imetelekezwa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nashauri, Serikali itoe maelekezo ipitie upya mikataba iweze kuondoa ile mikataba ili wananchi wapate huduma stahiki. Nia hiyo ya Serikali kusema tunalipa kile kilichokamilika ni utaratibu mzuri wa Serikali, lakini kama

hawawezi kufika na hawawezi kutekeleza ungefanyaje? Kuna miradi toka mwaka 2013 haijakamilika mpaka leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante nashukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Emmanuel John Papian atafuatiwa na Mheshimiwa Seif Khamisi Said Gulamali, Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo ajiandae.

**MHE. EMMANUEL P. JOHN:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza nampongeza Waziri wa Fedha kwa hotuba nzuri ya bajeti ambayo inatupa matumaini ya huko tunakokwenda kwa kipindi hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ninalotaka kuzungumzia ni kushukuru kwa bajeti hii kwa sababu hii bajeti itafanya Watanzania waweze kufanya kazi. Naomba na kushauri sana wabane, watafute vyanzo vingine, hata hivi ni kidogo, pesa zishindikane kupatikana Watanzania waanze kufanya kazi kwa sababu hawataki kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona *speech* ya Rais akizungumza juu ya vijana ambao wanazunguka, watu hawataki kufanya kazi. Naomba Mheshimiwa Waziri Mpango na Naibu Waziri wajitahidi wahangaike kiasi kwamba pesa iwe ngumu ili watu waamke wanatafuta pesa badala ya kufikiri kuangalia runinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna msamaha wa kodi kwenye makanisa na mashirika ambayo yanatakiwa kusamehewa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipindi hiki ni kipindi ambacho watu wengi wamekuwa wana *diverge* kodi wanakwepa kwa sababu siyo waaminifu kama zamani. Mtu anaweza kuleta kontena nne anasema hii tunajenga kanisa, ni *tiles,* ni vioo, kontena moja ndio inayofanya kazi, kontena tatu zinapigwa mtaani, halafu mkimaliza mnasema tunakwenda kusali kumbe kodi imepotea. Hiyo usibadilishe yeyote anayesema kodi ilipwe kwanza, watakapomaliza kulipa kodi atakaporejesha zile risiti kwamba hivi vitu vimetumika, basi wewe mrudishie kilicho chake lakini msamaha usiondoe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo na mifugo. Na-*declare interest* kwamba, mimi ni mkulima na ni mfugaji, si mdogo ni mkubwa. Naomba na kuzidi kusisitiza ili Watanzania watoke kwenye huu umaskini waende kufanya kazi, wafanye kazi kwa bidii watafute maisha ni lazima Benki ya Kilimo iongezewe mtaji ili tuweze kuondoa wale watu wanaosongana mijini, wanashinda vijana wenye vifua

wanatembeza nguo za akinamama za elfu mbili mbili. Ili warudi vijijini ni lazima hii benki iweze kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la matrekta. Hebu tuingizieni matrekta ya kutosha watu wetu wakope waende mashambani maana hawatalima Dar es Salaam. Tusaidieni ruzuku za pembejeo, hakikisha kwamba tunainua mashamba yote ya kilimo ambayo yanaweza kuzalisha mbegu ili mbegu tunayo-*import* zaidi ya asilimia 80, zaidi ya bilioni kadhaa zinazotoka nje zibaki hapa ndani ili kuwe na *creation* ya *employment* na watu wao watafanya kazi mashambani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa na kitengo cha kilimo-anga. Zamani tulikuwa na wataalam wazuri wa kilimo-anga ambao ma-*pilot* wetu ndio wa kwanza *East Africa* na *Central* kwa kuendesha ndege za kumwaga madawa, lakini leo hatuna *pilots,* hatuna ndege, na kesho kutwa mwezi wa tisa Kondoa inaomba chakula cha msaada. Naomba msikie hapa, tukirudi Bungeni Waziri wa chakula ataombwa chakula kupeleka Kondoa, ndege wamemaliza chakula. Niwaombe, kwenye bajeti yao wafikirie kununua ndege ya kilimo, wapelekeni vijana wetu wakasomee kuendesha ndege za kumwaga madawa Uingeza badala ya kukodi wataalam wa kuja kumwaga dawa hapa, huo ndio ushauri wangu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, *ATC*. Tunanunua ndege tunapongeza kwa mpango huo ndege na zije Watanzania wafanye kazi na shirika lifanye kazi. Naomba kushauri tangazeni nafasi ya *Chief Executive Officer* wa *ATC* ambaye atasimamia. Atoke nje hatutaki ubabaishaji kwenye hili shirika tena. Madeni yote yanayodaiwa weka pembeni wataendelea kudaiana na Serikali, wataendelea kudai mishahara huko huko shirika lianze upya, akaunti mpya, *CO* mpya, watendaji wapya, tusonge mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Hifadhi ya Mazingira. Nchi ya Tanzania ni chafu sana. Niombe kushauri wametenga pesa kwa ajili ya kupanda miti milioni kadhaa nchi nzima. Kwa nini wasifikirie ni namna gani tunaweza kufuta mifuko ya *plastic* nchi nzima ili tuokoe kwanza udongo, tuokoe ardhi, tuondoe uchafu, tuokoe magonjwa, tuokoe uhai kabla ya kupanda miti? Maana hizi *plastic bag* zimesambaa na ni nyingi sana madhara yake ni makubwa hatuwezi kuyaona leo lakini ukiangalia nchi yetu kwa uchafu huu ni mara mia tutumie *disposable paper* ambayo inaweza kwisha na udongo wetu ukabaki salama, huo ndio ushauri wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *CAG* tunaomba aongezewe pesa, ndilo jicho letu, ndilo jicho la Mheshimiwa Rais, ndilo jicho la Mheshimiwa Waziri Mkuu, ndilo jicho la Mheshimiwa Waziri wa Fedha; hiki kitengo kipewe pesa. Lakini naomba kushauri jambo, kumekuwa na mrundikano wa madeni; mara tunaangalia

yalienda wapi, yakaenda wapi miaka kumi bado *CAG* anakagua haviishi vilipanda vilishuka. Hebu mshaurini *CAG* afute haya matakataka yaliyoliwa huko nyuma, maana yameliwa na Watanzania hawa hawa wamemaliza, ayafute ili hiki kitengo kiweze kufanya kazi vizuri na kwa ufanisi. Ni kwamba kipunguziwe mzigo wa ku-*audit*. Ana-*audit* miaka kumi ishirini iliyopita huku mbele vinaliwa, huku nyuma ameshindwa kuzuia sasa afanye nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu wafute hivi vitu, Mheshimiwa Waziri afute haya matakataka yote haya yaishe tuanze upya mafaili mapya, tukamatane kwa upya, *CAG* aweze kufanya kazi kwa ukaribu vinginevyo unamfanya ana-*audit* vitu wiki mbili tatu hawezi ku-*cover* nchi kumbe ana *audit* vitu vya 2013, 2012 huko, badala yake tungekuwa tunakwenda mbele ili aweze kukabiliana na uovu ambao umetokea kwa wakati huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine ambalo nataka kushauri, hawa *auditors* wa *CAG* wangeweza hata kukabiliana na watendaji wetu wahalifu kwa wakati. Sasa *otherwise* ni kwamba anapokwenda ku-*audit* anakuta mtumishi alihama aliiba, akapandishwa cheo, akaua zaidi badala ya kuokoa pale. Watu wakamatwe kwa wakati kwa sababu tunahitaji hawa watu tuweze kuwakamata kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *TRA*. Tunaomba isaidiwe watumishi wengi wa *TRA* wanapata vitisho kutokana na walipa kodi, kudai kodi siyo kazi rahisi wamefunga roho. Hawa watumishi wetu wa *TRA* wasaidieni ili waweze kulindwa na usalama wao, *otherwise* wanaweza kuyumbishwa na wafanyabiashara na viongozi wanasiasa watendaji, mwisho wa siku wakafanya uhalifu wa kuhujumu nchi bila wao kutaka. Naomba wasaidiwe maana wanakutana na shida nyingi na maamuzi mengine wanayafanya bila wao kutaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, watakapofanya hivyo itatusaidia sisi kujua na kukagua vitu vyetu ambavyo vyote vinawezekana na makusanyo mengi yatakuwa makubwa kiasi kwamba, tutakuwa tumeweza kukusanya kiasi ambacho sisi tulikuwa tunakitarajia. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zahanati. Kiteto tumepewa zahanati tatu, sasa wale Wamasai wangu wa kule porini naenda kilomita 150 watakutana lini na dawa? Simangilo zahanati moja watakutana lini na dawa, *clinic* watakutana nayo wapi, sasa Mheshimiwa Waziri tunaomba hili suala mliangalie…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. EMMANUEL P. JOHN:** Mheshimiwa Naibu Spika, muda umekwisha? Yesu wangu! Naunga mkono hoja. (*Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Seif Khamis Said Gulamali atafuatiwa na Mheshimiwa Taska Restuta Mbogo kama muda utakuwa unatosha Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve tutaendelea naye.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi jioni ya leo kuchangia bajeti hii ya Mheshimiwa Waziri. Kwanza nampongeza Waziri kwa kazi nzuri kwa bajeti aliyoiwashilisha na tumeona asilimia 40 imetengwa kwa ajili ya kutatua kero za wananchi, fedha za maendeleo asilimia 40. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchango wangu nijielekeze kwenye ofisi ya *CAG*. Wabunge wengi wamezungumza juu ya kumpa uwezo *CAG* ili aweze kufanya kazi mimi binafsi na-*declare interest,* ni Mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali za Mitaa. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jicho letu ni *CAG,* lakini pia hata Bunge hili *CAG* ndiye jicho letu. Pamoja na wote kuwa jicho letu ni *CAG* hata Rais mwenyewe jicho lake ni *CAG*. Haiwezekani tuseme hapa kazi tu, tutenge fedha nyingi tupeleke kwenye maendeleo na sehemu mbalimbali halafu tusimtengee fedha mtu ambaye anaweza kuzikagua ili kurudisha *feedback* kwa Mheshimiwa Rais kwamba, fedha ulizopeleka zimetumiwa kwa kiwango gani kwa utaratibu mzuri au mbaya. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Mheshimiwa Rais aweze kutamba ni lazima apate *report* kutoka kwa *CAG* na ndipo ataweza kumsaidia yeye sasa kujua wapi wanaharibu na wapi wanafanya vizuri. Hivyo Ofisi ya *CAG* hiyo bajeti iliyotengwa ya bilioni 42 ambapo maombi yake yalikuwa ni zaidi ya bilioni 65, tuombe Wizara itenge fedha, siyo aje aombe, itengwe fedha kwa ajili ya utendaji kazi wake. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ameona kila Mbunge akisimama akizungumza anazungumzia uwezeshwaji wa Ofisi ya *CAG,* nafikiri ame-*take note* hapo, kwamba *CAG* inatakiwa sasa katika ku-*finalize* akapeleke fedha ili tumwezeshe huyu. Hata *PCCB* hawezi kufanya kazi bila *CAG,* haiwezekani *PCCB* afanye kazi, kwa *report* kutoka kwa nani?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapopunguza fedha za bajeti ya Ofisi ya *CAG* maana yake *LAAC* na *PAC* zinakuwa hazina kazi ya kufanya, lakini hata Rais *report* yake ya kutambua wapi kuna udhaifu atashindwa kutambua. Tunaomba sasa Wizara iangalie jinsi ya kuwasaidia hiyo Ofisi ya *CAG* kwa kuwapa fedha ya kutosha. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine nichangie kwenye hili suala; Serikali ina nia nzuri ya kuweka tozo katika *crude oil* katika alizeti, ina nia nzuri katika kukusanya mapato lakini tuangalie *outcome* yake isije kutokea kama ile ya sukari. Muda mfupi uliopita ukatokea uhaba wa sukari na mwisho wake tukaanza kufanya kutafuta njia za haraka kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashauri tunapoweka tozo hizi ambayo ilikuwa haipo mwanzo tutasababisha upungufu wa mafuta haya ambayo uhitaji wake ni zaidi ya lita laki sita na uzalishaji wetu ndani ya nchi ni karibu laki moja na nusu, hivyo, kuna asilimia 75 ya mafuta haya tunaagiza nje ya nchi. Kwa hiyo, tuangalie athari yake isije kutokea sasa kwa wauza chipsi hawa maana mafuta yanapanda bei kutokana na tozo hii au ulipaji wa kodi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafuta haya yakipanda bei hata muuza chipsi atazipandisha bei chipsi zake, hata mama ntilie anayeuza chakula pale naye atapandisha bei chakula chake. Hiyo itapelekea yule mbeba zege kununua chakula kwa mama ntilie kwa bei ya juu. Kwa hiyo tunapandisha maisha ya mtu wa chini yaende kuwa ghali zaidi hali itakayopelekea ugumu wa maisha kujitokeza kwa kasi ya ziada. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe Serikali iangalie hii tozo isije ikaja kuumiza watu wa chini. Nia ya Serikali ni nzuri; tuangalie, Mheshimiwa Rais ana uchungu sana na watu wa chini, lakini kutowekeza katika sehemu kama hizi ambazo zinawagusa moja kwa moja watu wa chini tutawaongezea ugumu badala ya kuwarahisishia maisha. Niombe Wizara ya Fedha iangalie tozo kwenye hii *crude oil* hasa kwenye mafuta ya *sun flower* na mengineyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumze lingine la maji. Tumeona jitihada za Serikali katika kutatua kero mbalimbali za nchi yetu, mfano tumeona jitihada kubwa za ujenzi wa barabara Tanzania, tumeona jitihada kubwa inayofanyika katika kutatua tatizo la umeme vijijini lakini hatujaona Serikali ikiwekeza kwa njia ya dhahiri ya dhati kabisa kutatua tatizo la maji nchini kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila Mbunge akisimama hapa anazungumza tatizo la maji, kila Mbunge akisimama maji, maji, maji, sasa kumbe ipo haja, hebu tuongeze fedha, tutenge fedha za kwetu kwa ajili ya kutatua tatizo la maji, kwa maana tuongeze. Wameshauri hapa wengine wamesema tuongeze Sh. 50/= kwenye mafuta na Mfuko wa Maji uwepo, kwa sababu miradi mingi ya maji inayotekelezwa ni fedha za wahisani, fedha zetu wenyewe hatujawekeza vya kutosha. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna uhaba wa maji, uhaba wa maji kwa mama zetu, uhaba wa maji kwa mama lishe, uhaba wa maji kwa wafugaji,

uhaba wa maji kwa kada mbalimbali ndani ya nchi yetu. Tuangalie sasa namna gani huu Mfuko wa Maji tunauweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo Sh. 50/= tubariki sasa ipitishwe, ili fedha itakayopatikana ipelekwe kwenye kutatua shida ya maji. Tukisimama hapa tunamwangalia Waziri wa Maji. Mbunge yeyote atakayesimama anazungumzia maji. Kwa hiyo, hii inaonesha suala la maji hatujalipa uzito wa hali ya juu. Sasa ni wakati wa kuhakikisha kwamba, tatizo la maji tunaliondoa ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wamezungumza wengine hapa tuna mabwawa, tuna maziwa, tuna bahari, tuna vitu vingi, lakini bado tumebaki kuwa na tatizo la maji ndani ya nchi yetu. Ukienda nchi zingine za wenzetu ambazo zina uhaba wa vyanzo vya maji wanatatua tatizo hili la maji wenyewe wakati sisi tunavyo lakini tuna tatizo la maji ndani ya nchi. Niombe Wizara iangalie namna ya kulitatua hili jambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo naweza nikachangia ni juu ya suala la bajeti. Tunatenga bajeti hapa, tunaiomba Wizara, fedha hizi ziende kwa wakati, kwa sababu fedha tunavyozipitisha hapa halafu mwisho wa siku tunakwenda kwenye mwezi Machi au Mei mwakani tunakuta asilimia tano, kuna sehemu zimepelekwa asilimia 10, asilimia saba; mwisho wa siku maana yake ile kazi kubwa tuliyoifanya na kutumia muda mrefu kuijadili ile miradi inashindwa kutekelezeka kwa wakati. Niiombe Wizara ipeleke hizi fedha kwa wakati ili miradi na yale malengo ya Serikali yaweze kutimizwa kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo nichangie pia kwenye suala zima la lugha yetu ya Kiswahili. Lugha yetu ya Kiswahili tunatambua mchango wake ndani ya nchi yetu na juzi kati nimesoma katika vyombo vya habari Zimbabwe wameanzisha somo la lugha ya Kiswahili katika mitaala yao. Je, fursa hizi Tanzania tunazitumiaje? Mabalozi wetu watumie fursa hii kwa kuwaangalia vijana wetu, vijana wetu ndiyo hivyo wana-*graduate,* wamesomea mambo haya ya kufundisha Kiswahili, lakini hatujapeleka Walimu wa kutosha nje ya nchi kwenda kufundisha lugha hii ya Kiswahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona Taifa la Kenya linapeleka watu wetu sana wanafundisha mpaka vyuo vikuu, lugha ya Kiswahili. Nilipata bahati ya kuhudhuria kongamano moja nchini Ekuador mwaka 2013. Nilikutana na mwanafunzi ametoka kusoma chuo kimojawapo nchini Marekani, akaniuliza umetokea nchi gani nikamwambia Tanzania…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naona muda wangu umekwisha. Ahsante sna na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gulamali tusaidie sisi wa kizazi kilichopita, juzi kati ndiyo nini? *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, juzi kati maana yake siku zilizopita za karibuni hapa. Ahsante. (*Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Taska Restuta Mbogo.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti ya Awamu ya Tano ya Serikali ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Kwanza kabisa napenda nimshukuru Mungu kwa kunipa uhai na leo nachangia hoja kwa mara ya kwanza kwa hii bajeti ya Serikali mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Rais mwenyewe kwa kazi nzuri anazozifanya na juhudi anazozionesha kwa kunyanyua maisha ya Watanzania. Napenda nikupongeze wewe mwenyewe kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpongeze Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Philip Mpango na Naibu wake Mheshimiwa Ashatu kwa kazi nzuri wanazozifanya. Napenda niwaambie Wabunge wenzangu kwamba, Jimbo la Mheshimiwa Philip Mpango ni Tanzania nzima si kwamba Mheshimiwa Philip Mpango hana Jimbo, Jimbo lake ni mipaka ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niwapongeze akinamama wenzangu, Wabunge wa Viti Maalum na niwaambie kwamba ninyi akinamama Wabunge wa Viti Maalum Majimbo yenu ni makubwa kuliko Wabunge wa Jimbo kwa sababu mipaka yenu ni mkoa mzima, kwa mfano wewe unatoka Mkoa wa Kigoma, ina maana wewe ni Mbunge wa Jimbo la Mkoa wa Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo napenda kuchangia bajeti hii ya Serikali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nianze kwenye elimu. Nashukuru sana Serikali ya Awamu ya Tano imetenga pesa nzuri kuboresha elimu mpaka tunaweza kupata elimu bure ambayo itashughulikia vitabu bure mashuleni, chakula bure, gharama zote za mitihani zitakuwa zinashughulikiwa na Wizara ya

Elimu. Napenda niipongeze sana Serikali kwa hilo. Hata hivyo, napenda kutoa angalizo kwa maneno machache kuhusu elimu ambayo wanafunzi wanaipata ndani ya nchi yetu ya Tanzania. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Wizara ya Elimu ingeangalia utaratibu wa kujenga shule za *kindergarten* kwenye shule zetu za *primary* ili watoto kabla hawajaingia darasa la kwanza waweze kujifundisha, kwa sababu unakuta uelewa wa mtoto Mtanzania ambaye ana miaka mitatu ni wa chini ukilinganisha na mtoto wa miaka mitatu wa *kindergarten* kutoka nchi nyingine. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba shule zetu za *primary* zijengewe darasa kwa ajili ya *kindergarten* ili watoto wawe wanapita pale *kindergarten* kabla hawajaingia kwenye elimu ya *primary school.*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naomba kuchangia juu ya tatizo la wasichana wadogo wa umri wa miaka 15 mpaka 19, ambapo imeainishwa kwenye kitabu ukurasa wa 10 kwamba, kuna ongezeko, kutoka asilimia 23 mwaka 2010 hadi kufikia asilimia 27 mwaka 2015; ambapo watoto wenye umri mdogo wa miaka 15 mpaka 19 wamekuwa wakipata mimba za utotoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iliangalie hili suala kwa makini kwa sababu baada ya miaka mitano tutajikuta tuna watoto wengi sana, Serikali itakuwa na mzigo wa kuhudumia hawa watoto, pia Serikali inakuwa na mzigo wa kuwasomesha kwa sababu watoto wengi wa aina hii wanaishia mitaani na Serikali yenyewe na nchi yetu yenyewe kama tunavyojua hatuna nyumba nyingi za kulelea hawa watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo natoa ushauri kwamba, Serikali ingezifuatilia shule za sekondari ambazo zinajengwa, hasa shule za watu binafsi, iangalie kwamba, zile shule ziwe na mabweni ya kulala wasichana. Kwa sababu unakuta shule nyingine inajengwa haina mabweni, matokeo yake wasichana wanapanga kwenye nyumba za watu binafsi, hii inapelekea kupata matatizo ya upataji mimba za utotoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia napenda Serikali iangalie suala la kubadilisha sheria ili hawa watu ambao huwa wanakatisha masomo ya watoto waweze kupewa adhabu kali. Pia naomba Serikali ingeangalia suala la kurekebisha sheria ya ndoa ya mwaka 1971 ambayo inamruhusu mtoto kuolewa akiwa na umri wa miaka 15; kwa sababu vyote hivyo ni vitu ambavyo vinamfanya yule mtoto aone kwamba yuko tayari kuingia katika majukumu hayo kwa sababu hata sheria za nchi zinamruhusu kwa upande mmoja aolewe na miaka 15 na upande mwingine zinamwita mtoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Serikali ijaribu kuzileta zile sheria zijadiliwe na wadau na kubadilishwa hasa sheria ya ndoa ya mwaka 1971, kwa sababu hatuwezi tukawa na sheria mbili ambazo zinakimbizana; sheria ya mtoto ya mwaka 2009 na sheria ya ndoa ya mwaka 1971. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba niende kwenye suala la Mkoa wangu wa Katavi. Katika Mkoa wangu wa Katavi tunayo matatizo kwa sababu mkoa ni mpya na Halmashauri nyingi ndiyo zinaanza kujengwa na Wilaya zile ambazo zimepitishwa kuwa Wilaya kwa mfano kama Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda hawajatengewa fedha kujenga zile ofisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba Serikali ijaribu kuangalia utaratibu wa kutenga fedha kwa ajili ya kujenga ofisi za Halmashauri ili ziweze kujiendesha. Kwa sasa mkoa una Halmashauri mpya za Wilaya tatu. Awali mkoa ulikuwa na Halmashauri mbili na sasa hivi una Halmashauri tatu mpya ambazo hazina ofisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wa Katavi tunao wageni (waliokuwa wakimbizi) ambao sasa hivi ni Watanzania wenzetu, wako kule mishamo na Katumba. Wageni hawa walijengewa shule na Umoja wa Mataifa. Hata hivyo zile shule hazitoshi kwa sababu wale tangu walipokuja wakiwa wakimbizi ni siku nyingi na kwamba sasa wameongezeka kwa idadi yao, hivyo, unakuta wengine wanasomea chini. Kwa hiyo naomba Serikali iangalie utaratibu wa kuangalia suala hilo na kuweza kuongeza shule kwenye Mkoa wangu wa Katavi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la mitumba. Nchi yetu ya Tanzania hatujawa na viwanda vingi vya nguo, naomba hiyo mitumba iachwe kwa sababu ndiyo nguo ambazo zinatumika kule vijijini kwetu na nyingine zilizopo ni za ghali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nizungumzie suala la kukatwa kodi kwa kiinua mgongo cha Wabunge. Naomba kuzungumzia hili suala kwa sababu Mbunge ndiye kiunganishi cha Serikali na wananchi. Mwananchi wa kawaida anapopata matatizo anampigia simu Mbunge, hawezi kumpigia simu Waziri wala hawezi kuipigia simu Serikali. Kwa hiyo, naomba suala hili liangaliwe kwa sababu mishahara yetu inakatwa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba suala la kiinua mgongo cha Mbunge lijaribu kuangaliwa ili ile kodi isikatwe kwa sababu Mbunge mshahara wake au kitu chake anachokipata si kitu ambacho anatumia peke yake, mshahara wake anatumia na watu wengi na kusaidia wananchi na yeye ndiyo kiunganishi cha Serikali pamoja na wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwananchi anapomwomba Mbunge kitu chochote amsaidie, Mbunge kama hajamsaidia anachukulia kwamba, Serikali ndiyo haijamsaidia. Naomba suala hili liangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwatetea watu wa bodaboda, kwamba kodi hiyo kutoka 45,000 kwenda 90,000 ni kubwa sana. Ukiangalia vijana wengi hawana kazi, wamemaliza shule na vijana wengi wanajihusisha na biashara ya bodaboda kuwapa tozo la sh. 90,000 kulipa kodi ni hela kwa kijana na unaweza kukuta ile bodaboda amekopeshwa anatakiwa arudishe zile pesa kwa mwenye bodaboda. Sasa si sawa kumwambia alipe 90,000 akasajili ile bodaboda, na pesa yenyewe amechukua kwa mkopo na hiyo pesa ni kubwa sana naomba tuangalie vyanzo vingine vya mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kushauri; kwa mfano Mkoa wetu wa Katavi tunao utalii mzuri, tunaye twiga mweupe ambaye hapatikani mahali popote. Naomba Waziri wa utalii amtangaze huyo twiga ili watalii waje kumwangalia yule twiga kule na waweze kuleta mapato nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watalii wanakuja kuangalia vivutio vyetu vingi, lakini kama tutazidisha kodi watalii wanaweza wakakimbia wakaenda Kenya. Pia naomba Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii ijaribu kuutangaza sana Mlima Kilimanjaro kwa sababu mara nyingi unakuta Mlima Kilimanjaro unatangazwa kwamba upo Kenya. Kwa hiyo, watalii wengi wanapokuja wanashuka Kenya na wanapakizwa kwenye mabasi kupitia Namanga kuja Tanzania...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumemaliza kipindi chetu cha kuchangia kwa kipindi cha mchana, lakini ninalo tangazo moja hapa na tangazo hili linatoka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa, anawaalika Waheshimiwa Wabunge wote kwenye futari siku ya kesho tarehe 16/6 hapa hapa Bungeni saa kumi na mbili jioni baada ya kuahirisha shughuli za Bunge tutaelekea sehemu ile ambayo tunaweza kufuturu ama sehemu ya nyuma ya jengo ukienda upande huu hivi, utapata hiyo sehemu. Ama ukiingia lile jengo la Utawala unatokeza kwa nyuma ile sehemu ambayo wageni huwa wanakuwepo pale.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu anawaalika siku ya kesho, mtakapokuja Bungeni jioni basi muwe mmejitayarisha kwa ajili ya kufuturu na Waziri Mkuu.

Baada ya tangazo hilo kuna Waheshimiwa Wabunge ambao niliwataja wakati tukisitisha shughuli za Bunge asubuhi, Wabunge wanne kwamba, wangechangia mchana lakini muda wetu haukutosha, kwa hiyo watachangia kesho. Nao ni Rose Cyprian Tweve, Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, Mheshimiwa Mboni Mohamed Mhita na Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka siku ya kesho Alhamisi tarehe 16 Juni, saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.00 Jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi, Tarehe 16 Juni, 2016, Saa Tatu Asubuhi)*